

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 9 Novemba, 2012**

(Mkutano Ullanza Saa Tatoo Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza Maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Betty Eliezer Mchangu, atauliza swali la kwanza leo.

Na. 106

**Kuboresha Majengo, Vitendeakazi na Watumishi wa Hospitali Kilimanjaro**

**MHE. BETTY E. MACHANGU** aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Mawenzi Mkoani Kilimanjaro inahudumia wagonjwa zaidi ya milioni 2 lakini ina matatizo makubwa kama vile ukosefu wa chumba cha upasuaji, chumba cha wagonjwa mahututi (ICU), Martenity Ward, jengo la magonjwa ya dharura na jengo la akina mama wajawazito (Kujitazamia).

(a) Serikali itaweka lini majengo hayo na kurejesha huduma stahili.

(b) Je, Serikali ipo tayari kuziwezesha Hospitali za St. Joseph na Machame kupata vitendeakazi na watumishi ili zisaidie Hospitali ya Mkoa kutoa huduma kwa wananchi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
(TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba sehemu kubwa ya miundombinu ya Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi ni chakavu. Katika mwaka 2012/2013, sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro imeweka kipaumbele na kuelekeza fedha zote za miradi ya maendeleo kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Jumla ya shilingi milioni 744.2 zitatumika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la upasuaji.

Mheshimiwa Spika, jengo wa wodi ya wazazi ambalo limefika ghorofa ya tatu linahitaji kiasi cha shilingi bilioni 8 ili kukamilika ambapo shilingi bilioni 6 ni za kukamilisha ujenzi na shilingi bilioni 2 ni za ununuza wa vifaa. Maombi maalum ya fedha hizi tayari yamewasilishwa Hazina na ukamilishaji wa miradi hii ni kipaumbele cha Mkoa katika mpango wake wa kwanza wa miaka mitano 2011/2012-2015/2016. Aidha ni vizuri ikaeleweka kwamba kutafuta wahisani wa ndani na nje itasaidia sana kukwamua mradi huu kila mwaka.

(a) Mheshimiwa Spika, hospitali ya St Joseph ilipandishwa hadhi na kuwa Hospitali Teule kuanzia mwaka 2009 ambapo inapata mgao wa asilimia 30 ya fedha za *Basket Fund*. Katika mwaka 2012/2013 Hospitali hii itapokea shilingi milioni 100.6 kutokana na fedha za *Basket Fund*. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa dawa na vifaa tiba kutoka MSD ambapo katika mwaka 2011/2012 ilipata jumla ya shilingi milioni 67.2 na Watumishi 71 walilipwa mishahara na Serikali pamoja na *On call Allowance*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Hospitali Teule ya Machame, Serikali inatoa asilimia 15 ya Fedha za *Basket Fund* kwa ajili ya dawa.

Vilevile Hospitali inapata *Bed Grant* na mwaka 2011/2012 ilipata shilingi milioni 17.8. Aidha, vifaa tiba vinatolewa kutoka MSD ambapo katika mwaka 2012/2013 Hospitali inatarajia kupokea vifaa tiba/dawa vyenye thamani ya shilingi 66.1. Watumishi 55 wanalipwa mishahara na Serikali pamoja na *On call allowance*.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mawenzi ilifanywa ni Hospitali ya Rufaa na kawaida Hospitali za Rufaa zinatakiwa kuwa na madaktari bingwa katika fani zote, ziwe na vifaa kama X-ray zaidi ya moja, ziwe na vifaa kama *Utra sound*.

Je, Serikali ina haja gani ya kupandisha hadhi Hospitali hii na nyinginezo katika nchi hii wakati yenye haiwezi kuzipa hadhi ya Hospitali za Rufaa.

Mgombea wa Urais wa Chama cha Mapinduzi mwaka 2005 alitaja Hospitali ya KCMC kuwa ni *specialized Hospital*, lakini Hospitali hii inatibu wagonjwa wa Ukanda wa Kaskazini nchi za Jirani na wagonjwa kutoka Mikoa mingine. (*Makofii*)

Nilivyokuwa ninasema Mheshimiwa Rwakatare jana Hospitali hii ya KCMC haina mashine muhimu kama ya CT SCAN mgonjwa akienda KCMC anaandikiwa na kumuona daktari bingwa anaandikiwa akafanye kipimo cha CT SCAN apande basi aende Arusha Agha Khan au Seriani kwa bei aghali sana na ikiwa yeze hana Ndugu Arusha akodishe nyumba ya kulala halafu afanye CT SCAN, arudi Moshi na kama siyo Mkazi wa Kilimanjaro akodishe nyumba alale ili kesho yake amwone Daktari KCMC.

Mheshimiwa Spika, haya ni mateso kwa wananchi ni kwa nini Serikali isiweke vifaa muhimu katika mahospitali na kama wanaponunua hivi vifaa muhimu au kifaa cha maana kama CT SCAN kifaa aghali, kwa nini yale manunuzi yasijumuise Mikataba ya watu wetu kwenda kuwa trained ili waweze kurekebisha hivi vifaa vinapoharibika.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Betty kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Wanasema hawakusikii ongeza kwa sauti.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Hospitali ya KCMC ina hadi ya Hospitali ya Kanda yaani Zonal Hospital na hadhi yake ni kwa 25% kuwa ni specialized Hospital na 75% kuwa ni Hospitali ya Rufaa katika eneo hilo la Kanda, Mara baada ya Hospitali yoyote kupandishwa Hadhi inaanza kufanya kazi mara moja katika hadhi iliyopandishwa nayo mapungufu yanayokuwepo ni mapungufu ambayo yanaendelezwa kuboreshwa, kadiri hali inavyoweza kuwa sahihi kwa Serikali kuweza kufanikisha kuweka wataalam, kuweka vifaa na kuweka vifaa Tiba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Hivyo Hospitali ya KCMC ina hadhi sawasawa katika ngazi iliyotakiwa kuwa nayo ambayo ni Zonal Hospital na inafanya kazi katika ngazi hiyo ya Zonal Hospital. Tatizo la wagonjwa kupewa Rufaa kwa ajili ya vipimo kwa mfano kama CT SCAN na kutakiwa kusafiri hili ni eneo ambalo ni muhimu kutokana na unyeti na ughali wa mashine yenye ambayo tunaizungumzia.

Ni muhimu kuwa na CT SCAN karibu katika Zonal Hospital zote lakini pale ambapo uwezo unakuwa ni mdogo basi Zonal Hospital ambayo itakuwa na CT SCAN mgonjwa anaweza kusafirishwa kwenda katika eneo hilo na hivi ndivyo ilivyo na Serikali imo katika jitihada za kuwezesha Hospitali yetu ya Muhimbili, Bugando, Mbeya na hata hiyo ya KCMC zote kuwa na vifaa maalum kwa ajili ya kuwezesha vipimo vyote kuweza kufanyika katika sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, hata hapa Dodoma hivi juzi tu tumetembelea kituo cha Diagnostic Center cha University of Dodoma ambacho kitakuwa na vifaa vingi vya kisasa ambavyo vitawezesha utaalama wa kuweza kupima karibu magonjwa mengi uweze kufanyika pale pamoja na mambo ya figo pamoja na CT SCAN, MRI na mambo mengineyo. Ninachojaribu kusema hapa ni kwamba vifaa kama hivyo vinatakiwa kuwepo katika maeneo yote uhaba wake unaenda kutokana na uwezo wa Serikali katika wakati husika.

Mheshimiwa Spika, suala la unaponunua mashine kwa nini usiingie mkataba na wataalam waliokuuzia ili kufanya matengenezo ya hizo mashine ni kuwa mikataba hii huwa tunaingia na kipindi cha mwaka jana Serikali iliingia mkataba ule Wizarani moja kwa moja.

Lakini kwa hivi sasa tunashauri mashine inaponunuliwa basi hospitali husika hasa katika hizo Hospitali kubwa ziingie mkataba na mtu aliye supply hiyo mashine ili aweze kufanya ukarabati na kuhakikisha kuwa service ya mashine hiyo inafanyika mara kwa mara na inadumu.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri tulikwenda naye kutembelea Hospitali ya Mawenzi na ye ye mwenyewe alliona mazingira ya Hospitali ilivyokuwa mbaya na majengo ya wodi ya wazazi na theater.

Je, Serikali haioni kuwa sasa imefika wakati muafaka wa kutafuta fedha hizo ili kumalizia majengo yale kwasababu gharama zinazidi kupanda siku hadi siku? Ninamuomba Waziri ambaye anatoka Mkoa huo atupatie majibu. (Makofi)

**SPIKA:** Huyu Mheshimiwa Grace Kiwelu anauliza hata asingesimama ningemwita aulize swali na swali lake ninajua lingekuwa Maternity Ward.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema kuwa yalitoka maelekezo hapa kuwa twende hospitali ya Mawenzi kwenda kuangalia hali yake na hili swali siyo mara ya kwanza tunalijibu hapa tumelijibu mara nyingi. Mheshimiwa Owenya amesimama hapa ameuliza swali hili na Mheshimiwa Suzan naye amewahi kuulizia na tulikwenda wote pale. Hii wodi inayozungumzwa hapa ukichukua hela zote zinazohitajika pale kwa ajili ya kujenga hiyo wodi ni bilioni nane yaani kwanza tupate hiyo picha ni bilioni nane na Mheshimiwa Kiwelu anafahamu tulikwenda wote pale.

Mheshimiwa Spika, sasa Hospitali ile kuonyesha umuhimu huu ambao Wabunge wanazungumzia katika *Reginal Consultative Committee* tuliviyokutana pale hela zote za development tuliamua kuwa zipelekwe katika Hospitali hii kwa ajili ya shughuli hizi zinazozungumzwa hapa na ndicho tulicho jibu hapa.

Kwa vyovypole vile itakavyokuwa ukisema kuwa utachukua bilioni sijui tutazipata wapi tulichokisema humu ndani ni kwamba kuna haja ya kukaa sisi wote kwa pamoja tujaribu kufanya hata andiko twende kwenye *special request* tuzungumze na Wizara ya fedha ili hela hii iweze kupatikana hapa.

Ninachotaka kusema ni kweli kuwa Mheshimiwa Kiwelu anachokisema hapa kuwa jengo lile limekaa pale kama sorvenia hakuna kinachoendelea pale tujitahidi wote pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Kilimanjaro tuone kwamba tunaiondoa Hospitali kutoka pale na mimi ni mdau muhimu kama anavyosema kutoka Wilaya ya Siha na ni *referral hospital* kwa Mkoa kwa Mkoa wetu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuendelee majibu yetu yalikuwa mengi na marefu kwa hiyo tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa Moses Machali, atauliza swali hilo.

Na. 107

#### **Ubaguzi kwa Walimu Wanaojiendeleza Kitaaluma**

**MHE. MOSSES J. MACHALI** aliuliza:-

Kwa nini Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu huwabagua walimu wanaojiendeleza kwenye Vyuo mbalimbali kwa kutowapatia ada na katika suala zima la kuwapatia ruhusa kwenda masomoni?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Machali, Mbunge wa Kasulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma Mwajiri anawajibu wa kusimamia na kumwendeleza Mtumishi kitaaluma.

Mtumishi anayeajiriwa kwa mara ya kwanza anaruhusiwa kwenda masomoni baada ya kufanya kazi kwa muda usiopungua miaka miwili ikiwemo kuthibitishwa kazini. Mtumishi

anayejiendeleza ataruhusiwa kujinga na mafunzo mengine baada ya kufanya kazi muda usiopungua miaka miwili baada ya kupata mafunzo ya awali.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa walimu kwenda masomoni huratibiwa na Halmashauri husika kwa kubainisha mahitaji ya mafunzo ya walimu kitaaluma, kuandaa mpango wa mafunzo, kutenga fedha na kuhakiki ikama kujiridhisha kuwa rasilimali watu inayoondoka haiathiri nguvu kazi inayobaki katika kutoa elimu kwa wanafunzi walioko shulenii.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizopo na ambazo zinasababisha migongano kati ya walimu na waajiri katika eneo la ruhusa na kugharamiwa masomo na baadhi ya walimu kuomba kujijendezeza katika vyuo bila kuwasiliana na waajiri, kuomba kujijendezeza katika fani zisizo za ualimu, kuomba kwenda masomoni kabla hawajathibitishwa kazini, kuendelea na masomo baada ya kuhitimu bila kibali cha mwajiri na kwenda masomoni bila ruhusa (kutoroka).

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu wako walimu 32 ambaao walikwenda masomoni bila ruhusa na mashauri yao kipelekwa katika Mamlaka ya nidhamu na ajira. Kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba kuwasisitiza Wakurugenzi wote kuhakikisha wanaandaa mpango wa mafunzo kwa Watumishi unaotekelzeza ili watumishi waweze kuhudumiwa inavyostahili. Utaratibu huu ukizingatiwa ni wazi kuwa hakutakuwa na malalamiko ya upendeleo katika kuratibu ruhusa za watumishi kwenda masomoni.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wako baadhi ya walimu ambaao walipata ruhusa ya kwenda kusoma halafu baada ya kumaliza masomo yao mwaka huohuo waliomaliza kusoma walipewa ruhusa na kwenda tena kusoma kozi nydingine, halafu watu ambaao wamefanya kazi kwa muda mrefu wamekuwa wakinyimwa ruhusa. Serikali ikiweza kupatiwa ushahidi wa aina hiyo itachukua hatua gani? Hilo ni swalii la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa mujibu wa Public Service Regulation ya mwaka 2003 ina state wazi kuwa Mwajiri anapomruhusu Mtumishi wa Umma kama Mwalimu na wengineo kwenda masomoni ni sharti kuwagharamia masomo yao, lakini hivi karibuni katika maeneo kama ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kumejitokeza silka na hulka kwa waajiri kuwapatia mikataba kwamba waji-commit kuwa watajisomesha. Ningependa kupata kauli ya Serikali uhalali huu wa kuwataka Watumishi wajisomeshe unatoka wapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, Ninaomba kujibu naswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Moses Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninataka kueleza tu kuwa utaratibu huo wa kwenda kusoma na kuruhusiwa tena kabla hajamaliza kipindi cha miaka miwili kama nilivyoleza kwenye jibu la msingi hilo ni kosa, na kwa hiyo kama ni kosa taratibu za Kisheria zitatumika ili kuweza kupitia wale wote ambaao hawawezi kufuata Kanuni hizo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, sharti la kumgharamia Mtumishi kama nilivyoleza kwenye jibu la msingi ni kwamba Mtumishi yoyote anayetaka kwenda kusoma sharti aombe ruhusa kwa Mwajiri wake ili Mwajiri ajiridhishe ya kwamba kiasi cha fedha alizozitenga kwa ajili ya kugharamia watumishi kinatosha akiwemo na huyo aliyeomba ruhusa. Lakini kama hakitoshi Mwajiri anao uwezo wa kumwambia kwa mwaka huu Fedha iliyopo ni kwa ajili ya walimu

kadhaa kadiri alivyopanga na orodha ambayo ipo kwa namna ambavyo fedha ametenga kwenye eneo lake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kuna Mtumishi analazimisha kwenda kusoma bado ataambiya jibu la msingi kwamba hatuna Bajeti ya kugharamia kwa sababu ni haki ya Mtumishi kugharamiwa na Serikali yake. Sasa kama atakuwa na namna nyingine kuwa ana-sponsorship pengine anaweza kuruhusiwa lakini pia ataruhusiwa kama huko anakotoka ikama ya Rasilimali watu inatosha yeche kusoma katika kipindi hicho. (Makof)

**SPIKA:** Tunaendelea na Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu Mheshimiwa Moza Abeid, atauliza swali hilo.

Na. 108

### **Kutofikiwa kwa Malengo ya Milenia**

**MHE. MOZA ABEID SAIDY** aliuliza:-

Kuna malengo manane ya millenia (MDGs) ambayo Dunia imekadiria kuyafikia ifikapo mwaka 2012:-

(a) Je, kwa sasa Tanzania iko katika hatua gani kuyafikia hayo, hasa ikizingatiwa kuwa huu ni mwaka, 2012?

(b) Je, kuna tathimini yoyote iliyokwishafanyika kuhusu malengo hayo na je, tathmini hiyo itawashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Wabunge?

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa nane, kikao cha Ishirini na tatu cha tarehe 13 Julai, 2012 nilijibu swali Namba 189 liliolizwa na Mheshimiwa Salum Khalafani Barwany, Mbybge wa Lindi Mjini, liliolusiana na kutofikiwa kwa Malengo ya Millenia ambalo lina mantiki ileile na hili alilouliza Mheshimiwa Moza Abeid Saidy. Ninapenda sasa kumjibu Mheshimiwa Moza Abeid Saidy kwa kurejea kwangu majibu yangu niliyokuwa nimeyatoa hapo awali kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania inaelekea kufikia malengo ya Millenia yanayohusiana na Elimu ya Msingi (MMDG 2), Usawa wa Jinsia (MDG 3), baadhi ya shabaha za lengo la kupambana na maambukizi ya VVU na UKIMWI (MDG 6), na baadhi ya viashiria vilivypo chini ya Malengo kuhusu Mazingira Endelevu (MDG 7). Hata hivyo Tanzania ipo nyuma katika baadhi ya viashiria vya Malengo ya Millenia hasa kwa Shabaha zinazohusu Malengo Na.1 Na. 5 na Na. 8.

Mheshimiwa Spika, katika malengo 8 vya Millenia, kila lengo lina shabaha zaidi ya moja katika lengo moja baadhi ya shabaha zinaweza kufikiwa, wakati huo huo shabaha nyingine kutokana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza ambazo ni pamoja na:-

Ukuaji mdogo wa sekta ya Kilimo (4.2%), mabadiliko ya tabia ya nchi, kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu (2.9) na kupungua kwa misaada kutoka kwa wahisani wa maendeleo pamoja na kuchelewa kutimiza ahadi zao. Serikali imejipanga kutatua

changamoto hizo kuitia kilimo kwanza na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016).

(b) Mheshimiwa Spika, Tathimini ya awali kuhusu malengo hayo kwa Tanzania ilifanyika mwaka 2010 na ilishirikisha wadau mbalimbali kutoka katika idara na Taasisi za Serikali.

Tathmini hiyo inaonyesha maeneo ambayo itafikiwa na maeneo ambayo yanaweza yasifikasiwe pamoja na changamoto zake. Tathmini hii inapatikana tovuti ya Idara ya kuondoa umasikini <http://www.povertymonitoring.go.tz>. Ni matarajio yangu kuwa tathmini ijayo itawashirikisha wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. (Makof)

**MHE. MOZA ABEID SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kumwuliza Waziri swalii la nyongeza.

- (a) Kwa kuwa, tathmini ilifanyika mwaka 2010. Je, malengo yalifikasiwa?
- (b) Kwa kuwa, eneo la tatu limezungumzia kuwawezesha akina Mama na Jinsia.

Je, imefikia malengo hayo na kama bado kuna changamoto gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu ya msingi, yapo malengo ambayo au yamefikiwa au yanakaribiiwa kufikiwa na kwa hali tulioifiki hapo na kwa miaka iliyobaki, tunadhani malengo ambayo tuna nafuu nayo yanaweza yakafikiwa.

Lakini nimesema katika jibu la msingi kwamba yapo maeneo kama *Millenia Goal* Na. 1 ambayo hatutaweza kuyafikia kwa sababu ya matatizo ambayo nimeyaeleza yanayotokana na ukuaji mdogo wa sekta ya Kilimo. Lakini jitihada zinaendelea na mpango wa maendeleo umeweka malengo ambayo yanaweza kusaidia kusogeza ingawa hatuvezi kufikia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MDG inayohusiana na Jinsia, nimeshaeleza kwamba tumefikia kwa kiwango kizuri zaidi cha mafanikio katika eneo hilo hasa ukizingatia kwamba tumeweza kuongeza idadi ya akina mama wanaoingia katika shule za Msingi na Sekondari na uviano sasa kati ya watoto wa kike na wa kiume wanaoingia Sekondari ni asilimia mia moja. Kwa hiyo, kwa kweli ni kama tumeshafikia kwa upande huo.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna fursa ambazo Tanzania imezitoa kwa jinsia ya Kike na hasa katika kuongeza idadi ya akina mama katika maeneo yanayotoa maamuzi, ikiwemo Bunge ambapo sasa asilimia zaidi ya 30 ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano ni wanawake. Kwa hiyo tumepeiga hatua kubwa. (Makof)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, haya malengo nane (8) ya millennia yana vigezo vyake vinavyotakiwa kufikiwa yaani ukififikia labda asilimia 50 au 60 angalau uwe umefikia na ni nchi wanachama wote na kwa kuwa, malengo haya yote kuanzia la kwanza la kupunguza umaskini, elimu ya

msingi kwa wote, namna ya kuwawezesha akina mama na usawa wa kijinsia mpaka la mwisho la Global Partnership.

Je, isingekuwa ni vema kwa Serikali kutoa takwimu sahihi kwamba wakati huu tulipofikia ni asilimia ngapi tumefikia kwenye kila lengo kwa viwango ambavyo tumekubaliana kimataifa ili Taifa letu tujue tumeshafikia hatua gani ya utekelezaji wa malengo haya ya Millenia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi, ziko *millennia goals* ambazo tumezifikia na asilimia zake zipo. Kwa mfano Millenia inayohusiana na elimu ya msingi tumekwishafikia asilimia 94.5 ya kuandikisha watoto wote wanaostahili kuingia darasani. Kwa hiyo, upande mmoja takwimu zake ndiyo hizo.

Lakini vile vile liko lengo la usawa wa kijinsia ambalo linasema tumeshafikia asilimia karibu mia moja kwa upande mmoja na bado jitihada zinaendelea kwa upande huo kwa sababu hili ni pana, linahusiana na kushirikisha jinsia zote katika maamuzi. Nimetoa Bunge kama mfano ambapo kuna asilimia 36 mpaka sasa hivi na jitihada bado zinaendelea na tunaandika Katiba mpya huenda ikaleta hamsini kwa hamsini. Kwa hiyo, jitihada zinaendelea na takwimu zipo.

Mheshimiwa Spika, vile vile zipo takwimu zinazohusiana na vifo vya watoto ambapo vimeshuka kutoka watoto 112 kwa watoto 1000 wanaozaliwa mpaka kufikia 51. Kwa hiyo, unaweza ukaona hatua ambayo tumeipiga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini bado tuna tatizo kwa upande wa vifo vya akina mama wajawazito ambao bado tupo nyuma kwa sababu miundombinu na huduma za afya hazijawa karibu sana na akina mama. Kwa hiyo, bado idadi ya vifo vya akina mama wajawazito vipo juu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo zipo takwimu ambazo Mheshimiwa Mbatia akizitaka tunaweza tukampa tathmini nzima kuonesha tupo wapi mpaka hivi sasa.

**SPIKA:** Nadhani umesema ile website ndiyo waki-download wataipata. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 109

**Mshauri Mwelekezi wa Uchangiaji wa Ugawaji  
Mapato ya Serikali Mbili**

**MHE. ASHA MOHAMED OMARY** aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliajiri Mshauri Mwelekezi wa Mambo ya Uchangiaji na Ugawaji wa Mapato kati ya Serikali mbili:-

(a) Je, ni maamuzi gani yamefikiwa baada ya ripoti ya Mshauri huyo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba wananchi wa Zanzibar wanazidi kukerwa na Muungano kwa kukosa maamuzi katika kushughulikia kero za Muungano?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali Na. 109 liloulizwa na Mheshimiwa Asha Mohamed Omary, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mshauri aliyewekwa na Serikali ya SMT na SMZ ni Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo ipo kutokana na Ibara ya 134 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume hiyo ilishatoa mapendeleko Serikalini ya Vigezo vya kugawana mapato na kuchangia ghamama za Muungano. Kwa sasa Serikali zetu zote mbili bado zinalifanya kazi suala hili.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuchelewa kukamilishwa kwa utatuzi wa kero za Muungano, kunawaudhi sana Watanzania na siyo Wazanzibari peke yao.

Hata hivyo, Serikali zetu mbili zina nia ya dhati ya kushughulikia changamoto za Muungano. Lakini kwa kuwa masuala haya yanagusa maslahi ya Taifa na wananchi wa pande zote mbili, Serikali zetu zinahitaji kuwa na umakini mkubwa katika kufanya maamuzi ya masuala haya.

**MHE. ASHA MOHAMED OMARY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Waziri napenda kumwuuiliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, siku zote ngojangoja huumiza matumbo. Je, Waziri anaweza kuwambia Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla ni lini suala hili litapatiwa ufumbuzi? (Makof)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, siko kwenye position sasa hivi ya kumwambia lini, lakini suala hili lilianza mbali. Lilianza na vikao vya watalaam, tumekwenda vikao vya Makatibu Wakuu, limepitia kwa Mawaziri na sasa lipo katika vikao vya juu kwa maamuzi. Si muda mrefu maamuzi ya maswali haya yatakuwa yamepatikana, limekwenda hatua kwa hatua. (Makof)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika ahsante sana, Waziri anakubali kwamba majibu haya anayoyatoa katika Bunge hili yameshatolewa tokea Bunge hili lianze kwa sababu hili ni suala la Kikatiba na mpaka sasa Serikali bado zinaendelea kuvunja Kifungu cha msingi sana cha Katiba.

Je, haoni sasa ni muafaka baada ya muda mrefu sana na majibu haya haya hayajabadilika hata siku moja ndani ya Bunge hili, uka- refer kwamba Serikali ilishatoa ahadi kwa kutoka kwa Mawaziri wa Fedha kwamba Bajeti inayokuja fomula hii itakuwa tayari.

Je, huoni ni dhambi kubwa sana kuendelea kuvunja Katiba ya nchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mara mbili tatu, tumekuwa tukijibu kwamba suala hili linafanyiwa kazi na katika kufanyiwa kazi ni kuititia hatua zile ambazo nimezitaja kuanzia kwa Watalaam, Makatibu Wakuu, Mawaziri na sasa kama nilivyosema liko katika hatua za vikao vya juu kwa ajili ya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad amesema kwamba kulikuwa na ahadi ya Waziri wa Fedha kwamba Bajeti ijayo suala hili litakuwa limefanyiwa kazi, naomba tusubiri Bajeti ijayo nina hakika Wizara ya Fedha watakuwa wamelifanya kazi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize na mimi swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Wazanzibar wanaruhusiwa na wanapata Viwanja huku Tanzania Bara na wanaishi huku na Watanzania Bara hawapati Viwanja Zanzibar wala hawaishi ukiwaondoa wale Wanyamwezi waliokwenda zamani.

Je, Serikali halioni kwamba hii ni kero ambayo Wazanzibar wanaishi huku kwa sababu ni kwao na Watanzania Bara hawaishi Zanzibar? (Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Wamasai wamejaa kule!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Laizer angefanya safari ya kwenda Zanzibar na akaona mchanganyiko wa Watanzania ulivyo kule.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tumezoea kuwaona Wamasai kwenye picha lakini sasa tuna wamasai katika kila kona ya Zanzibar na wenyewe wanaji-identify kama Wazanzibar na wanaishi vizuri tu. Ahsante sana. (Kicheko/Makofi)

**SPIKA:** Ndiyo maana kuna haja ya kuendelea na Muungano. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 110

#### **Kero za Muungano**

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS** aliuliza:-

Serikali inayo dhamira njema ya kuondoa kero a Muungano kwa kuunda Kamati Maalum inayoongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye ni Kiongozi wa pili katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano:-

(a) Je, hadi sasa ni kero ngapi za Muungano tayari zimepata ufumbuzi kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar?

(b) Je, vikao vya kuondoa kero za Muungano mwaka huu 2012 vimeshafanyika vingapi Tanzania Bara na vingapi Tanzania Zanzibar?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali Na. 110 liloulizwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2006 Serikali zetu zilianza kufanya kazi kero 13 na katika kero 13 kero 7 zimepatiwa ufumbuzi kabisa. Katika mwaka 2008 kero mbili nyingine zilijitokeza nazo zikafanyiwa kazi na kumalizika kabisa na kufanya jumla ya kero zilizofanyiwa kazi kuwa tisa kuanzia 2006 mpaka mwaka 2012.

Kero mbili zipo katika hatua ya mwisho moja ni hii ya Watumishi wa Zanzibar katika taasisi za Muungano ambayo vikao vya Mawaziri wameshatoa Baraka zao na sasa tunasubiri kikao cha Makamu wa Rais kuridhia ili iweze kutoka kwenye kero ambazo hazijafanyiwa kazi na kufanya ziwe kero kumi.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ni suala la usajili wa Vyombo vya Moto ambalo nalo kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano linatungiwa sheria mpya chini ya Wizara ya Ujenzi ambayo zile tofauti zilizoonekana zitarekebishwa katika sheria hiyo mpya, na kwa upande wa SMZ wao wanaendelea na marekebisho ya sheria za usajili wa vyombo vya moto kama tulivokubaliana awali.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2012, Ofisi yetu imeratibu kikao kimoja cha Kamati ya Pamoja ya SMT/SMZ kilichofanyika tarehe 28 Januari, 2012 Dar es Salaam. Kikao hiki kilitanguliwa na vikao viwili (2) vya kisekta ambavyo vilijadili mambo ya sekta za fedha, usajili wa Vyombo vya Moto, mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, Bili kubwa ya umeme kutoka TANESCO na ZECO na pamoja na shughuli za Tume ya Pamoja ya Fedha.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika ahsante, kwanza sina budi kumpongeza kwa jibu lake zuri lillotoa taswira nzuri na mwanana ambayo inafahamika. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, vikao hivi vinashughulikiwa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Makamu wa Rais SMT na Makamu wa Pili wa Rais SMZ, na viongozi hawa mara nyingi wanakuwa na majukumu mengi wanashindwa hata kukutana mara kwa mara wakaweza kuendeleza shughuli hii.

Je, Waziri ningeshauri kwamba kwanini vikao hivi visikae kisekta ambapo wao ndiyo wanaelewa nini tatizo la suala hili na wakaweza kutanzua masuala haya na yakaweza kumalizika ili kuondoa bugudha kwa wananchi?

(b) Kwa kuwa, tayari katika maelezo yako mama umeelezea kwmaba baadhi ya kero zimeshaptiwa ufumbuzi.

Je, Waziri ulitoa taarifa hizi kwa wananchi ili kuwaelezea nini kilichotekelawa au nini kilichobakia kwani haya tayari umeshatolea ufumbuzi au yameshaptiwa ufumbuzi utakuta haya haya tunayarejea kwa sababu taarifa kamili wananchi hawajazipata.

Je, utachukua njia gani ya kuweza kuwafikishia wananchi maelezo hayo? (Makof)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vikao vya juu vinaongozwa na Viongozi Wakuu wa Serikali na Viongozi hawa ni kweli kwamba wana shughuli nyingi. Lakini kwa mwaka tumewapangia vikao viwili tu. Vikao hivi ni vya kuridhia au kushauri vinginevyo yale yaliyokubaliwa kwenye vikao vya kisekta.

Nataka nimhakikishie Mbunge kwamba kama nilivyojibu katika jibu mama kwamba kikao kimoja cha Makamu wa Rais kilitanguliwa na vikao saba vya kisekta. Kwa sababu katika vikao vya kisekta ndiko tunakopata maamuzi ya issue zenyewe.

Kwa hiyo, ushauri wake tumeupokea lakini ndivyo inavyofanyika, kwamba kunatangulia vikao vya kisekta kabla ya kile kikubwa cha Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni taarifa kwa wananchi, nataka nichukue nafasi hii kusema kwamba, Ofisi yetu ya Makamu wa Rais inajitahidi sana kupitia vijarida, majarida ya Muungano

wetu na vipeperushi vidogo vidogo, lakini pia kupitia televisheni zilizopo hapa nchini. Tumejitätidi sana kutoa taarifa hizi kwa wananchi.

Kwa hiyo, wale ambao wamekuwa makini katika kusoma na kusikiliza basi taarifa hizi wanazijua vema.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, kuna utaratibu kwa wageni wote au watu wote wanaotoka nje ya nchi hii wanapotaka kuingia Tanzania kwa kutumia usafiri wao, wanaruhusiwa kuingia hapa kwa kutumia kitu kinachoitwa *foreign permit*.

Je, kuna utaratibu gani kwa Mzanzibari au Mtanzania kutoka Zanzibar anapotaka kuingia na gari yake hapa ambayo kwa sasa inavyoiezwa Mzanzibari analazimika kuweka *deposit* ili aweze kuingia na gari yake katika nchi yake mwenyewe ya Tanzania?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu awali kwamba moja katika changamoto tunazopata katika Muungano ni suala la usajili wa vyombo vya moto.

Ni kweli kwamba gari zinazotoka Tanzania Bara zinaingia Zanzibar bila kuulizwa lakini Sheria zilizopo Tanzania Bara zinahesabu gari zinazotoka Zanzibar ni kama gari za kigeni.

Suala hili limekuwa changamoto kwa siku nyingi na kama nilivyosema kwamba tumelifanya kazi, tulifiki pahali kurekebisha sheria zilizopo, kwa Zanzibar imekuwa rahisi kurekebisha Sheria zilizopo lakini kwa upande wa Tanzania Bara suala hili linashughulikiwa na vyombo vinne; Ujenzi, Mambo ya Ndani na vyombo vingine.

Kwa hiyo, tumeamua kwamba Wizara ya Ujenzi watunge sheria mpya itakayofanya marekebisho yale ambayo yanawakera upande wa pili wa Muungano, hatua hiyo sasa inatekelezwa. Tayari Sheria mpya iko katika kutungwa na Wizara ya Ujenzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa njiblu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu awali kwamba moja katika changamoto tunazopata katika Muungano ni suala la usajili wa vyombo vya moto. Ni kweli kwamba gari zinazotoka Tanzania Bara zinaingia Zanzibar bila kuulizwa, lakini Sheria zilizopo Tanzania Bara zinahesabu gari zinazotoka Zanzibar ni kama gari za kigeni.

Suala hili limekuwa changamoto kwa siku nyingi na kama nilivyosema kwamba tumelifanya kazi, tulifiki pahali kurekebisha Sheria zilizopo, kwa Zanzibar imekuwa rahisi kurekebisha Sheria zilizopo lakini kwa upande wa Tanzania Bara suala hili linashughulikiwa na vyombo vinne; Ujenzi, Mambo ya Ndani na vyombo vingine.

Kwa hiyo, tumeamua kwamba Wizara ya Ujenzi watunge Sheria mpya itakayofanya marekebisho yale ambayo yanawakera upande wa pili na hatua hiyo sasa inatekelezwa, tayari Sheria mpya iko katika kutungwa na Wizara ya Ujenzi.

**Wafanyakazi Wanaoacha Kazi Kabla ya  
Miaka 60 Kulipwa Mafao**

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Watumishi wa Serikali wanaochangia Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma PPF wanalamikia utaratibu wa kutokuwalipa wastaaful mafao yao kabla ya hawajafikisha umri wa miaka 60 tofauti na Mifuko mingine ya NSSF, PSPF na LAPF:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kubadilisha utaratibu uliopo ili wafanyakazi wanaolazimika kuacha kazi kabla ya umri huo wapate mafao yao?

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Aprili mwaka huu wa 2012 wakati Bunge lako Tukufu linapitisha Sheria Na. 5 ya Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2012 na kuondoa Kifungu cha 44 katika Sheria ya Mfuko wa Pendheni wa PPF, Kifungu ambacho kilikuwa kinaruhusiwa wanachama wanaoacha kazi au kuachishwa kazi kuchukua michango yao, Sheria Na. 5 haikufuta utaratibu wa wanachama wanawake katika Mfuko wa LAPF na PSPF kuchukua michango wao pale wanapoacha kazi kwa sababu za kuolewa. Aidha, Sheria ya NSSF haikugiswa kwa kuwa haikuwa na utaratibu kama huu, ingawa Mfuko huu ulikuwa unatekeleza utaratibu huo kwa mazoea ili kustahimili ushindani.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kutangazwa na kuanza kutumika kwa Sheria hii yalijitozea malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi na vyama vyao; na pia kutoka kwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu. Baadaye kuititia Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Selemiani S. Jafo, Mbunge wa Kisarawe, Bunge liliazimia na kuielekeza Serikali kuandaa haraka Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi za Jamii kama zilivyokuwa zimerekebishwa na kuleta Bungeni ili Fao la Kujitoa liweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kufanya kazi ya awali malekezo ya Bunge, katika Mkutano wako wa Tisa nilitoa Kauli ya Serikali yenye hatua zifuatazo:-

(i) Ilikuwa imebainika kwamba yapo mambo ya msingi kadhaa ambayo sharti yawe yameshughulikiwa kwanza kwa kina kabla ya kuandaliwa kwa Muswada utakaokidhi matakwa ya Hoja ya Mheshimiwa Selemiani Jafo na kama ilivyordhiwa na Bunge mwezi Agosti, 2012.

Kwa hiyo Serikali ikaliomba Bunge lako Tukufu litoe muda wa kutosha kwa Serikali ili kuandaa na kuleta Bungeni Muswada wa Sheria utakaokidhi matakwa ya Azimio la Bunge.

(ii) Wakati Serikali inalifanya kazi Azimio la Bunge kabla ya kuandaa Muswada wa Sheria kusudiwa, tutaendelea kufanya majadiliano na wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri, Wananchi wenyewe, sambamba na kutoa elimu kwa Umma kuhusiana na suala la Fao la Kujitoa.

(iii) Mamlaka ya kusimamia na kudhibiti Mifuko ya Hifadhi ya Jamii SSRA tayari imekwishatoa Tangazo kwa Umma kutengua uamuzi wake wa mwezi Agosti, 2012 wa kusitisha Fao la Kujitoa. Hii ina maana kwamba wananchi wanaokidhi vigezo vyta kunufaika na Fao la Kujitoa sasa wataendelea kupata Fao hilo kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na SSRA.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Waziri hasa kwa Fao la kujitoa kwa wafanyakazi mbalimbali kwa sababu ilikuwa ni kero kubwa sana na kule Geita kuna mgodi wa GGM ilikuwa ni kero kubwa na kwa uamuzi wa Serikali. Kwa kweli kwa niaba ya wale wananchi napenda kuishukuru Serikali kwa uamuzi huo mzuri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa wastaifu wengi hasa Walimu, Wauguzi ambaa hasa wanatoka Vijijini wamekuwa na mahangaiko makubwa sana kufuatilia mafao yao hasa hasa wengine ulazimika kutokea Vijijini kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya kufuatilia mafao na hili ni kero kubwa sana kwa wananchi.

Kwa hiyo, ningependa kujua pia mkakati wa Serikali kwamba inajipanga vipi kuweza kuondoa kero hii kwa wastaifu walio wengi kwa sababu wanahangaika kusafiri hapa na pale na wakati mwingine hawapati mafao yao kwa wakati? (Makof)

(b) Kwa kuwa Mifuko hii ya Kijamii, mara nyindi wanachama wanachangia Mifuko hii lakini manufaa wanayosubiri wakati wa kustaifu, hapa kati kati hakuna namna yeote ya kutumia michango yao kwa ajili ya manufaa yao.

Kwa hiyo, ningependa kujua sasa kwamba Serikali inaweza mkakati gani kwamba hata kabla ya kustaifu, wananchi waruhusiwe kutumia Mifuko hii aidha kwa kujipatia zile fedha kuweza kuziwekeza katika shughuli zao binafsi kabla ya kustaifu ili wawze kunufaika na Mifuko hii kwa kuwa pia Mifuko hii inatumika kwa ajili ya kuwekeza yani Mifuko hii inawekezwa katika sehemu mbalimbali katika Miradi ya Maendeleo, Nina imani kwamba wanapata faida kubwa ambazo faida hizi zitumike pia kwa ajili ya kuwanufaisha wanachama.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Lollesia Bukwimba, kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru kwa pongezi kutokana na kutekeleza yale ambayo wafanyakazi walikuwa wanayatarajia, lakini naomba nimjibu kuhusiana na masuala haya mawili kwamba la kwanza anauliza Serikali inajipangaje ili wafanyakazi wasipate bugudha kutoka kwenye maeneo yao kufuatilia pensheni zao.

(a) Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba wale wanaotaka kwenda Dar es Salaam wanakwenda kwa ridhaa yao kwa sababu Mifuko mingi sasa hivi iko Mikano. Mifuko yote imeshapelekwa Ofisi Mikano na kwa wale ambaa wanatimiza vigezo kwa kupeleka vielelezo vyao kabla ya miezi sita kwa sababu mfanyakazi anapashwa kutoa notice kwa mwajiri wake kabla ya miezi sita kwamba atastaifu.

Akishafanya hivyo na mwajiri akampelekea barua ya kukubali basi anapashwa kuwasiliana na Mifuko kwa kuhakikisha vielelezo vyote, barua yake ya ajira, barua yake ya kudhibitishwa kazini, barua zake za kupewa promotion na kukubali hizo promotion zinakuwa tayari na kupelekwa katika Mikoa ambayo ina Ofisi zao za Hifadhi ya Jamii.

Baada ya hapo pesa hizi zinaandaliwa na wengi wanawekewa kwenye accounts zao kwa kutumia cash. Ni PSPF pekee yake ndio inapeleka hundi, lakini inapeleka Mikoani.

Kwa hiyo, naomba wafanyakazi wasisumbuke isipokuwa watumie ofisi zetu, Ofisi za Hifadhi ya Jamii zilizopo Mikoani kwa kuwasiliana nao kusudi pesa walipwe mapema na wengi kwa kweli wanalipwa mapema wanapokuwa wamefanya hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na uwekezaji wa Mifuko hii, Mheshimiwa anapenda kujuwa wanachama wanafaidikaje.

Kwa kweli wanachama wanafaidika kwa mambo mengi; kwanza faida ya kuwekeza inaonekana katika mafao yale ya muda mfupi, kuna mafao ya uzazi, kuna mafao ya kuumia kazini na mafao ya aina mbalimbali. Mafao haya inapofika mwisho wa pensheni hayakatwi kwenye pensheni. Kwa hiyo, hiyo tayari ni faida.

Lakini pia baada ya kurekebisha Sheria tumekubaliana na SSRA sasa hivi inaandaa taratibu kuhakikisha kwamba Mifuko yote inaongeza thamani ya pensheni kulingana na hali halisi ya uchumi pamoja na thamani ya pesa kadri inavyoendelea. Pesa hizi za thamani zitaongezeka kutokana na uwekezaji wa Mifuko hii.

Kwa hiyo, wanachama watafaidika kadiri Mifuko inavyowekeza na kupata faida wakati wanaendelea kufanya kazi. Lakini faida kubwa ni wakati wa pensheni, kwa hiyo katika kufanya *indexation* Mifuko hii itaweza kuboresha mafao ya wafanyakazi wakati wanaendelea na kazi lakini pia wakati wa pensheni.

Na. 112

#### **Ushuru wa Zao la Tumbaku**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Serikali ilipojibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, kuhusu ushuru wa zao la Tumbaku wa 5% unabaki kwenye Halmashauri kwamba asilimia 3 imezuiwa kuanza msimu uliopita ili ipelekwe kwa mkulima:-

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani kama hiyo asilimia 3 itapelekwa kwa wakulima msimu ujao?

(b) Wakati wa malipo ya zao la Tumbaku msimu wa 2010/2011 viongozi wa AMCOS ya Kijiji cha Upendo- Chunya walishirikiana na wafanyakazi wa benki kupokea Double Payment ya dola zaidi ya 100,000 ambayo sasa wanachama wa AMCOS wamelazimishwa kukatwa kwenye msimu wa 2011/2012 na Waziri husika analifahamu jambo hili.

Je, Serikali inasema nini juu ya uonevu wa hali hii?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ushuru wa Mazao (*Produce Cess*) wa asilimia 3-5 ya bei ya shambani (*Farm Gate Price*) unatozwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 pamoja na mabadiliko mbalimbali (*The Local Government Finance Act, 1982 and Subsequent Amendments*) na kutokana na bei ya Mkulima wa Tumbaku kushuka katika msimu wa 2009/2010, Serikali iliamua kuwa katika ushuru wa mazao wa asilimia 5 unaolipwa kwa Halmashauri za Wilaya husika hizo, ugawanywe ambapo Halmashauri husika zitapata asilimia 3 na wakulima walipwe asilimia 2 inayobaki ili kuongeza bei ya Tumbaku inayokwenda kwa Mkulima.

Hata hivyo, kwa kuwa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2011 (*The Finance Act, 2011*) haikufanya marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kuhusu mgawanyo wa mapato yatokanayo na Ushuru wa Mazao katika Halmashauri za Wilaya, uamuzi huo haukutekelezwa kwa kuwa kufanya hivyo kungekuwa ni kukiuka Sheria.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa mapato yatokanayo na ushuru wa mazao kwa Halmashauri za Wilaya na lengo la kuongeza kipato cha Wakulima kwa kupunguza makato mbalimbali, Serikali kwa kushirikiana na wadau itaangalia namna bora ya kutoza ushuru wa mazao ili kuhakikisha kuwa Halmashauri zinaendelea kutekeleza majukumu yao na wakati huo huo Wakulima wanapata kipato kizuri kutokana na mauzo ya mazao yao.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya waliokuwa viongozi wa Upendo AMCOS Ltd., walihusika na kufanya "Double Withdrawals" kutoka benki kwa mauzo ya Tumbaku msimu 2010/2011 ya kiasi cha Dola za Kimarekani 123,000/= ambapo fedha hizo zililipwa Wanachama/Wakulima kwa utaratibu sahihi wa Chama cha Ushirika cha Upendo AMCOS. Hata hivyo, fedha zilizochukuliwa mara ya pili na baadhi ya waliokuwa viongozi wa Upendo hazikupelekwa kwa Wanachama/Wakulima.

Katika kushughulikia tatizo hilo, Wizara yangu imefanya ukaguzi wa mahesabu ya Chama hicho na kubaini kasoro mbalimbali ambapo viongozi waliohusika wameondolewa na uongozi mpya umechaguliwa. Aidha, kwa kuwa suala hilo linahusu wizi, Mrajis wa Vyama vya Ushirika alilifikisha suala hilo Polisi Wilaya ya Chunya na upeletezi unaendelea.

**SPIKA:** Tunaomba utulivu kuna watu wanajisahau kila mtu anaongea utafikiri yuko nje. Mheshimiwa Zambi swali la nyongeza.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(a) Swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge wa Lupo linasema je Serikali itatoa tamko gani kuhusu yale makubaliano kwamba asilimia 2 ziende kwa Wakulima na asilimia 3 ziende kwenye Halmashauri, Mheshimiwa Naibu Waziri hajali-address suala hilo.

Je, Serikali itahakikisha fedha hizo zinaenda? Kwa sababu kusema kwamba Serikali illiona kwamba kufanya hivyo ni kuvunja Sheria wakati yenyewe ndio ilioamua nadhani Serikali itakuwa inajikanganya. Sasa inasema nini kuhusu tamko hilo?

(b) Mheshimiwa Spika, wanachama wa Upendo AMCOS wamekatwa pesa kwa maana zile zilizopelekwa mara ya pili na sio kosa lao, Serikali inatoa tamko gani pamoja na kwamba upeletezi unaendelea. Je, ikibainika kwamba wale viongozi waliiiba zile fedha, wale wanachama ambao walikatwa pesa mara ya pili watarudishiwa pesa zao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba nijibu swali la Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumesema hivi, kwenye swali la msingi nimesema kwamba yale maamuzi yaliyofanywa kinachokwenda kwenye Halmashauri ni asilimia 5, Halmashauri ile Halmashauri ya wananchi hawa hawa wa Chunya, lakini tulichosema ni kwamba katika mazingira haya ambayo yalikuwa ni mazingira maalum kutokana na mdoororo wa kuanguka bei.

Katika zile asilimia 5, 2 ziende moja kwa moja kwa Wakulima. Sasa ukifanya amendment kama ile kwa maamuzi ya Serikali lazima yawe na misingi ya Sheria ambayo inafanyiwa amendment humu ndani Bungeni, Sheria hiyo haikufanywa kwenye Finance Act. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba maagizo yakabaki kwamba ile asilimia 3 imekwenda kwenye Halmashauri na ile asilimi 2 ikarudi kule kule kwenye Halmashauri ambayo sisi wenyewe Wabunge ni Wajumbe kwenye hizo Halmashauri.

Kwa hiyo, sasa kama kulikuwa na nia njema ya kufikisha ile asilimia 2 kwa Wakulima, fikra iliyokuwepo ni kwamba Halmashauri zile zingefanya hivyo.

Sasa matokeo yake kama zilifika zile asilimia 2, Halmashauri zikaamua kuzitumia kwa mambo mengine nje ya kuwafikisha Wakulima, hayo ni maamuzi ambayo sasa ni ya kwenu, lakini nia nzuri ilikuwa ipo pale ya Serikali na Wananchi na Wakulima wanajua hilo.

Sasa sidhani kama kuna kujikanganya tu ila isipokuwa ni kwamba kwa sababu hiyo nia haikupata msingi wa Kisheria hapa Bungeni utekelezaji wake ulikuwa umepata hayo matatizo, lakini matarajio ni kwamba Halmashauri zingetusaidia kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la AMCOS SACCOS, hizi SACCOS ni mali za wanajumuiya wale wanachama wenyewe, kusema Serikali tuingilie kati, Serikali mpaka sasa hivi kwa mkondo wa Sheria, tumeingilia kati kwa kuwafikisha Mwenyekiti, nadhani Makamu wake na Katibu nilivyotoa maelezo kwa Vyombo vya Sheria, kesi iko Mahakamani.

Sasa nasema baada ya hilo likibainika Serikali itachukua hatua gani? Tutachukua hatua kulingana na hukumu iliyotolewa.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kuna Wakulima wa Tumbaku wa Kijiji cha ASANTE NYERERE, Wilaya ya Kasulu kuititia kikundi chao, chama chao cha ASANTE NYERERE AMCOS hawajalipwa malipo yao ya Tumbaku tangu 2010/2011, 2011/2012 nimefuatilia suala hili kwa Afisa Ushirika bila kupata majibu.

Je, Waziri yuko tayari kutuma wataalam kutoka Wizarani ili kusaldia kuititia mahesabu na kuhakikisha wakulima hawa wanapatiwa haki yao ya msingi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Hili ni swali very specific geni lakini Mheshimiwa Naibu Waziri jibu ni very specific, geni.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba nijibu swali la Mheshimiwa Agripina Buyogera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili mimi nimelipokea na hii SACCOS ya ASANTE NYERERE, Mrajis pamoja COASCO ambaye ni Mkaguzi wa Hesabu za Vyama vya Ushirika wote wanawajibika kuhakikisha kwamba Vyama vya Ushirika mahesabu yao yanakwenda sawa sawa.

Sasa kama kuna tatizo naomba nimwahidi kwamba tutamwagiza Mrajisi pamoja na wahusika wengine wote kwa kuanzia na Mrajisi wa Kigoma yenewe aanze kufuatilia tatizo hili na tutafanya nae kazi kwa karibu ili kupata majibu ya suala hili.

Na. 113

#### **Fedha Zinazotolewa kama Cess kwa Wakulima wa Tumbaku Nchini**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Wakulima wa Tumbaku nchini katika msimu uliopita 2010/2011 waliathirika na bei ya Tumbaku kuperomoka na hivyo kutakiwa asilimia 2 (2%) kukatwa kutoka kwenye asilimia 5(5%) zinazopelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya kama Cess zipelekwe kwa wakulima ili kupunguza makali ya bei waliyopata:-

- (a) Je, fedha hizo zitawafikaje wakulima wote wa Tumbaku nchini?
- (b) Je, ni nani anawajibika kuhakikisha fedha hizo zinawafikia wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli bei ya tumbaku kwa mkulima katika msimu wa mwaka 2010/2011 ilishuka kutoka Dola za Kimarekani 2.5 kwa kilo kwa msimu, hadi Dola za Kimarekani 1.4 kwa kilo, kwa msimu unaofuata wa 2010/2011. Aidha, katika msimu wa 2011/2012 bei ya tumbaku kwa mkulima imeimarika kidogo hadi kufikia Dola za Kimarekani 1.8 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia suala hilo Serikali, iliamua kuwa katika 5% ya ushuru wa mazao wanaotozwa wakulima na Halmashauri za Wilaya, 3% iende katika Halmashauri husika na 2% iende kwa wakulima waliothirika na kushuka kwa bei ya tumbaku katika msimu wa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika Swali Namba 112, la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, uamuzi wa kufanya makato hayo ulifikiwa wakati Finance Act ilikwishapitishwa. Hivyo ilionekana kwamba, kuendelea na makato hayo ya fedha ambayo kwa mujibu wa Sheria ni fedha halali za Halmashauri za Wilaya husika, ingekuwa ni kinyume cha Sheria.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza; kwa kuwa, kumekuwa na tatizo la kushughulikia matatizo ya zao hili kwa wakulima hasa yanapojitokeza matatizo ya kuanguka kwa bei kwenye soko la dunia, lakini vilevile majanga mbalimbali kama ukame na mvua za mawe kujitokeza.

Je, kwa nini sasa Serikali, isije na mkakati wa kuwahakikishia wakulima udhibiti wa mambo haya yanapojitokeza kwa kuanzisha Mfuko wa zao ambao unaweza ukasaidia pale ambapo matatizo haya makubwa yanapojitokeza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, wakulima wa tumbaku nchini, wamekuwa wakibebeshwa mzigo na baadhi ya Viongozi wa vyama vya msingi wakati wa kukatwa madeni yao kwa 100% ambayo wakati mwininge yanakuwa hayajapitishwa katika makisio yao kwa kuwabebesha mzigo wa madeni makubwa kwa ujenzi wa maofisi ama kwa kuongeza kwa kiasi kikubwa sana pembejeo wanazoingiza kwenye vyama vyao vya msingi.

Je, ni hatua zipo zinachukuliwa kwa viongozi hawa wa vyama vya msingi katika kudhibiti, ili kuhakikisha kwamba, Wakulima wetu wanapewa fedha zao zote ambazo zinatokana na kilimo ambacho wanakifanya?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Nkumba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni lazima tuseme tu kwamba, tulishakutana na Bodi ya Tumbaku terehe 17 Oktoba, 2012 na kuna matatizo mbalimbali ambayo zao la tumbaku linaendelea kukumbana na nayo matatizo.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri pia kusema na wananchi wakajua kwamba, zao la tumbaku ndio mchangiaji mkuu kwa mapato, kwa mazao yote ya kilimo hapa nchini Tanzania. Kwa hivyo, kuna masuala mbalimbali ambayo tukifanya kama Serikali, pamoja na kuwahusisha wadau tunaongeza mapato ya zao lenyewe la tumbaku.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili la kuanzisha mfuko wa Wakfu, korosho wanayo, pamba wanayo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mtulie, kuna watu wanakaa hapa wanazungumza kabisa, naomba mtulie.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nasema, hili la kuongeza mfuko wa Wakfu kwa zao la tumbaku, ni jambo ambalo wadau wameanza kulifanya kazi.

Mimi ninaomba niseme tu kwa sababu, Mwenyekiti wa Bodi na yeye mwenyewe Mheshimiwa Said Nkumba, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku, tumo naye humuhumu ndani ya Bunge, tufanye kazi kwa karibu, ili Mkutano unaofuata wa wadau ufikie maazimio ya kuwa na Mfuko wa Wakfu kwa sababu, hili litapunguza matatizo mengi kwa maana ya shared sanctions badala ya kusubiri Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la wakulima wa tumbaku kufanyiwa ndivyo sivyo na Viongozi wa vyama vya msingi. Hili litapatiwa ufumbuzi tutakapoleta Bungeni, mwezi wa pili, Sheria ya Vyama vya Ushirika, ili kupata wajibu na obligations za viongozi wa Vyama vya Ushirika dhidi ya wanachama wao. Hili la kwamba, viongozi wa vyama vya msingi wanafanya ndivyo

sivyo, wanabebesha mizigo ya madeni kwa wakulima, limejitokeza katika vyama vingi nya msingi kwa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kusema tu kwamba, ufumbuzi wake utakuja Sheria hii ya Vyama nya Ushirika, tutakapoikamilisha humu Bungeni, mwezi Februari, 2013 ili kila mtu abebe dhamana katika hili linalotokea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Said Juma Nkumba, ulitakiwa utangaze interest zako katika suala hili.

Mheshimiwa Mwatuka?

Nimemwona Mwenyekiti wa Bodl, lakini sitaki kumwita Mwenyekiti na Makamu wake.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo la tumbaku nchini linafanana na tatizo la watu wa korosho Kusini, ambalo msimu wake huwa unasuasua na hauna uhakika. Msimu wa mwaka jana 2011 kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani, korosho zilinunuliwa kwa bei ya 1,200/= lakini walilipwa 800/= na zingine kwamba, watalipwa awamu ya pili. Lakini kwa bahati mbaya, awamu ya pili hiyo mpaka leo wengine hawajapata.

Mheshimiwa Spika, sasa msimu uliofua huu tulionao, kwanza umecheleweshwa. Halafu hivi sasa kuanzia jana wameanza kupata pesa, lakini bei ni ileile ya mwaka jana 1,200/. Lakini wanalipwa 600/= Mikoa yote miwili na sijui sehemu nyingine, lakini Mtwara na Lindi, wanalipwa 600/= katika 1,200.

Mheshimiwa Spika, sasa kama mwaka jana...

(Hapa Mzungumzaji hakusikika)

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** ... na mwaka huu si itakuwa hivyo hivyo? Kama ni hivyo, si kuwaibia kujanja wakulima?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Kwanza kufanana hayafanani kabisa. Lakini kwa heshima yako, Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu.

Havifanani korosho na tumbaku kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibju swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu. Tatizo la tumbaku na la korosho halifanani sana. Tatizo linalotokana na korosho linatokana na kwamba, mabenki yalipokopeshya vyama nya msingi kwenye korosho, ulipaji ule ulikuwa na matatizo.

Tumekwenda tumefanya ukaguzi Mkoo wa Pwani, tutafanya ukaguzi Mkoo wa Mtwara, kwa hivi sasa kinachoonekana ni kwamba, vyama nya msingi viongozi wake wenywewe ndio

waliofanya uharibifu ule ambao sasa unazuwia mabenki mwaka huu kukopesha zile fedha. Kwa sababu, benki haiwezi ikaendelea kukukopesha kama hujalipa deni la mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, tulichofanya ni kwamba, Serikali, imeyaomba mabenki haya. Tumekutananayo yote. Bei ya msingi ya 1,200/= tunachofanya ni kwamba, itatoka ile asilimia 50%. Vyama vya msingi na vyama vingine vitaendelea kulipa yale madeni yaliyokuwa yanatoka mwaka jana kwa mauzo ya mwaka huu. Italipwa ile; hata usitikise kichwa, ukikopa ni lazima urejeshe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwaambie tu na niwasih i wakulima wa korosho kama ilivyo kwa wakulima wa tumbaku; jamani, vyama vya msingi ni mali yenu na wale viongozi mnawachagua wenyewe. Wakifanya uharibifu, ninyi muwe wa kwanza kuwajibisha, msisubiri Serikali. (Makofi)

Na. 114

#### **Kufufua Vyuo vya Watu wenye Ulemavu**

**MHE. RIZIKI O. JUMA** aliuliza:-

Katika kudhibiti na kuliwezesha kundi la watu wenye ulemavu, ili waweze kujiajiri wenyewe, Serikali ilikuwa na mpango wa kuvifufua vyuo vitatu vya Masiwani (Tanga), Mbeya na Mtapika (Masasi), ambavyo vilifungwa, kutokana na ufinyu wa fedha na upungufu wa watumishi wa kuiyendesha:-

Je, Mpango wa kuvifufua vyuo hivyo umefikia wapi?

**SPIKA:** Ahsantesana, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu?

Wataalam, mashine hii ni muda mrefu inaleta matatizo.

#### **NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma. Kwanza, kwa kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya taifa ya maendeleo na huduma kwa watu wenye ulemavu ya Mwaka 2004, Serikali, kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha jamii, ili watambue watu wenye ulemavu kama sehemu ya jamii na kuwahuishisha katika mipango ya maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Riziki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa kazi ni muhimu katika maendeleo ya binadamu kwa sababu, inamwezesha mtu mwenye ulemavu kujitegemea, Wizara yangu imeanza kuvifufua vyuo hivyo kwa awamu. Katika awamu ya kwanza, Wizara inaendelea kufanya ukarabati katika Vyuo vya Masiwani na Luanzari. Aidha, awamu hiyo katika Mwaka wa Fedha 2012, Chuo cha Masiwani Tanga, kilitengewa kiasi cha shilingi milioni 165 na Chuo cha Luanzari – Tabora, kilitengewa kiasi cha shilingi milioni 120.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili itahusisha ukarabati wa Chuo cha watu wenyewe Ulemavu, Mtapika – Masasi. Fedha kwa ajili ya kugharamia ukarabati huo zimetengwa kwenye Bajeti ya mwaka 2012/2013 ambapo kiasi cha shilingi milioni 500 zitatumika.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Luanzari – Tabora, kitakuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 144 kwa mwaka na Chuo cha Masiwani – Tanga, kitakuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 40 kwa mwaka. Tofauti hii inatokana na ukubwa wa eneo la Chuo na idadi ya majengo yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi waliopo Vyoni kwa sasa ni 102, Chuo cha Watu wenyewe Ulemavu – Yombo na 81, Chuo cha Wanawake wasioona – Singida.

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini swali langu la kwanza ni kwa sababu, mwaka 2011/2012 zilitengwa fedha kwa ajili ya ukarabati wa vyuo viwili, Masiwani na Luanzari.

Je, hadi sasa Mwaka huo wa Fedha umeshaisha karibu miezi mitano iliyopita. Je, ukarabati huo umefikia wapi? Umemalizika au la?

Lakini la pili ni, kundi hili ni kubwa sana la watu wenyewe ulemavu, ambao ukitizama takwimu ambazo ametupa Mheshimiwa Waziri, walioko vyoni ni watu kama 183.

Je, hawa ambao wako nje ya vyuo hadi sasa, hawapati haki yao ya msingi ya kupata elimu hii na wakaweza kujiajiri wenyewe na pia kulipunguzia Taifa mzigo?

Mheshimiwa Spika, ukizingatia kwamba, walemvu hawa wengi wako vijijini na ambako wamefichwa.

Je, Serikali, ina mkakati gani kuhakikisha ndugu zetu hawa na watoto wetu hawa wanapata hiyo fursa ya kujifunza na wao, ili waweze kujiajiri wenyewe? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Riziki Omar Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majengo hayo yameanza kufanyiwa ukarabati na yamo katika hatua mbalimbali za kukamilika, ikiwemo jengo hilo la Luanzari – Tabora, pamoja na lile la Masiwani kule Tanga. Kuhusu kuwepo na idadi chache kuliko ukweli wa uwepo wa idadi ya watu wenyewe ulemavu nchini, ni kweli hili tunalitambua na ndio sababu Serikali, imeanza zoezi hilo la kuvipanua vyuo hivyo na kuvifungua vile ambavyo vilikuwa vimefungwa; kikilwemo chuo kile cha Masasi, cha Tabora pamoja na hicho cha Tanga.

Mheshimiwa Spika, kwa ukweli, kile chuo cha Singida kimeshafanyiwa ukarabati na kinafanya kazi sasa vizuri. Chuo hiki cha Yombo na chenyewe kipo katika hali nzuri sana. Lakini sasahivi kina wanafunzi 102. Kwa hiyo, juhudhi za Serikali, zipo pale na zitaendelea kuongezeka. Ninaamini baada ya kuongeza idadi ya wanafunzi hawa takribani 184 ambao wataingizwa kwenye vyuo hivyo, ninaamini idadi yao watakuwa wanahitaji kupata fursa hiyo, itakuwa ni kubwa pia. Ahsante sana.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kuwawezesha walemavu katika kupata elimu na masuala mengine ndani ya jamii yetu. Lakini bado kuna Sheria ambayo inatoa fursa ya Idara mbalimbali za Serikali, katika kuwawezesha walemavu kuajiriwa. Lakini wale wenye mamlaka ambao wana nafasi hiyo ya kuajiri watu wenye ulemavu katika Idara mbalimbali, bado nafasi hizo kwa walemavu huwa ni tatizo kuzipata.

Je, Serikali, inawaambia nini walemavu wa Tanzania pindi wanapokwenda kutafuta ajira katika taasisi mbalimbali, hupata usumbufu wa kuajiriwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Barwany, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010, inahamasisha na inataka maeneo yote ya ajira kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu, ili waweze kupata ajira sawasawa na watu wengine. Sasa suala la utekelezaji kama Mheshimiwa Mbunge, anavyolielezea ni kufuata na kuzingatia Sheria iliyopo. Kwa hiyo, vyombo vinavyohusika ninavita na ninaviomba viweze kufuata Sheria iliyopo, ili waweze kuwapa haki inayostahili kwa watu wenye ulemavu. (Makof)

Na. 115

#### **Serikali Kushirikiana na Wananchi Kukamilisha Mahitaji ya Sekondari za Kata**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuliza:-

Wilaya ya Rombo, imefanikiwa sana katika ujenzi wa sekondari za Kata na ziko baadhi hazijakamilika na nyingine zinahitaji watumishi na vifaa mbalimbali:-

(a) Je, Serikali iko tayari kusaidia nguvu za wananchi wa Rombo, kwa kuwapatia maabara, maktaba, walimu wa kutosha na vitendea kazi vingine?

(b) Je, Serikali, iko tayari kushirikiana na wananchi wa Rombo, kujenga Chuo cha Ufundu (VETA), ili iwawezeshe wanafunzi wanaomaliza kidato cha 5 na 6 kuijendeleza?

#### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, Serikali, ina mpango wa kuboresha miundombinu ya shule 264 nchi nzima, shule mbili kwa kila Halmashauri hizo 132. Ujenzi wa Maabara na nyumba za Walimu, kwa sasa ujenzi huo upo katika hatua ya utangazaji wa zabuni. Katika Halmashauri ya Rombo, ujenzi wa nyumba za walimu na Maabara, utafanyika katika Shule za Sekondari za Mawanda na Maki. Kuhusu kupanga Walimu, Serikali imekuwa kila mwaka ikipanga Walimu katika Shule za Sekondari kadiri ya upatikanaji wa Walimu wanapohitimu mafunzo yao. Mwaka 2010/2011 Halmashauri ya Rombo, ilipangiwa jumla ya Walimu 116 na mwaka jana 2011/2012 ilipangiwa Walimu 209.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa vitendea kazi. Serikali, imekuwa ikitoa ruzuku ya uendeshaji (Capitation Grant) kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vitabu. Katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 kila mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya

Serikali, alitengewa kiashi cha 21,000/= katika mgao uliokwenda kwa kila Halmashauri, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Rombo. Mwaka huu 2012/2013, kila mwanafunzi wa shule ya Sekondari ya Serikali, ametengewa kiasi cha 25,000/= kwa mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Sera ya Kushirikisha Sekta Binafsi na Wananchi katika kufanikisha mipango ya maendeleo. Hivyo basi, wananchi wa Wilaya ya Rombo, wanashauriwa kujenga Chuo cha Ufundı Stadi (VETA), kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa na Mamlaka ya Elimu ya Ufundı Stadi (VETA). Wilaya ya Rombo, ina Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Mamtukuna, ambacho kipo katika awamu ya kwanza ya ukarabati, kukiwezesha kutoa mafunzo ya ufundı stadi kuanzia Januari 2013.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifauatvyo:-

Kata zote za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, kuna shule za Sekondari kati ya mbili hadi nne. Kwa kuwa, wanafunzi wengi wanaomaliza Kidato cha Nne na cha Sita, hawapati nafasi ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu. Na kwa kuwa, takwimu zinaonesha kwamba, wanafunzi wa darasa kwanza, wanapungua katika Jimbo langu kutokana na vijana kuhamia Mijini na hivyo, ndoa mpya kukosekana.

Je, Serikali, haioni kwamba, ipo haja, badala ya wananchi wa Rombo kufikiria kujenga chuo kipyä cha ufundı stadi, baadhi ya shule za Kata ambazo zinatosheleza, zikageuzwa kuwa shule za ufundı stadi, ili kusaidia hawa vijana wanaomaliza kidato cha nne na cha tano, kupata stadi za kuwawezesha kujajiri wenyewe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Tatizo la Maabara...

**SPIKA:** Naomba liwe fupi, maswali yawe mafupi.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, tatizo la Maabara ni kubwa nchi nzima. Badala ya Serikali kufikiria kutengeneza maabara katika kila shule, ni kwa nini Serikali, isirudie utaratibu wa zamani wa kutenga shule za Sayansi peke yake na kuziwezesha hizo kupata Maabara, badala ya kufikiria kupeleka Maabara katika shule kwa sasa, kitu ambacho kitachukua muda mrefu sana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA JUU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza anasema ni vizuri Serikali katika kuboresha elimu ya ufundı kubadilisha baadhi ya shule za Kata kuwa VETA, mimi hapa naweza nisiwe na majibu kwa sababu litakuwa limekaa kisera zaidi.

Lakini kama wazo lako litakuwa nzuri huko baadaye tutaendelea kulifiria lakini nia ya Serikali ni kumtaka mtoto wa Kitanzania aweze kupata elimu ya ufundı na elimu hii ya kawaide. Lakini suala la kuliangalia kwa mapana zaidi halina majibu kwa haraka haraka kwa sasa kwa sababu ni suala la kisera.

Kuhusu suala la pili kwamba kuwe na shule za Sayansi kama zamani Mheshimiwa Mbunge unapotumia mifano ya zamani kulikuwa ni kweli na shule za Sayansi zamani huko shule za Ifunda, sijui shule za wapi lakini kwa sababu tuliamua kupanua elimu hii ifike mpaka kwenye zile shule za ngazi ya kata na Serikali tayari imejipanga kuboresha hizo.

Mheshimiwa Spika, shule kama nilivyosema kwamba mwaka huu tunayo Bajeti, ya kuzijenga shule 264 ziwe *functional school* na kule kwako tayari kuna hizo shule mbili ambazo nimezitaja hapa moja ya zile shule utapata karibuni milioni 178 na nyingine milioni kama 140 kuweza kuwa *functional School* ni pamoja na kuwa na vitabu na kuwa na maabara.

Mheshimiwa Spika, naomba tuipe tu muda Serikali iweze kutekeleza azma ya kuhakikisha kwamba kila shule hizi, shule za Kata zinapewa madarasa zinapewa walimu, zinapewa vitabu na vifaa vya maabara pamoja na walimu wa Sayansi. (*Makofi*)

Na. 116

### **Uwekezaji kwenye Sekta ya Madini**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO (K.n.y. MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA)** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini Serikali haikomeshi uwekezaji kwenye sekta ya madini, gesi na mafuta kwa kuwa toka tuwekeze hakuna mafanikio ya maana kama nchi nyingine zenyre rasilimali hizi?

(b) Je, kwanini Serikali haianzishi *Ring Fencing* ya miradi ya migodi na visima vya mafuta na kuanzisha kodi ya *Windfall Gains Tax* ili kudhibiti ukwepajji kodi na kuongeza mapato ya Serikali?

(c) Je, kwanini Serikali isivunje mikataba yote ya uwekezaji wa madini wanaothibitika kukwepa kodi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASALLE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangala, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika sekta ya madini na mafuta zinahitaji mtaji mkubwa na teknolojia ya juu na pia huchukua muda mrefu kugundua madini, gesi na mafuta ili kuanza uzalishaji. Kwa upande wa sekta ya madini, Taifa limepata mafanikio mbalimbali kutokana na utekelezaji wa sera ya madini ya mwaka 1997 na sheria ya madini ya mwaka 1998 pamoja na kwamba bado mafanikio zaidi yanahitajika. Aidha, Serikali imefanya marekebisho ya sera na sheria ya madini ambapo ilitunga sera ya madini ya mwaka 2009 na sheria ya madini ya mwaka 2010 ili Taifa linufaika zaidi.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji kwenye sekta ya gesi na mafuta ulianza takribani miaka 60 iliyopita lakini kuanzia mwaka 2010 na 2012 kumefanyika ugunduzi wa gesi nyingi kufuatia uchimbaji wa visima kumi na moja vya kina kirefu cha maji baharini. Kiasi cha gesi kilichogunduliwa hadi sasa kinakadiliwa kuwa futi za ujazo zipatazo trillioni 33.

Kwa sasa Serikali inaandaa sera na sheria mbalimbali zinasimamia shughuli za gesi na mafuta ili kuhakikisha kuwa manufaa zaidi yanapatikana kwa Taifa letu. Hivyo siyo busara kusitisha uwekezaji badala yake ni kusimamia shughuli zainazofanywa na wawekezaji hao ili Serikali ipate mapato yanayostahili bila kuibiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, sheria ya kodi ya mapato imefanyiwa marekebisho ambapo kipengele cha *ring fencing* kimeongezwa ili kuhakikisha kuwa kila mradu unajitegemea wakati wa kukokotoa kodi. Mpaka sasa Serikali na TPDC imesaini mikataba 26 ya uzalishaji na utafutaji

wa mafuta na gesi. Mikataba yote inazingatia maoni ya Mheshimiwa Mbunge ikiwemo *ring fencing*. Aidha, suala la *Wind Fall Gains Tax* tumelipokea na tunaomba tupewe fursa ya kulifanya kazi.

(c) Mheshimiwa Spika, sheria za nchi ziko wazi kwa yoyote anayezikiuka ikiwemo kushindwa kulipa kodi mbalimbali zilizopo kisheria inapothibitika kukiukwa hatua husika huchukuliwa ikiwemo kulipa faini. Kwa mfano kulingana na sheria na madini ya mwaka 2010 mwekezaji anapochelewa kulipa mrabaha au kodi ya pango la mwaka kwa siku 90 inatakiwa kulipa mrabaha huo na faini ya asilimia 50 kama ni kampuni na asilimia 25 kama ni mtu binafsi.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana hasa katika migodi na pato dogo linalotokana na migodi hiyo inayozalisha dhahabu kutokana na mrahaba mdogo inayoipata Serikali.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuweza kuangalia mikataba hiyo mipyä ili iweze kuwanufaisha wananchi katika Taifa hili?

Kwa kuwa sekta ya nishati ya gesi ni mipyä katika Taifa letu.

Je Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inawasaidia wananchi na wananufaika na sekta hiyo ya gesi mipyä?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu kwa kifupi pia.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASALLE):** Mheshimiwa Spika, tangu uwekezaji mkubwa wa madini uanze hapa nchini takribani miaka 14 Serikali imeweza kupata mafanikio mengi ikiwemo kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta hii ya madini ambapo mpaka sasa ilipoanza ilikuwa ni zaidi ya dola za Marekani milioni moja nukta tano na mpaka sasa ni dola za Marekani milioni 2.5.

Lakini pia ajira zimeongezeka kutoka elfu moja mia tatu kabla ya uwekezaji mpaka sasa tumefikia elfu kumi na tatu lakini tumeweza kupata teknolojia na tumeweza kupata usoefu ambaao ndiyo umetusaidia kugundua mapungufu ambayo tumekuwa tukiyafanyia kazi katika kurekebisha sera na sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, mimi nichukue nafasi hii kuwapongeza na kushukuru Bunge lako Tukufu haswa Wabunge waliokuwepo 2010 na huko nyuma baada ya kugundua haya mapungufu yote na kuyafanyia marekebisheshambayo ambayo yaliletea kutungwa sheria mipyä ya 2010.

Kwa hiyo Serikali inaendelea kufanya jitihada za kurekebisha mapungufu yote katika mikataba ya madini iliyopo sasa na tunaendelea na majadiliano na kampuni za madini ili yale mapungufu yote ambayo tumeyagundua tuweze kuyarekebisha ikiwemo service levy.

Mheshimiwa Spika, katika gesi kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza sasa hivi tunaendelea tuko katika hatua za mwisho za kutayarisha sera ya gesi, na sera hii tunawashirikisha wadau mbalimbali katika sekta hii ya Nishati na Madini ili waweze kuleta maoni ambayo yatakuwa na manufaa zaidi kwa Taifa.

Kwa hiyo anavyouliza kwamba Serikali imejipanga vipi tunapoandaa sera na baadaye tutakuja kuwa na sheria mipyä inayosimamia gesi na mafuta hiyo ni hatua ambayo Serikali inachukua katika kujipanga kuhakikisha kwamba tunakuwa hatupunjwi.

**SPIKA:** Ajira nadhani zimeongezeka mpaka 13,000 mmesema 13, Mheshimiwa nadhani ni kumi na tatu elfu tuna maswali manne, dakika zimebaki mbili, kwa hiyo naendelea na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kabla ya swali langu Namba 117 kujibiwa naomba nifanye masahihisho kidogo pale inaposema:-

Je, ni lini TANESCO itapunguza, iwe je lini TANESCO italipunguzia bei Shirika la umeme Zanzibar (ZEC). Baada ya masahihisho hayo naomba swali langu Namba 117 lijibiwe.

**SPIKA:** Hayo masahihisho ni kwamba je, ni lini TANESCO itaipunguzia?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Italipunguzia bei.

**SPIKA:** Italipunguzia?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Ilipunguzia bei Shirika la Umeme la Zanzibar (ZEC).

**SPIKA:** Kumbe siyo makosa makubwa sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Na. 117

#### **Gharama za Kuunganisha Umeme Zanzibar**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Gharama ya kuunganisha umeme kwa Tanzania Bara zimeshuka kutoka Shilingi 480,000 hadi 177,000 lakini kwa upande wa Zanzibar bado bei hiyo hajashuka.

Je, lini TANESCO itapunguza italipunguzia bei Shirika la umeme Zanzibar (ZEC) gharama ya kuunganisha umeme Zanzibar ili hatimaye wananchi nao wapate umeme kwa bei nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASALLE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa masahihisho hayo msingi wa swali unabadijika, likisomeka tu hivyo swali zima linabadilika maana swali ambalo tulilijibu lilikuwa...

**SPIKA:** Naomba mheshimiwa Naibu Waziri kidogo, kwa kweli nimeletewa ki-note na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis akilalamika kwamba swali linavyoonekana kwenye Order Paper yangu sivyo aliyopeleka na pamoja na masahihisho aliyopeleka ofisini kwangu bado yule aliyechapa kwa makosa tena.

Sasa mimi nilifikiria makosa yenye madogo madogo nikamwambia ukisimama utafanya masahihisho lakini ninavyosoma swali lilokoo kwenye jibu langu na swali liliko kwenye Order Paper ni maswali mawili tofauti. Kwa hiyo naomba niliondoe swali hilo.

(Hapa swali Namba 117 liliondolewa na Mheshimiwa Spika, kutokana na Makosa ya uchapaji)

**SPIKA:** Kwa hiyo, tunaenda Wizara inayofuata Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

Na. 118

### Huduma za Kibenki (ATM) Shelui

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Mji mdogo wa Shelui una wakazi wengi na mzunguko mkubwa wa fedha. Je, Serikali haioni umuhimu wa kushawishi taasisi za fedha kufungua huduma za ATM ambayo itawasaidia wananchi wa eneo hilo kuchukua fedha kirahisi kuliko kwenda Kiomboi umbali wa kilomita 25 ambako ndiko kuna Benki ya NMB?

**NAIBU WA FEDHA (MHE. JANETH Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, M-NEC, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuona kuwa wananchi wanapata huduma za fedha ikiwa ni pamoja na huduma za ATM karibu na maeneo wanayoishi. Hata hivyo kwa sasa Serikali haitoi huduma hizo bali huduma hizo zinazotolewa na taasisi za fedha chini ya misingi ya soko huria. Jukumu la Serikali ni kuweka mazingira yanayovutia uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji wengi kuanzisha na kufungua huduma za fedha katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Aidha, kwa ujumla wetu tunajukumu la kushirikiana na kuweka mazingira mazuri yanavutia wawekezaji katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, taasisi za fedha hufanya maamuzi kuhusu maeneo gani yanafaa zaidi kuweka mashine za ATM kwa kuzingatia mambo mbali mbali ikiwemo usalama, fursa za kibiasara mzunguko wa fedha, idadi ya watu gharama za uendeshaji, idadi ya taasisi na watumishi wa umma katika eneo husika.

Ni dhahiri kuwa taasisi za fedha hufanya utafiti kwanza kabla ya kuweka mashine ya ATM mahali kwa lengo la kuhakikisha kwamba kila upande unanufaika yaani taasisi za fedha na wateja wenyewe. Pamoja na kuzinagia vigezo hivi huangalia pia gharama ya kuweka mashine ya ATM katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, gharama ya kuweka ATM moja ni kati ya Shilingi milioni 40 hadi milioni 65 kutegemeana na aina ya mashine umri na ubora wake.

Mheshimiwa Spika, mpango mbadala ni kuwahamasisha wananchi kuijunga na huduma zinazotolewa na makampuni ya simu kwa kushirikiana na mabenki yaani Mobile Banking kwani gharama zake ni ndogo ukilinganisha na gharama za kuweka mashine za ATM, kufungua tawi kuanzisha benki katika maeneo ya vijiji.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu nina maswali mawili, la kwanza kwa kuwa swali hili ni kilio cha wananchi, na kwa kuwa maelezo aliyojatoa Mheshimiwa Naibu Waziri ya vigezo vya kuweka Benki ama ATM katika mji huu mdogo wa Shelui viro vyote. Na kwa kuwa mji huo una mgodi wa dhahabu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari sasa kama mdau mkubwa wa Taasisi hizi za kibenki kuzishawishi benki kuweka hata ATM kama siyo benki kabisa ili wananchi hawa wengi wanaopata shida kufuata benki, Kiomboi, Singida, Igunga adha yao ipungue?

La pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba huduma nyingine ambayo inatolewa kwa wananchi ni Mobile Bank na tawi la NMB Kiomboi halina Mobile Bank.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuwa mpiga debe wa wananchi wa Shelui kushawishi benki hizi kupeleka Mobile Bank katika tawi la benki NMB Kiomboi, ili miji midogo ya Shelui, Ndago na mingine iweze kupata huduma hii ya kibenki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi maswali yenye ya nyongeza marefu.

**NAIBU WA FEDHA (MHE. JANETH Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, naahidi nitajitahidi kwa uwezo wangu kuwashawishi mabenki husika kuweka ATM kufanya tathmini na kuweka ATM katika eneo la Shelui hasa kwa sababu amenihakikishia kuwa vigezo vyote vinaweza kuwa vipo. (Makofi)

Na. 119

#### **Ukarabati wa Kivuko cha Kamsamba**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Wakati wa Serikali ikiendelea na kutafuta fedha za kujenga Daraja la Mto Mombasa wananchi wa Wilaya ya Sumbawanga Vijijini na Kamsamba – Mlowo wilaya ya Mbozi wanaendelea kuteseka kwa kulipia kivuko kidogo cha Kamsamba kinachomilikiwa na Kanisa Katoliki kwa Shilingi 500 kwa mtu anayevuka na Shilingi 1000 kuvusha gunia la kilo 100 kwa madai kuwa fedha hizo zinatumika kukarabati kivuko kinapoharibika.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kufanya mazungumzo na mmiliki ili ukarabati huo ufanywe na Serikali ili kuondoa kabisa kero inayowapata wananchi wanaotumia kivuko hicho?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Kivuko anachozungumzia Mheshimiwa Mbunge ni daraja la watembea kwa miguu lililoshikiliwa na kamba, cable supported Pedestrian Bridge lililopo katika kijiji cha Kilyamtundu wilaya ya Sumbawanga Vijijini na kijiji cha Kamsamba wilayani Mbozi.

Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, daraja hilo la watembea kwa miguu linamiliikiwa na kanisa Katoliki Parokia ya Kamsamba, hivyo Serikali haina mpango wa kuingilia taratibu za uendeshaji wake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali Namba 119 la Mheshimiwa Silinde tarehe 10 Februari, mwaka huu 2012 Serikali tayari imefanya usanifu wa daraja la kudumu katika mto Momba lenye urefu wa mita 75. Katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga shilingi milioni 180 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo. (Makofi)

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuonyesha kutatua tatizo la ujenzi wa daraja. Lakini bado ninalo swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, yapata miaka 51 tangia wamisionari wajenge daraja hilo ili kuwasaidia wananchi kuweza kuvuka lakini baada ya misionari hao kuondoka wananchi wamekuwa wakitozwa tozo la kivuko hicho wakiwemo watoto, wagonjwa, wakinama wajawazito na wale wanaoshindwa kuwa na fedha ya kulipa hulazimika kuvuka kwenye maji na kunusuru maisha yao kukamatwa na mamba au kwenda na maji.

Je, Serikali haioni kuwa ni changamoto inayopaswa kushughulikiwa na Serikali mapema ili kuokoa maisha ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikupongeza kwa namna unavyolifua tilia suala hili la kuweza kuokoa maisha ya wananchi na ndiyo maana Serikali imeshaamua kujenga daraja badala ya kutumia hicho kivuko ambacho ni hatari kwa maisha ya wananchi. Kwa hiyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inakuuhakikishia kwamba itajenga daraja hilo.

Na. 120

#### **Barabara ya Kisarawe Maneromango**

**MHE. SELEMANI S. JAFO** aliuliza:-

Je, ujenzi wa barabara ya lami yenyе urefu wa kilomita 54 kutoka Kisarawe hadi Maneromango utaanza na kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kisarawe – Maneromango, yenyе urefu wa kilomita 54 ni barabara ya Mkao inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia wakala wa barabara nchini TANROADS. Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kuanzia Kisarawe Mpuyani hadi Maneromango unatarajiwa kuanza baada ya kuanza kwa upembizi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali imekamilisha taratibu za kumpata mhandisi mshauri kwa ajili ya kufanya upembizi yakinifu na usanifu wa kina ambapo mhandisi mshauri MAKCONSULT amepatika na mkataba umesainiwa tarehe 17 Oktoba, 2012. Ni matarajio yetu kuwa kazi ya upembizi yakinifu na usanifu itakamilika katika mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Lengo la usanifu ni pamoja na kujua gharama za ujenzi ili kuingiza katika makisio ya Bajeti zizajo kwa ajili ya kuanza ujenzi kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha Wizara yangu kuititia Wakala wa Barabara itaendelea kufanyia matengenezo barabara hii ili iendelee kuitika majira yote ya mwaka wakati maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami yanaendelea.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Selemani Jafo swali lingine la nyongeza.

**MHE. SELEMANI SAID JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, nilitaka kujua, kwa sababu katika mwaka wa fedha 2011/2012 swali hili niliuliza na inaonekana mpaka hivi sasa ndiyo mpembuzi yakinifu amepatikana na mkataba umesaliniwa.

Sasa nataka kujua ahadi halisi ya Serikali mara baada ya upembuzi yakinifu utakapokamiliika.

Je, Serikali ipo tayari sasa katika mwaka wa Bajeti unaokuja kwamba Bajeti ioneshe wazi kwamba ujenzi wa barabara ya lami Kisarawe unakwenda kuanza mara moja?

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yetu kuna watu wamewekewa alama ya bomoa na alama za X, bahati mbaya maeneo yao wanashindwa kuyaendelea kutokana na suala zima la sheria. Je, ni utaratibu gani sasa umewekwa na Serikali kwamba watu hawa sasa wako katika utaratibu wa kulipwa haraka iwezekanavyo ili mradi waweze kuwa huru?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selemani Said Jafo kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa kwa niaba ya Waziri naomba nimpongeze Mheshimiwa Jafo kwa namna anavyofuatalia ujenzi wa barabara hii ambayo ni muda mrefu imeahidiwa kujengwa.

Kuhusu mara moja kuanza kujengwa, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba tukimaliza usanifu ndiyo tutajua gharama halisi za kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Pia, katika usanifu ndiyo tutajua kabisa tathmini halisi ya wale watu wanaohitaji kulipwa fidia. Sheria inaruhusu watu ambao barabara imewafuata kulipwa fidia lakini kama uko ndani ya hifadhi hawataweza kulipa fidia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bahati mbaya sana muda umekwisha lakini nimejitahidi kurusha pia maswali yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, sasa niwatambue baadhi ya wageni waliopo katika ukumbi huu.

Wageni waliopo katika ukumbi huu kwanza yupo Mheshimiwa Balozi wa Marekani Mheshimiwa Alfonso Reinhard na maafisa wake wawili. Naomba tuipongeze nchi ya Marekani kwa uchaguzi mzuri ambao Mheshimiwa Barrack Obama amechaguliwa tena.

Waheshimiwa Wabunge mu-applause, muwapigie makofi. Naomba muwashangilie Wamarekani, si ndiyo hivyo? Mheshimiwa Balozi wa Marekani tunaomba usimame! Ahsante sana! Pia ameongozana na Maafisa wake wawili. (Makofi)

Lakini pia tunaye Balozi wa Uingereza Mheshimiwa Diana Korna, naye pia ameongoza na maafisa wake wawili. Mheshimiwa Balozi karibu sana. (Makofi)

Vilevile, tunaye Mwenyekiti wa Mkoa wa Lindi ni maarufu anaitwa Mwenyekiti wa Wenyeviti wote wa CCM nchini hapa, Mheshimiwa Mohamed Mchopa. Mzee huyu ndiye Mwenyekiti wa Mkoa wa Lindi na maarufu, ye ye akisimama na mtu mwingine itabidi aache tu.

Kwa hiyo, tunakupongeza sana Mzee kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine. Lakini ameongozana na Katibu wa Mkoa Bi. Angelina Geti. Ahsante na karibuni sana. (Makofi)

Wageni wengine waliofika kwa ajili ya mafunzo, wapo viongozi watano wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wakiongozwa na Rais wa chuo Ndugu Paul Yunge, hawa wapo wapi? Ah! Mpo wachache tu, karibuni sana na msome kwa bidii. (Makofi)

Vilevile tuna wanafunzi 52 kutoka Chuo Kikuu cha Tiba na Afya cha IMTU cha Dar es Salaam, wasimame walipo. Kumbe mlikuwa hamjaondoka, mpo, karibuni sana na ninyi pia msome kwa bidii tunawahitaji sana katika maeneo yetu, Madaktari wanatakiwa sana. Karibuni sana. (Makofi)

Sasa tuna warembo, wapo warembo 16 wanaoshiriki shindano la Miss Utalii leo hapa Dodoma wameambatana na viongozi wao watatu pamoja na Walimu wawili. Hawa warembo wako wapi? Ooh! kumbe wapo hapo! Karibuni sana warembo tunawatakia kheri na ahsante sana pia mfanye kazi hiyo kwa uadilifu. (Makofi)

Wapo pia Umoja wa Vijana 20 wa Kanisa la TAG Area 'E' Dodoma, wako wapi? Ahsante na karibuni sana pia tunawatakia kheri katika mafanikio yenu. (Makofi)

Pia tuna wanafunzi 60 na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Gairo B, wako wapi na Walimu wao? Ah! Ahsanteni na karibuni sana tunawatakia masomo mema.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni 14 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Naibu Waziri wa Elimu TAMISEMI ambao ni wajumbe wa Mkutano wa CCM Taifa kutoka Ruangwa Lindi wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Issa Njinjo Mwenyekiti wa Wilaya ya Luangwa.

Naomba wasimame wajumbe hawa wa Mkutano Mkuu. Ahsante sana na karibuni, mpaka mmefikia hapa mmEchaguliwa na kwa hiyo ninawapongeza sana kwa uchaguzi mlioufanya huko mlilotoka. (Makofi)

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Selemani Said Jafo, ambao ni Ndugu Asha Shame Vuai na mtoto wake, karibuni sana na ahsanteni sana. (Makofi)

Pia, tuna wageni watano wa Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere wakiongozwa na Ndugu Frank Maira, hawa wageni watano wa Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere wako wapi? Ahsanteni sana na karibuni sana. (Makofi)

Kadhalika, tuna wageni wa Mheshimiwa Said Musa Zubeir ambaye ni Mohamed Ghalib Hajji, sijui ni nani ye ye lakini ahsante na karibu sana. Ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wawe na kitu fulani maana yake otherwise kila mtu yupo hapa. (Makofi)

Kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Mansour Shanif Hiran, ambao ni Ndugu Benjamin Samson Mwenyekiti wa Kijiji cha Kikubiji na Ndugu Mericki Mliyungu Kaimu WEO Kikubiji. Naomba hawa wasimame walipo. Ah! Ahsante sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, niingie kwenye Matangazo ya Kazi, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao chao kwenye Basement.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimwa Jenista J. Mhagama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao katika ukumbi namba 227, jengo la Utawala.

Mwenyekiti wa Masuala ya UKIMWI Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 watakuwa na kikao katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Pia, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madara ya Bunge Mheshimiwa Brig. General Hassan Ngwilizi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba watakuwa na kikao leo, sina uhakika na saa waliyopanga, nafikiri wapendelee saa saba na kikao hicho kitafanyika katika ukumbi namba 219. Ni Saa saba kwani saa tano hapaba tuna shughuli ambazo tunataka wote tuwepo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao katika ukumbi wa Pius Msekwa C.

Vile vile, Katibu wa Wabunge wa CHADEMA Mheshimiwa David Silinde, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kuwa leo saa 7.00 tarehe 9 Novemba, 2012 lakini saa 7.00 mchana baada ya Kuahirisha Bunge kuwa watakuwa na kikao chao katika ukumbi wa Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, CHADEMA saa 7.00 watakuwa na kikao chao katika ukumbi wa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Pia, Wabunge wa Mikoa inayolima Pamba watakuwa na mkuano wao ambao ulikuwa ufanyike jana usiku lakini haukufanyika. Sasa watakuwa na kikao hicho saa 7.00. Sasa ukumbi wa Msekwa hapo mtajua wenyewe maana mmeshasema ukumbi wa Msekwa kama mara tatu.

Vilevile Waziri wa Katiba na Sheria anawaalika Wabunge wote kwenye uzinduzi wa report yao ya Gender utakaofanyika kesho Jumamosi katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 4.00 asubuhi.

Kwa hiyo, haya ndiyo baadhi ya matangazo tuliyonayo. Lakini Waheshimiwa Wabunge tuendelee.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoangalia sasa hivi ni karibu saa tano na leo ndiyo siku ambayo tulipanga kufunga mkutano huu. Kwa hiyo, kama ambavyo mmeona leo katika orodha ya shughuli za leo tumepanga shughuli zote zilizobakia ambazo zilipangwa katika mkutano huu wa tisa wa Bunge. Shughuli zote hizo ni muhimu na zenye maslahi makubwa kwa nchi yetu.

Hata hivyo, muda tulionao wa majadiliano ni mdogo sana na nikiruhusu ziwasilishwe na kujadiliwa hoja zote zilizopangwa sitakuwa nimewatendea haki wahusika kwani mjadala hauwezi kuwa na tija na manufaa kwa taifa. (Makof)

Kwa msingi huo na kwa kutumia mamlaka niliyopewa na kanuni ya 5(1) na kanuni ya 8(a) ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2007, na baada ya kushauriana na Wabunge wenyewe hoja binafsi, tumekubaliana kuwa muda tulionayo hautoshi kukamilisha kikamilifu shughuli zilizopo katika orodha ya siku ya leo. Hivyo, natumia kanuni ya 30(6) ya Kanuni za Bunge ambayo inasema hivi:-

"shughuli za Bunge kutoka kila kikao zitatekelezwa kwa kufuata orodha ya shughuli za siku hiyo au kwa kufuata utaratibu mwingine amba Spika ataagiza uflatwe kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za Bunge."

Kwa hiyo, naelekeza kwamba hoja binafsi za Wabunge zote ambazo zimepangwa leo zitaahirishwa hadi Mkutano wa Kumi wa Bunge kupangiwa nafasi ili ziweze kuwasilishwa na kujadiliwa vizuri. Aidha, kauli ya Waziri wa Katiba na Sheria ambayo ilikuwa itolewe leo inaondolewa na kubakiza kauli moja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na hiyo itatoa nafasi ya kutosha kwa taarifa yangu mimi ninayokusudia kuitoa leo. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunaendelea! Katibu tuongoze!

### **KAULI ZA MAWAZIRI**

#### **Hali ya Chakula Nchini**

**KATIBU WA BUNGE:** Kauli za Mawaziri, kauli ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa kauli ya Serikali juu ya Hali ya Chakula Nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba nchi yetu iko salama kwa upande wa chakula na hivyo hakuna wasiiasi wa hali tete ya kuwepo kwa njaa. Hali iliyopo ni baadhi ya maeneo nchini kuwa na upungufu wa chakula na kupanda kwa bei ya Mahindi ambapo wafanyabiashara nao wametumia fursa hii kuingia sokoni na kununua Mahindi kwa bei ya juu.

Pamoja na changamoto hii NFRA ina akiba ya kutosha ambayo itaendelea kupelekwa kwenye maeneo yaliyobainika kuwa na uhaba, hivyo hakuna mwananchi atakayekufa kwa njaa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 uzalishaji wa chakula nchini ulikuwa wa kuridhisha, tathmini ya uvunaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2011/2012 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2012/2013 iliyofanywa mwezi Juni, 2012 ilionesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa ujumla katika msimu huo ulifikia tani milioni 13.6 zikiwemo tani milioni 7.6 za nafaka na tani milioni 6 za mazao yasiyo ya nafaka.

Uzalishaji huo utakidhi mahitaji ya chakula ya tani milioni 12 kwa mwaka 2012/2013 na kuwepo kwa ziada ya tani milioni 1.6 za chakula. Hivyo, nchi yetu inajitosheleza kwa asilimia 115.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wanaoondoka mwondoke kwa ustaha jamani.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya upatikanaji wa chakula imeendelea kuwa ya kuridhisha, pamoja na hali ya chakula kwa ujumla kuwa ya kuridhisha, kuna baadhi ya maeneo yenye uhaba wa chakula kutokana na mvua kutonyesha vizuri katika maeneo yanayopata mvua za vuli na katika baadhi ya maeneo. Uhaba wa chakula umesababisha kupanda sana kwa bei za chakula katika maeneo husika.

Tathmini ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini imebaini kuwepo kwa ziada ya chakula katika mikoa saba ya Iringa, Rukwa, Mbeya, Kagera, Mtwara, Kigoma na Ruvuma. Utoshelevu katika mikoa nane ya Morogoro, Pwani, Mara, Tanga, Lindi, Mwanza, Singida, Dodoma na uhaba katika mikoa sita ya Shinyanga, Tabora, Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Dar es Salaam. Uzalishaji wa chakula nchini hususan nafaka kwa msimu wa kilimo mwaka 2011/2012 ulifkia tani milioni 7,558,342 wakati mahitaji yetu ni tani milioni 7,551,244 na hivyo kujitosheleza na kuwa na ziada ndogo ya tani 7,097 za nafaka. Ziada hii ni ndogo hivyo ni lazima itumike kwa uangalifu. Aidha, uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo ya nafaka kwa maana ya Viazi, Muhongo, Ndizi, Maherage na kadhalika unakadirwa kuwa tani milioni 6,014,463 wakati mahitaji ya taifa ni tani milioni 4,438,870 hivyo kuwa na ziada ya tani milioni 1,575,592.

Mheshimiwa Spika, tathmini imebainisha pia kuwepo kwa uhaba wa chakula katika Halmashauri 63 zilizo katika mikoa 17 katika viwango tofauti.

Aidha, Halmashauri 35 katika mikoa 12 tayari zimeidhinishiwa na Kamati ya maafa jumla ya tani 18,417.8 za chakula cha msaada kwa miezi miwili mpaka mitatu kwa kipindi cha Novemba, 2012 mpaka Januari, 2013 kwa ajili ya watu 526,607 walioainishwa kuwa na uhaba wa chakula wa kukithiri.

Mheshimiwa Spika, bei za mazao. Bei ya mazao ya nafaka katika masoko makuu nchini bado iko juu. Kwa mfano, uchambuzi wa bei za vyakula unaonyesha kuwa bei ya wastani ya Mahindi kwa kilo kitaifa mwezi Septemba ilikuwa shilingi 540 kwa kilo wakati bei ya tarehe 15 Oktoba ilikuwa ni shilingi 570 kwa kilo moja.

Mwelekeo huu unaonyesha kuwa bei inaendelea kupanda ikilinganishwa na miezi ya Juni hadi Septemba, 2012. Hali hii inaashiria kupungua kwa kiasi cha Mahindi kinachoingia sokoni wakati huu. Aidha, bei ya wastani ya Mahindi kwa mwezi Septemba, 2012 katika masoko ya miji mikuu ya mikoa 10 iko juu ya bei ya wastani wa kitaifa wa shilingi 540 kwa kilo. Baadhi ya masoko hayo ni Mwanza shillingi 670, Tabora shillingi 660, Musoma shillingi 620, Bukoba shillingi 610, Dar es Salaam shillingi 600 na Shinyanga shillingi 600. Aidha, bei ya wastani ya Mchele kitaifa hivi sasa ni shilingi 1,640/= kwa kilo, hili ni ongezeko la asilimia  $3 \frac{1}{2}\%$  ikilinganishwa na bei ya mwezi Agosti, 2012 au 21% ikilinganishwa na mwaka jana 2011 kipindi kama hiki.

Mheshimiwa Spika, hali ya chakula duniani na nchi jirani. Taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Taifa (FAO) iliyotolewa mwezi Juni, 2012 inaonyesha kuwa katika mwaka 2011/2012 uzalishaji wa nafaka duniani utaongezeka kwa 3.2%.

Jumla ya tani milioni 2,419 za nafaka zitazalishwa ikilinganishwa na matumizi ya nafaka ya tani milioni 2,376 kwa mwaka 2012/2013, matumizi ya nafaka kwa ajili ya chakula cha mifugo yataongezeka kwa asilimia 3.8 wakati matumizi ya chakula yanatazamiwa kuongeza kwa asilimia 1 na kiasi kikubwa kwenda sambamba na ukuaji wa watu duniani. Akiba ya nafaka duniani inatazamiwa kufikia tani millioni 36, ikiwa ni ongezeko kidogo kutoka kiwango cha mwaka jana.

Kutokana na ongezeko hilo, takriban nchi 66 duniani zilizo kwenye kundi la nchi maskini zenyenipato kidogo zinatazamiwa kunufaika na uzalishaji ulioongezeka na hivyo kupunguza kwa kiasi uagizaji wa nafaka kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko hilo, uzalishaji wa mazao ya chakula unatazamiwa kupungua na hivyo kusababisha Uhaba wa chakula kwa viwango mbalimbali kwa mwaka 2012/2013 katika takriban nchi 36 duniani hasa kutoka kundi la nchi maskini zenyenipato kidogo za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kwa ujumla nchi nyingi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika ni mionganoni mwa nchi hizo ambapo baadhi ya nchi jirani hususan, Burundi, Congo (DRC), Kenya, Sudan ya Kusini, Somalia, Madagascar, Malawi na Msumbiji zinatazamiwa kuwa na maeneo yatakayokabiliwa na uhaba wa chakula kutokana na sababu mbalimbali hasa ukame, mafuriko na vita vya wenye kwa wenye kwa wenye.

Kutokana na Uhaba huo na ikizingatiwa kuwa nyingi ya nchi hizo ziliikuwa na uhaba mkubwa wa chakula kwa mwaka jana, bei za nafaka katika maeneo hayo hususan Kenya, Uganda, Sudan ya Kusini zimeendelea kupanda kuanzia kipindi cha Januari hadi Mei, 2012. Bei za juu zaidi zimeripotiwa katika masoko ya Juba, Kampala na Nairobi.

Kwa mfano, bei ya mtama katika soko la Juba, Sudani ya Kusini kwa mwezi Aprili, 2012 imepanda kwa asilimia 145 ikilinganishwa na ile ya mwaka jana kipindi kama hicho, wakati bei ya mahindi Soko la Kampala kwa mwezi Mei, 2012 imepanda hadi kufikia dola za Kimarekani 390 kwa tani au shillingi 616,200 za Kitanzania kwa tani sawa na ongezeko la asilimia 40 ikilinganishwa na viwango vya mwezi Mei, 2011. Aidha, kati ya mwezi Septemba na Oktoba, 2012 bei ya jumla hususan ya mazao ya nafaka katika nchi jirani imepanda na kuchochera kwa kiwango kikubwa ongezeko la biashara ya mazao ya chakula kutoka nchini kwenda nchi hizo zenyenipato ya chakula. Aidha, hali hiyo imechochera ongezeko kubwa la bei ya chakula katika masoko ya miji mikuu ya mikoa katika maeneo ya mipakani na hivyo kuathiri usalama wa chakula hasa kwa wananchi wa kipato cha chini wenye uwezo mdogo wa kujinunulia chakula.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali. Ili kukabiliana na hali ya uhaba wa chakula, hususan nafaka katika mwaka 2012/2013 na kuendelea kupanda kwa bei za vyakula, Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuhamisha sehemu ya akiba ya nafaka iliyopo kwenye maghala yaliyopo Sumbawanga, Makambako na Songea kwenye ziada kwenda kwenye maghala ya Dar es Salaam, Dodoma, Shinyanga na Arusha yaliyo karibu na maeneo yenye uhaba wa chakula.

Hatua hiyo itaiwezesha Serikali kukabiliana na uhaba wa chakula na mahitaji mengine ya soko kwa haraka zaidi.

Hadi sasa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) ina akiba ya takribani tani 100,000 na inaendelea kununua nafaka kutoka kwa wakulima wa mikoa ile iliyozalisha ziada hususan, mikoa ya Rukwa, Iringa, Mbeya na Ruvuma.

(ii) Kuhimiza wananchi kutumia aina mbalimbali za vyakula ikiwa ni pamoja na muhogo, viazi vitamu, viazi mviringo, ndizi na vyakula vingine ambavyo vinapatikana kwa wingi katika maeneo yao.

(iii) Serikali imeagiza mikoa na Halmashauri za wilaya zenyenye uhaba wa chakula kuongeza upatikanaji wa chakula katika maeneo yao kwa kuhamasisha wafanyabiashara wenyenye uwezo wa kununua chakula kutoka mikoa yenye ziada na kuuza kwenye maeneo yenye uhaba wa chakula.

(iv) Wakulima wanashauriwa kutumia vizuri mvua zinazoanza kunyesha sasa kupanda mbegu za mazao yanayokomaa haraka. Tayari maandalizi muhimu ya msimu wa kilimo wa 2012/2013 yamekamilika kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na kufikisha mbolea Wilayani na baadhi ya Vijiji.

(v) Halmashauri zote zihakikishe kwamba skimu zote za umwagiliaji na mabonde yenye unyevunyevu zinatumika kikamilifu na kuelekeza pembejeo muhimu za kilimo katika skimu hizó.

Serikali inawahimiza wananchi wote katika ngazi ya kaya hususan wakulima kuepuwa matumizi mabaya ya chakula ikiwemo kutengeneza pombe na ikibidi wauze ziada tu ili kuijiwekea akiba ya chakula cha kutosha kwa ajili ya mahitaji ya kaya zao mpaka msimu ujao.

Mheshimiwa Spika, Usambazaji wa Vocha na Pembejeo Msimu wa Kilimo wa 2012/2013: Ruzuku ya Pembejeo. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, jumla ya kaya 940,783 katika Mikoa 23 zitanufaika na ruzuku ya pembejeo kwa ajili ya mazao ya mahindi na mpunga ikilunganishwa na kaya 1,800,000 ambazo zilinufaika na ruzuku kwa mwaka 2011/2012.

Kati ya kaya hizó, kaya 640,783 zitatumia fedha za Serikali na kaya 300,000 zitatumia fedha za Benki ya Dunia. Aidha, ruzuku ya mtama na alizeti itahusisha jumla ya tani 402 za mtama kwa ajili ya ekari 190,000 na tani 366 za alizeti kwa ajili ya ekari 90,000 ambazo zitatolewa kwa wakulima wa mazao hayo.

Chini ya utaratibu huo, kila ekari moja ya mtama na alizeti itapata mfuko mmoja wa kilo 50 ya mbolea ya kupandia aina ya Minjingu Mazao ambapo jumla ya tani 14,000 za mbolea ya Minjingu Mazao zinatarajiwa kutumika.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora. Hadi tarehe 19 Oktoba, 2012, jumla ya tani 2,824.3 za mbegu bora zikiwemo tani 2,814.3 mahindi na tani 10 za mpunga ziliikuwa zimefikishwa kwenye Mikoa inayoanza msimu wa kilimo mapema ambayo mahitaji yake ni tani 2,232.6.

Makampuni ya mbegu yanaendelea kukamilisha uvunaji, usafirishaji na ufungashaji wa mbegu ili kuzipeleka mikoani. Mahitaji ya mbegu nchini ni tani 60,000. Tayari makampuni mawili yameshateuliwa kwa ajili ya upelekaji wa mbegu za mtama na alizeti kwa wakulima kuanzia tarehe 30 Oktoba, 2012.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji na usambazaji wa mbolea. Hadi tarehe 30 Septemba, 2012. Jumla ya tani 150,000 za mbolea kati ya mahitaji ya tani 400,000 zipo nchini. Jumla ya tani 85,495 za mbolea zinatarajiwu kuingizwa nchini ifikapo tarehe 30 Desemba, 2012. Aidha, jumla ya tani 18,977 kati ya tani 21,064 za mbolea ya Minjingu Mazao zinahitajika kwenye Mikoa inayotumia mbolea hii kwa kupandia zimekwishafikishwa katika maeneo ambayo msimu wa kilimo unaanza mapema na kiwanda cha Minjingu kinaendelea na upelekaji wa mbolea hiyo kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa vocha maeneo ambayo msimu wa kilimo unawahi. Mikoa ambayo msimu wa kilimo unawahi imekwishapelekewa vocha ambazo hazikutumika mwaka 2011/2012.

Jumla ya vocha 421,362 kati ya vocha 750,000 za mbegu na mbolea ya kupandia zinazotakiwa kugongwa mhuri zimepelekwa tarehe 27/8/2012 katika Mikoa ya Kigoma, Kagera, Geita, Mwanza, Mara, Shinyanga, Katavi (Wilaya ya Mpanda), Mbeya (Wilaya ya Rungwe na sehemu ya Wilaya za lleje na Mbeya Vijiji), Morogoro (sehemu za Wilaya ya Mvomero) na Njombe (Wilaya ya Makete na sehemu ya Wilaya ya Njombe Vijiji). Zoezi la kugonga vocha mihuri limekamilika. Vocha zitapelekwa Mikoa ya Katavi (Wilaya ya Mlele na kaya zilizobakia kwa Wilaya ya Mpanda), Njombe (Wilaya za Ludewa, Wanging'ombe na Wilaya ya Njombe kwa kaya zilizobakia), Iringa, Mbeya (Wilaya za Mbozi na Wilaya ya lleje kwa kaya zilizobakia).

Mheshimiwa Spika, uchapaji wa vocha. Hadi tarehe 25 Septemba, 2012, Kampuni zilizoomba kuchapisha vocha zilikwishafanyiwa tathmini na taarifa ya tathmini hiyo kuwasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata maoni yao na hatimaye kibali cha 'no objection'. Benki ya Dunia walirudisha maoni ambayo yalifanyiwa kazi na kupelekwa tena tarehe 5 Oktoba, 2012.

Baada ya mchakato wa maandalizi ya zabuni kwisha mzabuni aliyeshinda zabuni alipewa taarifa tarehe 18 Oktoba, 2012. Chini ya utaratibu huu, vocha 2,072,349 zitachapishwa.

Mheshimiwa Spika, makampuni kuteua mawakala. Makampuni ya mbegu na mbolea yanaendelea na uteuzi wa mawakala wa pembejeo katika Mikoa. Aidha, Wizara imeyahimiza makampuni ya pembejeo kuweka kipaumbele kwenye Mikoa ambayo msimu wa kilimo unaanza mapema. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Waraka wa Usimamizi wa Utekelezaji wa Ruzuku ya Pembejeo kwa mwaka 2012/2013 umekamilika na kutumwa Mikoa yote tarehe 25 Septemba, 2012. Waraka huo umewekwa kwenye tovuti ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ([www.kilimo.go.tz](http://www.kilimo.go.tz)).

Mheshimiwa Spika, Mikakati mingine ya baadaye itakayoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuimarisha usalama wa chakula ni pamoja na ifuatavyo:-

(i) Ili kukabiliana na kupanda kwa bei za vyakula kunakochangiwa kwa kiasi kikubwa na uzalishaji mdogo na ukame Serikali itaendelea kuimarisha mikakati ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kuongeza uwekezaji katika kilimo na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia SAGCOT, Feed the Future, Bread Basket; na kuongeza ruzuku ya pembejeo na mikopo ya zana bora za Kilimo.

(ii) Kuhakikisha kwamba skimu zote za umwagiliaji na mabonde yenye unyevunyevu zinasimamiwa ili zizalische chakula kwa wingi na kila inapoweza kana zaidi ya mara moja kwa mwaka.

(iii) Serikali itaendelea kujengea uwezo wa NFRA ili iweze kununua na kuhifadhi nafaka ya kutosha kukabiliana na maafa mbalimbali na kudhibiti bei za vyakula nyakati za uhaba. Lengo ni kununua tani 200,000 katika msimu wa ununuzi wa 2012/2013.

(iv) NFRA itaendelea kuimarisha uwezo wake wa kuhifadhi kutoka uwezo wa sasa wa kuhifadhi tani 241,000 za chakula kwa kukarabati maghala yaliyopo na kujenga maghala mapya yenye uwezo wa kuhifadhi tani 160,000 ili hatimaye iweze kuhifadhi angalau tani 400,000 ifikapo mwaka 2015.

(v) Serikali itaimarisha masoko (vituo) rasmi vya kuuzia mazao ili kudhibiti walangazi wanaokwepa kununua mazao yaliyovunwa kwa kununua mazao yakiwa bado shambani. Hatua hii itasaidia, kumpa bei nzuri mkulima na Serikali kupata ushuru wa mazao unaostahili kwa kiasi cha mazao yanayouzwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa chakula unaoendelea katika nchi jirani hususan Burundi, Congo DRC, Kenya, Sudan Kusini, Somalia na nchi nyingine. Kwa kuzingatia kuwepo kwa fursa za kuzalisha mazao katika nchi yetu, Serikali itajikita zaidi katika kuzalisha mazao ya kutosha ili kupata ziada ya kuuza kwa kutumia fursa ya soko la mazao katika nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**Uamuzi wa Spika Kuhusu Tuhuma Kwamba Baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini Walijihuisha na Vitendo vya Rushwa Katika Kutekeleza Kazi Zao za Kibunge**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema si mnafahamu Spika anaweza kutoa hotuba au Kauli yake wakati wo wote. (Kicheko/Makofi)

Kwa hiyo, nakusudia kutoa uamuzi Kuhusu Tuhuma kwamba Baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini walijihuisha na vitendo vya rushwa katika kutekeleza kazi zao za Kibunge. Hii inatolewa chini ya Kanuni ya 5(1) na Kanuni ya 72(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 na Kifungu cha 12(1), (2) na Kifungu cha 25 (c) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, tarehe 27 na 28 Julai, 2012 wakati wa mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, baadhi ya Wabunge walitoa michango mbalimbali na kuibua tuhuma zilizotolewa pia kwa maandishi, kwa barua ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Bwana Eliakim C. Maswi, kwa Katibu wa Bunge kama ifuatavyo:-

(a) Kwamba, baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini walikuwa wanaenda Ofisini kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuomba rushwa ili waitetee Wizara hiyo inapowasilisha taarifa mbalimbali kwenye Kamati hiyo;

(b) Kwamba, baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati hiyo wana mgongano wa kimaslahi (*Conflict of Interest*) katika kutekeleza majukumu yao ya kibunge ya kuisimamia Wizara ya Nishati na Madini, kwa kufanya biashara na Shirika la Usambazi wa Umeme (TANESCO);

(c) Kwamba, baadhi ya Wabunge wamekuwa wanajihuisha na vitendo vya rushwa kwa kupokea fedha kutoka kwenye Makampuni ya mafuta, kwa lengo la kuyatetea Makampuni hayo kwa kupinga uamuzi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Bwana Eliakim C. Maswi wa kutoa Zabuni ya Ununuzi wa mafuta mazito ya kuendeshea mitambo ya *IPTL* kwa Kampuni ya *PUMA Energy (T) Ltd.*; na

(d) Kwamba, kutokana na kupewa rushwa na baadhi ya Makampuni ya mafuta ili wayatetee, baadhi ya Wabunge walikuwa wanaendesha kampeni ya kukwamisha kuitishwa kwa Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, kwa mwaka wa Fedha 2012/2013. Hizi ndiyo zilikuwa tuhuma ambazo zilitolewa humu ndani.

Wakati wa mjadala huo, Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa, alitoa Hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1), 53(2) na 55(3) (f) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 kwamba, kwa kuzingatia kuwa michango mingi iliyotolewa na Wabunge wakati wa kuchangia hotuba hiyo imewatuhumu baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kujihuisha na vitendo vya rushwa, anaomba mambo yafutayo yafanyike:-

(a) Kamati ya Bunge na Nishati na Madini ivunjwe; na

(b) Tuhuma za vitendo vya rushwa zilizotolewa zifanyiwe uchunguzi na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Baada ya Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa kuwasilisha hoja yake, Bunge liliipitisha Azimio kwamba:-

"Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ivunjwe; na pia kwamba, tuhuma za vitendo vya rushwa zilizotolewa zichunguzwe na Kamati Ndogo ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na kumshauri Spika."

Katika kutekeleza Azimio hilo la Bunge, niliivunja Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa kutoa tamko la kufanya hivyo Bungeni, kwamba kwa mamlaka niliyonayo kwa mujibu wa Kanuni ya 113(3), ikisomwa pamoja na Kifungu cha 48(1) (a) cha Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya 1 [*The Interpretation of Laws Act (Cap.1)*] nilivunja ile Kamati.

Aidha, kwa kuzingatia kuwa kwa hali-asili yake, jambo hilo linahusu 'haki za Bunge' (*Parliamentary privilege*), nillipeleka kwenye Kamati Ndogo ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili Kamati hiyo ilifanyie uchunguzi na kunishauri. Kamati hiyo Ndogo ilipewa Hadidu ya Rejea moja tu, ambayo ni: "Kuchunguza na kumshauri Spika iwapo tuhuma kwa baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kujihuisha na vitendo vya rushwa ni za kweli au hapana."

Kwa hiyo, narudia hadidu hiyo illikuwa, Kuchunguza na kumshauri Spika iwapo tuhuma kwa baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kujihuisha na vitendo vya rushwa ni za kweli au hapana." Baada ya Kamati hiyo kukamilisha kazi yake, iliwasilisha taarifa yake rasmi kwangu ili kwa wakati muafaka, niweze kutoa uamuzi wa Spika kuhusu suala hilo. Sasa huu ndiyo wakati muafaka.

Kwa kuzingatia kuwa suala hilo linahusu: "Haki za Bunge" (*Parliamentary Privilege*), napenda nitoe maelezo ya ufanuzi kuhusu dhana hiyo kabla ya kutoa Uamuzi wa Spika, yaani dhana ya kupokea rushwa inahusu haki za Bunge.

Dhana ya Haki za Bunge (Parliamentary Privilege) na Madhumuni yake. Kwa ajili ya Uendeshaji bora wa shughuli zake, Bunge kwa mujibu wa Katiba na Sheria, limepewa kinga, madaraka na haki, fulani (*Immunities, Powers and Privileges*) ambazo zinaliwezesha kutekeleza majukumu yake kwa niaba ya wananchi, kwa uhuru, uwazi na uwajibikaji, bila ya kuingiliwa au kutishwa na mtu au chombo chochote cha Dola.

Katika Kitabu chake kiitwacho *"Treaties on the Law, Privileges, Proceedings and Usage of Parliament,* Mtaalamu Erskine May, ametoa tafsiri ya 'haki za Bunge' kama ifuatavyo:-

*"Parliamentary privilege is the sum of the peculiar rights enjoyed by the House collectively... and by Members of the House individually, without which they could not discharge their functions."*

Kwa tafsiri, nukuu hiyo inaeleza kwamba, "Maana ya haki za Bunge ni haki zote za kipekee za Bunge na za kila Mbunge binafsi kwa ujumla wake, ambazo bila kuwepo kwake, Bunge na Wabunge hawawezi kutekeleza majukumu yao."

Mwandishi mwingine aitwae Hood Phillips, ameeleza kwamba, kila Bunge linatekeleza madaraka na haki ambazo zinachukuliwa kuwa ni muhimu kwa hadhi ya Bunge, na pia katika kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake. Kwa ajili ya ufasaha zaidi, maelezo ya Mwandishi huyo kwa lugha alioitumia yanosomeka kama ifuatavyo:-

*"Each House exercises certain powers and privileges which are regarded as essential to the dignity and proper functioning of Parliament."*

Ufanuzi huo unaonesha kwamba, madhumuni ya msingi ya kuwepo kwa 'haki za Bunge' ni kuliwezesha Bunge na Wabunge kutekeleza ipasavyo majukumu yao ya Kikatiba.

Mtaalamu Erskine May ameelezea kuhusu madhumuni ya uwepo wa 'haki za Bunge' kama ifuatavyo:-

*"... certain rights and immunities such as freedom from arrest or freedom of speech belong primarily to individual Members of the House and exist because the House cannot perform its functions without the unimpeded use of the services of its Members. Other such rights and immunities, such as the power to punish for contempt and breach and the power to regulate its own constitution belong primarily to the House as a collective body, for the protection of its members and the vindication of its own authority and dignity. ... The term "privilege" is therefore used to mean those fundamental rights absolutely necessary for the exercise and due execution of constitutional powers and functions of the House."*

Maelezo hayo yanaonesha kwamba, uwepo wa 'Haki za Bunge' ni nyezo muhimu kwa ajili ya kulinda hadhi na heshima ya Bunge, na pia kwa ajili ya kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba ipasavyo. Maelezo hayo yanaonesha pia kwamba, haki hizo zinawalinda na kuwawezesha Wabunge kutekeleza majukumu yao ya kibunge ndani ya Bunge na Kamati zake, kwa uhuru, uadilifu na bila woga wa vitisho vyana namna yoyote ile, kutoka katika Mihimili ya Dola au Vyombo vingine vyana Dola au watu binafsi.

Mwaka 1873, Mbunge mmoja wa Bunge la Canada, alieleza kuhusu 'haki za Bunge' katika maneno yafuatayo:-

*"The privileges of Parliament are the privileges of the people, and the rights of Parliament are the rights of the people."*

Kwa Lugha ya Kiswahili, nukuu hiyo inaeleza kwamba; "Kinga za Bunge ni kinga za wananchi na haki za Bunge ni haki za wananchi." Kwa maneno mengine, 'haki za Bunge' hutumiwa na Bunge na Wabunge, kwa niaba ya wananchi wanaowawakilisha (i.e. Privileges are enjoyed by the House and by its Members on behalf of the citizens whom they represent).

Kwa nchi yetu ya Tanzania, msingi wa haki za Bunge letu ni Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoelekeza kwamba:-

"100(1): Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge.

(2) Bila ya kuathiri Katiba hii au masharti ya Sheria nyingine yoyote, Mbunge ye yeyote hatashtakiwa au kufunguliwa shauri la madai Mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge au kulileta kwa njia ya maombi, Muswada, hoja au vinginevyo."

Kwa mujibu wa masharti ya Ibara hiyo, haki za Mbunge Kikatiba ni zifuatazo:-

- (a) Kutoa mawazo yao Bungeni kwa uhuru na bila vikwazo au vitisho vyovyyote;
- (b) Kutohojiwa na Mahakama au chombo chochote nje ya Bunge kutokana na jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge; na
- (c) Kutofunguliwa mashtaka ya madai au jinai kutokana na jambo au mawazo aliyyoatoa Bungeni.

Haki na Kinga hizo zimetolewa kwa Bunge na Wabunge kwa ajili ya:-

- (i) Kulinda hadhi na heshima ya Bunge kama chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano chenye madaraka kwa niaba ya wananchi, ya kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake; na
- (ii) Kuwawezesha Wabunge kutekeleza majukumu yao ya Kibunge bila woga wala kuingiliwa.

Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act (Cap. 296)*), imeainisha kwa ufasaha za idhili haki za Bunge. Kifungu cha 12(2) cha Sheria hiyo, kimempa madaraka Spika kuamua kama Bunge lina mamlaka ya kusikiliza jambo lolote na kilitolea uamuzi kama linavunja 'haki za Bunge' (*breach of privilege*) na masharti ya Kifungu hicho ndiyo yaliyozingatiwa na yanaendelea kuzingatiwa katika kulisughulikia suala hili.

Napenda ieleweke kwamba, 'haki za Bunge' zinajumuisha pia haki ya kuendesha shughuli za Bunge katika Kamati za Bunge, kwa sababu Vikao vya Kamati ni sehemu ya Bunge na pia Kamati za Bunge zinafanya kazi kwa niaba ya Bunge lenyewe. Kwa kutambua hilo, Kifungu cha 5 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, kimetoa kinga kwa maneno

yaliyosemwa Bungeni au kwenye Kamati ya Bunge au yaliyoandikwa katika taarifa ya Bunge au Kamati ("... words spoken before or written in a report to the Assembly or Committee..."); na kwa sababu hiyo, Mbunge ana kinga ya kutoshtakiwa kijinai, wala kwa madai, kutokana na maneno aliyoysasema au taarifa aliyoitoa Bungeni au katika Kamati ya Bunge.

Napenda ieleweke pia kwamba, masharti ya Kifungu cha 12(1) na 13(1) vya Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge yanaelekeza kwamba, katika kutilia nguvu uhuru na haki zake, Bunge kwa kuzingatia Katiba na Kanuni za Bunge, lina madaraka ya kufanya yafuatayo:-

- (a) Kusikiliza na kuamua kuhusu mambo yote yanayovunja 'haki za Bunge' (*contempt or breach of privilege*) ndani ya Bunge, isipokuwa makosa ya kijinai.
- (b) Kuita na kuhoji mashahidi kwa ajili ya kuthibitisha jambo lolote linalohitaji kuamuliwa na Bunge au Kamati ya Bunge.

Kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 12(2) cha Sheria hiyo, uamuzi wa kama jambo fulani linavunja 'haki za Bunge' au la, unapaswa ufanywe na Spika, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Kanuni za Bunge.

Kutokana na madaraka aliyonayo kwa mujibu wa Kifungu cha 12(1) na (2) cha Sheria hiyo, Spika ana wajibu wa kulinda na kutetea haki za Bunge, kwa sababu bila ya kuwa na haki hizo za msingi ambazo ni uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu, ni dhahiri kwamba Bunge na Wabunge watashindwa kutekeleza majukumu yao ya Kikatiba na pia watashindwa kutekeleza wajibu wao kwa wapiga kura na wananchi wanaowakilisha kwa ujumla. Kama ilivyo kwa umuhimu kwa Mahakama, wa kuwepo kwa 'uhuru wa Mahakama' katika kutekeleza jukumu lake la utoaji haki, 'haki za Bunge' zina umuhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Kikatiba ya Bunge na kwa sababu hiyo, 'haki za Bunge' zinapaswa kulindwa na Bunge lenyewe, kuitia kwa Spika. Aidha, Vifungu vya 12(1) - (4) vya Sheria hiyo, vimetamka bayana kwamba, mambo yanayohusu 'haki za Bunge' yasiyo ya kijinai, yanaweza kutiliwa nguvu na Bunge lenyewe ndani ya Bunge na yale ambayo ni ya kijinai, yanapaswa kushughulikiwa na Mahakama.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa maelezo haya ya ufanuzi kuhusu dhana ya 'haki za Bunge', napenda sasa nirejee kwenye suala lenyewe ambalo ndiyo msingi wa Uamuzi nitakaoutoa.

**Msingi wa Suala Husika:** Kama nilivyooleza kwenye maelezo yangu ya utangulizi, msingi wa suala hili linalohusu 'haki za Bunge' ni tuhuma kwamba, baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini walijihuisha na vitendo vya rushwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya Kibunge.

Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri kwamba, tuhuma kuwa baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wanajihuisha na vitendo vya rushwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kibunge, ni suala linalohusu uvunjaji wa 'haki za Bunge' (*breach of parliamentary privilege*).

Hakuna ubishi kwamba, kitendo cha Mbunge kuomba au kupokea rushwa kwa madhumuni ya kutumia wadhifa wake kama Mbunge kutekeleza matakwa fulani ya Kampuni, Shirika au ya mtu ye yeyote binafsi, ni uvunjaji mkubwa wa 'haki za Bunge' (*a serious breach of parliamentary privilege*), na pia iwapo kimethibitika pasipo mashaka yoyote, ni kosa la jinai.

Kuhusiana na hilo, Erskine May ameelleza kwamba:-

*"The acceptance by a Member... of a bribe to influence him in his conduct as a Member, or of any fee, compensation or reward in connection with the promotion of or opposition to any bill, resolution, matter or thing submitted or intended to be submitted to the House, or to a Committee, is contempt."*

Tafsiri ya maelezo hayo ni kwamba, "upokeaji wa rushwa kwa Mbunge kama kishawishi cha kumfanya atende kazi zake za kibunge, au kama malipo, fidia au zawadi kwa ajili ya kuunga mkono au kutounga mkono Muswada wa Sheria, Azimio, au jambo lingine lolote lillowasilishwa au linalokusudiwa kuwasilishwa Bungeni, au kwenye Kamati ya Bunge, ni kitendo cha kulidhalilisha na kulifedhehesha Bunge."

Hali kadhalika, kitendo cha Mbunge kuomba au kupokea rushwa kwa madhumuni ya kutumia wadhifa wake kama Mbunge kutekeleza matakwa au maslahi fulani ya Kampuni, Shirika au ya mtu ye yote binafsi, kama kimethibitika pasipo mashaka yoyote, ni kosa la jinai, kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 28(1), (2) na 32 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Vifungu hivyo vinasomeka kama ifuatavyo:-

*"28(1): Any person who offers to any Member or Officer... either directly or indirectly any bribe, fee, compensation, gift or reward in order to influence such Member or Officer in his conduct as such member or officer or for or in respect of the promotion of or opposition to any Bill, resolution, matter, rule or thing submitted to or intended to be submitted to the Assembly shall be guilty of an offence.*

*(2) Any Member or Officer... who demands, accepts or receives directly or indirectly, any bribe, fee, compensation, gift or reward, the offering of which is or would be an offence under this section, shall be guilty of an offence."*

*"32. any Member who accepts or agrees to accept or obtains or attempts to obtain for himself or for any other person any bribe, fee, compensation, reward or benefit of any kind for speaking, voting or acting as such member or for refraining from so speaking, voting or acting on account of his having so spoken, voted or acted or having so refrained, shall be guilty of an offence..."*

Hoja ya Kutolewa Uamuzi: Waheshimiwa Wabunge, hoja ambayo natakiwa niitolee Uamuzi kuhusiana na suala hili ni moja tu, nayo ni je, kwa mujibu wa matokeo ya uchunguzi uliofanywa na Kamati Ndogo ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, tuhuma za baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kujihusisha na vitendo vya rushwa zimethibitishwa au hapana.

Kwa mazingira ya suala hili, nimeona kuna ulazima wa kueleza matokeo ya uchunguzi wa Kamati hiyo kwa kila tuhuma, kwa ajili ya kuondoa mashaka yoyote kwa Uamuzi nitakaoutoa.

Sehemu ya Pili; Matokeo ya Uchunguzi wa Kamati. Waheshimiwa Wabunge, tuhuma mahususi zinazohusu baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kujihusisha na vitendo vya rushwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kibunge zilizochunguzwa na Kamati Ndogo ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ni zifuatazo:-

- (a) Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, kwa mujibu wa barua yake kwa Katibu wa Bunge, Kumb. Na. SAB.88/223/01/28 ya tarehe 31 Julai, 1012 alimtuhumu Mheshimiwa Sara Msafiri Ally (MB.) kwamba, tarehe 6 Februari, 2012, Mheshimiwa huyo alikwenda ofisini kwa Katibu Mkoo huyo wa Wizara, Mjini Dodoma, ambapo alimwomba ampe rushwa ya Shilingi milioni hamsini kwa ajili ya kuwagawia baadhi ya Wabunge na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, ili watetee mipango ambayo Wizara ya Nishati na Madini itakuwa inaiwasilisha kwenye Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini iliandikwa barua kwa Katibu wa Bunge kama utetezi wake Katibu Mkoo huyo.
- (b) Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, kwa barua hiyo hiyo alidai kwamba, tarehe 4 Juni, 2012, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi (MB.), alimtaka Bw. Eliakim C. Maswi, awalipe Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Shilingi milioni mbili kila kila Mjumbe, ili awatulize au awazibe midomo wasiendelee kumshambulia ye (Bw. Eliakim C. Maswi), kutokana na utendaji wake waliokuwa wanaulalamikia.
- (c) Katika michango mbalimbali iliyotolewa Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wabunge kadhaa walituhumu baadhi ya Wabunge na pia Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kujihusisha na vitendo vya rushwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kibunge, kwa kupewa rushwa na Makampuni ya Mafuta ili wayatetee kuhusiana na Zabuni ya Ununuzi wa mafuta mazito ya kuendeshea mitambo ya IPTL.
- (d) Waziri wa Nishati na Madini, Mhe. Prof. Sospeter Muhongo (MB.), kuwatuhumu baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuwa na mgongano wa kimaslahi kwa kufanya biashara na Shirika la Kusambaza Umeme (TANESCO).

Matokeo ya uchunguzi wa Kamati kwa kila moja ya tuhuma zilizoainishwa hapo juu, kwa mujibu wa Taarifa ya Uchunguzi iliyowasilishwa na Kamati kwa kuzingatia Hadidu za Rejea iliyopewa ni kama ifuatavyo:-

Tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Sara Msafiri Ally (MB.), ya kwamba alimwomba Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, rushwa ya Shilingi milioni hamsini.

Kuhusiana na tuhuma hiyo, uchunguzi wa Kamati ulibaini yafuatayo:-

- (a) Kwamba, Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, aliibua tuhuma hiyo kama njia ya kujihami dhidi ya tishio la Wabunge; Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, ambao kwa ushahidi wake wa maandishi, Bw. Eliakim C. Maswi, ameeleza kwamba, walitamka ni lazima aachie nafasi yake ya Ukatibu Mkoo, kwa kuwajibika kutokana na utendaji wake usiordhisha.

Katika kutoa ushahidi wake alipouliwa na Kamati kwamba, "... Mheshimiwa Sara angekwambia uachie Ukatibu Mkoo usingemtuhumu kwamba alikuja kukuomba rushwa, ila ulilazimika kuzua tuhuma hizo baada ya kuona nafasi yako inatishiwa..." Bw. Eliakimu C. Maswi alijibu kama ifuatavyo:-

"Nakubali alitamka hivyo mbele ya Waziri Mkoo kwamba, mimi sina sababu za kuendelea kuwa Katibu Mkoo, sasa na mimi mtu akiniambia hivyo, na yeze kwa nini aendelee kuwa Mbunge?"

- (b) Kwamba, Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, ambaye kwa mujibu wa barua yake kwa Katibu wa Bunge, Kumb. Na. SAB. 88/223/01/28 ya tarehe 31 Julai, 2012 ndiye alitoa tuhuma hii na ndiye aliyekuwa na jukumu la kuthibitisha, ameshindwa kuthibitisha ukweli wa tuhuma yake.

Kwamba, ukweli wa tuhuma kuwa Mheshimiwa Sara Msafiri Ally ... (Makof)

Mimi sijatoa uamuzi, nasema tu Kamati ilivyoona. Kwamba ukweli wa tuhuma kwamba Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, aliomba rushwa ya Shilingi milioni hamsini kutoka kwa Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi haukuthibitika. Kilichothibitika ni kwamba, Katibu Mkoo huyo alizua tuhuma hii kwa nia ya kujihami dhidi ya baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini waliokuwa wanahoji kuhusu utendaji wa Wizara yake, hususan ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma katika ununuzi wa mafuta ya kuendeshea mitambo ya kufua umeme ya IPTL na utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa umeme wa dharura.

Tuhuma ya pili; tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi kwamba alimwomba Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, rushwa ya Shilingi milioni mbili kila Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini.

Kuhusu tuhuma hii, uchunguzi wa Kamati ulibaini yafuatayo:-

Kwamba, matamshi ya baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, amba ni Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi kwamba, ni lazima Bw. Eliakim C. Maswi, aachie nafasi kwa sababu hastahili kuwa Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati na Madini, yalimfanya Katibu Mkoo huyo atafute mbinu ya kujihami dhidi ya tishio hilo.

Mbinu aliyoitumia ni kutaka kuwalipa fedha Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, shilingi milioni mbili kila Mjumbe, kwa sharti la kuwataka wamsainie nyaraka za kukiri kupokea fedha hizo, lakini mbinu hiyo haikufanikiwa na mbinu hiyo iliposhindikana, aliamua kuzua tuhuma za rushwa dhidi ya Wabunge hao.

Kwamba, Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, ndiye alitaka kuwalipa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa lengo la 'kuwafunga midomo' wasiendelee na madai yao ya kumtaka awajibike kwa kuachia nafasi ya Ukatibu Mkoo wa Wizara, kuhusiana na suala la utekelezaji usioridhisha wa Mpango wa Uzalishaji wa Umeme wa Dharura (billioni 408) na kuhusiana na ununuzi wa mafuta mazito ya kuendeshea mitambo ya IPTL kutozingatia Sheria.

Tuhuma nyingine zilizotolewa na Wabunge wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, kwamba baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, wanajihuisha na vitendo vya rushwa katika

utekelezaji wa majukumu yao ya kibunge, kwa kupewa rushwa na Makampuni ya Mafuta ili wayatetee kuhusiana na Zabuni ya Ununuzi wa Mafuta Mazito ya Kuendeshea Mitambo ya IPTL. Katika Uchunguzi wake kuhusu tuhuma hii, Kamati ilibaini yafuatayo:-

Kwamba, katika Wizara ya Nishati na Madini kulifanyika ununuzi wa dharura wa mafuta mazito kiasi cha zaidi ya lita milioni kumi kutoka katika Kampuni ya PUMA Energy (T) Ltd., kwa ajili ya kuendeshea mitambo ya IPTL. Ununuzi huo ulifanyika wakati tayari Shirika la Kusambaza Umeme (TANESCO), lilishaingia Mikataba na Kampuni nyingine kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya aina hiyo, na kwa lengo lile lile la kuendeshea mitambo ya IPTL, hali ambayo ilizua shaka kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ambaye kwa kuamini kwamba utaratibu wa ununuzi wa mafuta hayo uliofanywa na Wizara ulikuwa umekiuka Sheria ya Ununuzi wa Umma, Namba 7 ya Mwaka 2011, alianza kuwashawishi (*lobbying*), Wabunge kadhaa ili waunge mkono hoja yake aliyokusudia kuiwasilisha kwa ajili ya kuitaka Serikali itoe maelezo kuondoa shaka hiyo ya ukiukwaji wa Sheria.

Kwamba, kutoptana na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kushikilia msimamo wa kutaka hatua zichukuliwe dhidi ya Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bw. Eliakim C. Maswi na baadhi ya Wabunge ambaoni Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Vick Kamata na Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, walanza kutilia shaka msimamo huo, wakidhani kwamba, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka alikuwa amepewa rushwa na Makampuni ya Mafuta.

Kwamba, tuhuma hii kuwa baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini walikuwa wamepewa rushwa na Makampuni ya Mafuta ili waibane Wizara ya Nishati na Madini kuhusu ununuzi wa mafuta ya kuendeshea mitambo ya IPTL kufanya kinyume cha utaratibu uliowekwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma, haikuweza kuthibitika kama ilivyooneshwa na majibu ya Wabunge walioitoa tuhuma hiyo Bungeni, walipotakiwa watoe ushahidi kuthibitisha ukweli wake:-

- (i) Mheshimiwa Joseph R. Selasini: Mheshimiwa Joseph R. Selasini alitamka Bungeni kwamba:-

*"Makampuni ya Mafuta yalikuwa hapa Dodoma yakigawa fedha. Ni lazima niseme kuna wenzetu wanasema kwa sauti kubwa, kuna wenzetu wanasema kwa mbwembe, lakini sasa naamini wanasema kwa nguvu ya chochote kilicho mfukoni..."* Haya maneno aliyasema humu ndani.

Alipotakiwa na Kamati kuthibitisha ukweli wa tuhuma hiyo, majibu ya Mheshimiwa Joseph R. Selasini, yalikuwa kama ifuatavyo:-

*"... Kabla Hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini haijasomwa Bungeni, kulikuwa na minong'ono mingi sana kwamba, baadhi ya Wabunge na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, walikuwa wamepewa fedha ili kutoa ushawishi wa kukwamisha Bajeti hiyo na kushinikiza Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo wawajibike kwa kuachia nyadhifa zao. ... Lazima niwe wazi, majina ya Wabunge hao yalikuwa yanatajwa; Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Zedi, Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Tambwe, Mheshimiwa Sara Msafiri na Mheshimiwa Zitto Kabwe, ingawa binafsi sina ushahidi kama kweli walichukua fedha au hawakuchukua."*

Mheshimiwa Selasini anaendelea; *"Kwa kutambua kwamba rushwa ni kitu kibaya, na nikiwa Mbunge, napaswa kusimamia public interest, niliamua kuzungumza ili mjadala mpana*

ufanyike na kama yeote ana ushahidi utolewe... kwa ajili ya kunusuru hadhi na heshima ya Bunge letu." Mwisho wa kunukuu.

Kamati ilimwuliza swalii: "Kwa hiyo, huna ushahidi wowote kuhusu Mbunge nani kapewa rushwa, nani kapokea rushwa, zilikuwa tuhuma tu?"

Jibu la Mheshimiwa Selasini: "...Mimi sina ushahidi wa moja kwa moja kwamba fulani kapokea na kapokea kiasi gani. Kama nilivyosema, Wabunge katika ujumla wao walikuwa wanatuhumu na sijui kama walikuwa na ushahidi au hawana."

Hayo ndiyo maelezo ya Mheshimiwa Joseph Selasini.

Mheshimiwa John John Mnyika: Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Nishati na Madini, Mhe John John Mnyika, wakati akiwasilisha Maoni ya Kambi hiyo Bungeni alitamka kama ifuatavyo:-

"...Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba, kuna kampeni kubwa inafanywa ndani na nje ya Bunge ili Uamuzi wa Katibu Mkoo wa Wizara ya Nishati, Bw. Eliakim C. Maswi, ubatilishwe kwa maslahi ya Makampuni yaliyokosa Zabuni ya kuiuzia TANESCO mafuta ya kuendesha mitambo ya kufua umeme ya IPTL na Wapambe wake wa ndani na nje ya Bunge. Aidha, wanaoendesha kampeni hiyo wanashinikiza Katibu Mkoo huyo ajuzulu kwa kile kinachoitwa kitendo chake cha kukiuka Sheria ya Ununuzi wa Umma."

Alipotakiwa na Kamati kuthibitisha ukweli wa tuhuma hiyo, Mheshimiwa John John Mnyika, alitoa maelezo yafuatayo:-

"...Vyombo mbalimbali vya Habari vimeandika kwa mfululizo, habari zinazoeleza tuhuma ya masuala ya ununuzi wa mafuta. Baadhi ya habari hizo zimenukuu Wabunge kwa majina yao... na mpaka naingia kusoma Hotuba Bungeni tarehe 27 Julai, hakukuwahi kuwa na kanusho la habari hizo." Haya ni maneno ya Mheshimiwa Mnyika.

Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola: Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola alipotakiwa na Kamati kuthibitisha ukweli wa tuhuma alizosisema Bungeni kwamba "... kuna watu wameanza kutumia Bunge kwa kudhani Wabunge tunakimbilia peremende na vipesa vyao ili kuhakikisha kwamba Serikali inatekeleza matakwa yao, na kwamba Nchi haitawaliki kwa kukosa umeme," maelezo yake yalikuwa kama ifuatavyo:-

Maneno ya Mheshimiwa Kangi Lugola yanasema: "...nilisema maneno hayo kutokana na uzalendo nillionao na kwa uchungu nillionao. Nilichangia Bungeni ili tu ku-pre-empty kama wapo watu waliojandaa kuwahonga Wabunge wajue kwamba sisi Wabunge hatuko tayari kutumika."

Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed: Katika kutaka kupata ushahidi kuhusiana na tuhuma hii ya rushwa, mahojiano ya Kamati na Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed yalikuwa kama ifuatavyo:-

Swali; "Mbali na hisia zako tu kwamba Wabunge hawa waliokuwa wanampinga Waziri, wanampinga Katibu Mkoo, kwamba lazima wamepewa chochote; je, una ushahidi mwingine zaidi ya huo?"

Mheshimiwa Keissy alijibu; ... "Huu ni ushahidi wa kukisia, mtu yeote mwenye akili timamu lazima atajua kuna chochote." (Kicheko)

Alipoitwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Prof. Sospeter M. Muhongo: Mahojiano kati ya Kamati na Waziri wa Nishati na Madini Prof. Sospeter M. Muhongo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Swali la Kamati: "Unaithibitishiaje Kamati hii kwamba madai hayo ya Makampuni ya MAFUTA kuwepo Dodoma na kugawa fedha kwa Wabunge?"

Jibu la Mheshimiwa Waziri: "...Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani naomba nikukumbushe kwamba, mambo yote ambayo mtakuwa mnayasikia kutoka kwangu na kutoka kwa wengine ambao mnahitaji kuwahoji yatakuwa ni allegations ..."

Narudia majibu ya Waziri: "Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani naomba nikukumbushe kwamba, mambo yote ambayo mtakuwa mnayasikia kutoka kwangu na kutoka kwa wengine ambao mnahitaji kuwahoji yatakuwa ni allegations ..."

Nukuu za Mahojiano hapo juu kati ya Kamati na mashahidi waliohojiwa zinaonesha wazi kwamba, hakuna ushahidi wowote uliotolewa kama uthibitisho wa tuhuma hii ya Makampuni ya Mafuta kuwapa rushwa Wabunge.

Tuhuma inayofuata: Tuhuma iliyotolewa na Waziri wa Nishati na Madini, Prof. Sospeter M. Muhongo, kwamba baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini wana mgongano wa kimaslahi (*Conflict of Interest*) kwa Kufanya Biashara na TANESCO.

Tuhuma hii ilitolewa na Waziri wa Nishati na Madini, Prof. Sospeter M. Muhongo, alipokuwa akihitimisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake Bungeni, kama ifuatavyo:-

"... tunao ushahidi usio na shaka wa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kufanya biashara na TANESCO... baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameingia Mkataba wa kuiuzia TANESCO matairi na kushinikiza kubadili bei ya matairi hayo baada ya mkataba kufungwa..." Mwisho wa nukuu iliyotolewa hapa Bungeni.

Tuhuma hii pia ilitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, katika barua aliyomwandikia Katibu wa Bunge, akitaja kwamba, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, pamoja na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, wanafanya biashara ya matairi na TANESCO. Waziri hakutaja jina lakini barua alioandika Ndugu Maswi ilitaja majina ya hawa ndugu. Aidha, tuhuma hii ilitolewa pia na Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, katika Mkutano na Waandishi wa Habari, kwa kumtaja Mheshimiwa Sara Msafiri Ally na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah kwamba, kwa taarifa alizonazo Wabunge hao walikuwa na mgongano wa kimaslahi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kibunge, kwa kuwa wanafanya biashara na TANESCO wakati wao ni Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, yenyе jukumu la kuvisimamia Wizara ya Nishati na Madini.

Katika Uchunguzi wa kupata ukweli kuhusu tuhuma hii, Kamati ilichambua nyaraka zilizowasilishwa kama vielelezo, pamoja na maelezo ya mashahidi waliohojiwa, ambapo Kamati ilibaini yafuatayo:-

Kampuni iliyoingia Mkataba na TANESCO kwa ajili ya kuiuzia TANESCO matairi inaitwa "Shariffs Services and General Supply Limited," ambayo kwa mujibu wa taarifa za Mamlaka ya Usajili wa Makampuni (BRELA), Mheshimiwa Sara Msafiri Ally na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, siyo wamiliki wala wanahisa wa Kampuni hiyo.

Hakuna mahali popote katika hatua za mchakato wa Zabuni ya Kuiuzia TANESCO matairi ambapo Wabunge waliothumiwa wamehusika.

Kitendo cha Mheshimiwa Sara Msafiri Ally kufuatilia kusainiwa kwa Mkataba ambao TANESCO ilikuwa imeupitisha, kuchukua nakala na kumpelekeea mhusika ambaye ni jirani yake, si uthibitisho wa kutosha kwamba, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally ndiye anayefanya biashara ya kuiuzia matairi TANESCO au kuwa yeche ndiye mmiliki wa Kampuni iliyoingia Mkataba wa kuiuzia matairi TANESCO.

Ukweli wa kauli iliyotolewa na Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Prof. Sospeter M. Muhongo Bungeni kwamba, baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini wana mgongano wa kimaslahi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kibunge kwa kufanya biashara ya kuiuzia matairi TANESCO haukuthibitishwa.

Madai ya Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu kuhusu Mheshimiwa Sara Msafiri Ally na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah kuwa na mgongano wa kimaslahi hayana ukweli pia, kwa sababu alipotakiwa na Kamati kuthibitisha ukweli kuhusu madai hayo, maelezo yake yalikuwa kama ifuatavyo:-

Maelezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu; "... ni kweli nilifanya huo Mkutano na Waandishi wa Habari, na ni kweli vilevile kwamba, nilitaja majina ya Mheshimiwa Sara Msafiri na Mheshimiwa Munde Tambwe, kama Wabunge ambao nilisema wana matatizo ya mgongano wa kimaslahi kama Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini. Niseme kifupi niliyatoa wapi hayo maneno. Siku moja au mbili kabla ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kuwasilishwa Bungeni, nilifanya vikao kadhaa na Waziri mwenyewe Mheshimiwa Prof. Muhongo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Masele na Katibu Mkuu, Bw. Maswi, katika Ofisi za Wizara hapa Dodoma, kwa ajili ya kufuatilia matatizo ya TANESCO na huo mgogoro wa tuhuma dhidi ya TANESCO. Kwa hiyo, niliyoyasema siku ya Press Conference yalitokana na taarifa ambayo niliipata kutoka kwa hao Waheshimiwa niliowataja." Maana yake Wizara.

Habari za kuambiwa (hear say), haziwezi kuchukuliwa kama ni ushahidi wa kuthibitisha madai au tukio fulani.

Ukweli wa tuhuma kwamba baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini wanafanya biashara ya kuiuzia TANESCO matairi ya magari na walihusika kutaka kubadilisha bei ya matairi hayo baada ya Mkataba kufungwa, haukuthibitika pia.

Waheshimiwa Wabunge, yafuatayo ni maelekezo ya Spika:-

Napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Brigedia Jeneral (Mst.) Hassan A. Ngwilizi (MB.), Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo, kwa umakini wao katika kuchunguza tuhuma zinazohusika na kuwasilisha Taarifa yao ya Uchunguzi na Ushauri kwangu.

Waheshimiwa Wabunge, tuhuma ya Wabunge kujihusisha na vitendo vya rushwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kibunge ni nzito na haiwezi kupuuzwa hata kidogo. Kwa kuzingatia uzito wa tuhuma yenyewe, ndiyo maana niliivunja Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, baada ya Bunge kuitisha Azimio la kufanya hivyo na kuagiza tuhuma hiyo ifanyiwe uchunguzi ili kubaini ukweli wake.

Kupokea rushwa ni kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria za Nchi na kwa vitendo nya jinai, Mbunge ye yote hana kinga na kama nilivyooleza hapo awali, Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296, imeweka bayana mambo yanayohusu haki za Bunge, yanayoweza kutiliwa nguvu na Bunge lenyewe ndani ya Bunge na yale ambayo yanapaswa kushughulikiwa na Mahakama.

Tuhuma hii ni kati ya mambo ambayo yana sura mbili kwa pamoja, yaani ni kosa la kijinai na ni jambo linalopaswa kushughulikiwa na Bunge lenyewe, ndani ya Bunge, kutokana na kuwa ni jambo linalohusu haki za Bunge.

Iwapo matokeo ya uchunguzi wa Kamati yangeonesha kuwepo kwa ushahidi kwamba tuhuma husika zimethibitishwa, ningepaswa kuwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kuchukua hatua zinazohusika, kwa mujibu wa Kifungu cha 12(4) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Suala hili limetupa somo na mfano mzuri wa mazoea yasiyofaa ya Wabunge wa Bunge hili kusema jambo lolote Bungeni bila kufanya utafiti wa kutosha wa kupata ukweli wa jambo lenyewe au taarifa kuhusu hilo analolisema, na hasa kama linahusu tuhuma kwa taasisi au mtu binafsi; na kwa sababu hiyo, kuna umuhimu wa Wabunge kujizua kusema mambo ambayo ni tetesi tu (*rumours*), na pia ni lazima Wabunge wajizue na tabia ya kutaka kusema tu kuhusu jambo lolote ili wasikike, bila ya kuwa na ukweli wa jambo lenyewe. Aidha, kwa mambo ya kibunge ambayo yamewekewa utaratibu na Kanuni za Bunge, ni vizuri Wabunge wayatekeleze kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Kanuni hizo za Bunge. Kwa mfano, kama Mbunge anahisiwa kuwa na tatizo la mgongano wa kimaslahi, Kanuni za Bunge zinaelekeza nini kifanyike. Mazoea ya kwenda kuvitangazia vyombo nya habari kuhusu suala kama hilo ni kinyume cha utaratibu uliowekwa na Kanuni za Bunge. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, lazima niseme wazi kwamba, vitendo vyovyote vinavyovunja haki za Bunge na pia kuathiri hadhi na heshima ya Bunge, kama vile rushwa na kadhalika, havitavumiliwa na Bunge hata kidogo. Vitendo kama hivyo vitakemewa na kuchukuliwa hatua zinazostahili mara vitakapothibitika. Sambamba na hilo, vitendo nya kulizushia Bunge tuhuma za uongo na kulizua Bunge au Kamati yoyote ya Bunge kutekeleza ipasavyo majukumu yake, havitavumiliwa hata kidogo, kwa sababu ni hatari kwa mustakabali wa Taifa letu. (Makofi)

Vitendo kama hivyo nya kuzusha tuhuma za kutunga zisizo na ukweli dhidi ya Bunge, si kwamba tu vinalifedhehesha na kulidhalilisha Bunge, bali pia vinalizua Bunge kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na vilevile vinawawekea kikwazo Wabunge wasitimize wajibu wao kwa Bunge, kwa wapiga kura wao, kwa wananchi kwa ujumla na pia kwa Taifa. (Makofi)

Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu ya Bunge, hususan kuisimamia na kuishauri Serikali, kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63(2) ya Katiba, utendaji wa Kamati za Bunge hautakiwi uwe ni wa kuingilia majukumu ya klutendaji ya Serikali, kwa sababu kwa kufanya hivyo, Kamati za Bunge nazo zinakuwa ni sehemu ya Serikali ambayo zinatakiwa ziisimamie na kuishauri. Kwa kuzingatia udhaifu uliojitekeza katika eneo hilo, kuanzia sasa, suala hili litafuatihi na kuratibiwa kwa karibu ili kuhakikisha kwamba kuna utekelezaji bora wa majukumu ya Kikatiba ya Bunge. Aidha, ni muhimu kwa nidhamu na mienendo (*conduct*) ya Wabunge kuwa katika kiwango (*standard*) cha Mbunge ambaye anatazamwa na jamii kama ni Kiongozi na mfano mzuri wa kuigwa.

Haitakiwi mwenendo na Maadili ya Kiongozi kama Mbunge kuwa na dosari au kutiliwa mashaka kutokana na matendo maovu yasiyotegemewa kufanywa na Kiogozi wa Umma. Ili

kusimamia ipasavyo nidhamu za Wabunge, Kanuni za Maadili (Code of Conduct) kwa Wabunge zimeandalika na zinategemewa kuitishwa hivi karibuni, ambapo masuala ya nidhamu kwa Wabunge yataratibiwa na kuchukuliwa hatua zinazostahili, kwa ajili ya kulinda hadhi na heshima ya Bunge na Wabunge. (Makofi)

Kwa kuzingatia kuwa matokeo ya uchunguzi wa Kamati yameonesha kwamba tuhuma husika hazikuweza kuthibitishwa; na kwa kuwa uzito wa tuhuma zenyewe umeathiri kwa kiasi kikubwa hadhi na heshima ya Bunge kama Taasisi, na pia hadhi na heshima ya Wabunge waliohusishwa; na kwa kuwa kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 25(c) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296, suala husika linahusu haki za Bunge na linapaswa kutolewa Uamuvi na Spika kwa mujibu wa utaratibu wa kibunge; sasa natoa Uamuvi wa Spika kama ifuatavyo:-

- (a) Uamuvi wa Spika: Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, amelifiedhehesha na kulidhalilisha Bunge kwa kuzusha tuhuma za uongo na kuufanya Umma wa Watanzania kuamini kwamba, baadhi ya Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini wanajihuisha na vitendo vya rushwa; na kwa kufanya hivyo, ametenda kosa la kuvunja haki za Bunge na anastahili adhabu. (Makofi)

Kwa kuwa baada ya kosa hilo kufanywa, uwepo wa uhusiano mzuri kati ya Bunge na Serikali, kwa maslahi ya Wananchi na Taifa kwa ujumla, ni jambo linalopaswa kupewa umuhimu wa kwanza. Uamuvi wa Spika ni kwamba, natoa onyo kali kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi na kumtaka asirudie tena kosa hilo la kuzua tuhuma za uongo dhidi ya Bunge na Wabunge. (Makofi)

- (b) Kwa kuwa Wabunge waliosema suala hili la rushwa Bungeni, walilisemea kwa nia njema ya kulikemea na hawakumtaja Mbunge ye yeyote kuhusika nalo; na kwa kuwa pamoja na nia hiyo njema, Wabunge hao walilisemea suala hilo bila ya kufanya utafiti kupata ukweli wake, Uamuvi wa Spika ni kwamba, Wabunge hao nawapa onyo kali na kuwataka wasirudie kosa hilo la kuzungumzia jambo Bungeni wasilokuwa na uhakika nalo. (Makofi)
- (c) Kwa kuwa Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu (MB.), alikuwa na fursa ya kulisemea suala la mgongano wa maslahi kwa Wabunge wahusika Bungeni, lakini aliamua kulisemea nje ya Bunge, kwa kutoa tuhuma dhidi ya Wabunge kuhusiana na suala hilo kwenye Vyombo vya Habari kwa kuwataja majina, kwa ushahidi wa habari za kuambiwa (*hear say*), kinyume na masharti ya Kanuni ya 61(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007; na kwa kuwa kwa kufanya hivyo aliwadhalilisha na kuwafedhehesha Wabunge hao; Uamuvi wa Spika ni kwamba, nampa onyo kali Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu na kumtaka asirudie kosa hilo la kuvunja Kanuni za Bunge na pia kuzungumzia jambo bila ya kuwa na uhakika nalo. Pamoja na onyo hilo, wale Wabunge waliotajwa na Mheshimiwa Tundu Lissu, nawaomba wamsamehe ili tuanze ukurasa mpya wa kupendana, kuheshimiana na kuvumiliana. (Makofi)
- (d) Kwa kuwa kauli ya Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo (MB.) kwamba, upo ushahidi usio na mashaka kwamba wapo baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini wanaofanya biashara ya kuiuzia matairi TANESCO na kwamba kwa

kufanya hivyo, wana mgongano wa kimaslahi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kibunge ya kuksimamia Serikali, aliitoa Bungeni, ambapo ukweli wake haukuweza kuthibitishwa; Uamuzi wa Spika ni kwamba, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Prof. Sospeter M. Muhongo (MB.), anatakiwa awe mwangalifu anapotoa kauli Bungeni, kwa sababu kauli za Mawaziri huchukuliwa kuwa ni Kauli za Serikali. Hivyo, anapotoa kauli yoyote Bungeni, ahakikishe kuwa ana uhakika wa ukweli wa jambo analolisema. (Makofi)

Uamuzi huu nimeutoa Bungeni, Dodoma leo tarehe 9 Novemba, 2012.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda kuwa mfupi, tunaendelea na shughuli zinazofuata.

#### **HOJA BINAFSI ZA WABUNGE**

#### **Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto Kuhusu Kuitaka Serikali Kuchukua Hatua Dhidi ya Watanzania Walioficha Fedha Haramu Nje ya Nchi**

(Majadiliano yanaendelea)

#### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kuwa ninaunga mkono hoja hii. Hoja hii ni muhimu. Umuhimu wa hoja hii umejikita kwenye ukweli kwamba inahusika na suala la ujisadi ambao kihistoria umekuwa ni chanzo cha upotevu wa mabilioni ya fedha za umma, jambo ambalo mara nyingi husababisha maendeleo ya nchi ama kukwama/kucheleweshwa. Hoja hii ni muhimu kama ilivyokuwa hoja ya Richmond katika Bunge liliopita.

Mheshimiwa Spika, nimesoma pia maelezo ya hoja iliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Werema. Lengo la hoja ya Mheshimiwa Werema ni kufanya mabadiliko katika hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto. Mheshimiwa Werema anapendekeza kwamba Azimio la 1, 2, 3, 4, na 7 katika hoja ya Mheshimiwa Zitto yafutwe/yaondolewe na anafanya mabadiliko ya maneno katika Azimio la 5 na la 6.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Werema anapendekeza kuviachia vyombo na mamlaka ya uchunguzi vya Serikali vifanye ufuatiliaji wa fedha iliyofichwa Uswisi badala ya Kamati Teule ya Bunge kama Mheshimiwa Zitto Kabwe anavyopendekeza.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi sikubaliani na pendekoz hilo la Mheshimiwa Werema sababu kubwa ni kwamba vyombo vya mamlaka ya uchunguzi vya Serikali peke yake mara nyingi hukabiliwa na tatizo la kigugumizi katika kuchunguza watu wakubwa Serikalini au katika Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, iwapo sisi Wabunge tuna nia ya dhati katika mapambano yetu dhidi ya rushwa/ufisadi, inafaa Bunge lichukue hatamu katika suala la ujisadi/rushwa kwa kuwa Serikali imeonyesha udhaifu mkubwa katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, uamuzi sahihi na wenyе maslahi kwa Taifa letu ni kwa Wabunge wote kuikubali hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto. Utakuwa ni uamuzi wa kihistoria katika vita dhidi ya rushwa/ufisadi katika eneo lengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, napendekeza uchunguzi ufanyike katika mfumo wa manunuzi yote (*tendering process*) katika zabuni zote kubwa nchini zilivyopatikana na nani walikuwa wahusika zaidi. Thamani ya tenda na kazi ilivyofanyika ili kubaini wizi na thamani ya fedha iliyotumika, hususan tenda za ununuzi wa mafuta, tenda za barabara nchini pamoja na ujenzi, tenda za ununuzi wa Rada. Kufungua upya mijadala yote iliyofungwa ya Meremeta, Tangold, Richmond, Dowans/IPTL na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, udhaifu wa Serikali katika kupata taarifa, unatokana na nini? Inawezekanaje watu binafsi wakawa na taarifa juu ya wizi huo wa fedha ilihali tuna Kitengo cha Usalama wa Taifa (*TISS*)? Nini ni kazi za usalama wa Taifa nchini?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na taarifa mbalimbali za viongozi wa juu Serikalini kutamka hadharani kuwa wanawafahamu wale wote wanaohusika na rushwa kubwa pamoja na mafisadi wakiwemo:-

- (i) Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Kuna wakati aliwataka wote walioiba fedha za Kagoda pale Benki Kuu warudishe na atawasamehe na taarifa za ziada zinasema wapo waliorudisha. Je, ni akina nani na fedha hizo zilitunzwa katika akaunti zipi?
- (ii) Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU aliwahi kusema anawafahamu mafisadi wote nchini.
- (iii) Waziri Mkuu (Mheshimiwa Mizengo Pinda) naye aliwahi kukiri hivyo Bungeni juu ya mafisadi na wala rushwa wakiwemo waliokuwa Mawaziri wa Fedha wa zamani walio na kesi Mahakamani sasa. Fedha wanazotuhumiwa zinatunzwa wapi?
- (iv) Mfanyabiashara mashuhuri Mzee Reginald Mengi alishawahi kuwataja mafisadi papa. Ipi ni hatua ambayo Serikali ilichukua?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Andrew Chenge (wakati akiwa Waziri wa Miundombinu) alipata kutuhumiwa kuwa na fedha nje ya nchi Dola milioni 1.2 katika kisiwa cha New Jersey ambapo alisikika akisema kuwa vile ni vijisenti.

Mheshimiwa Spika, kashfa ya Richmond ambayo ilimwondoa madarakani aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa tuhuma za kampuni kujilipa shillingi milioni 152 kwa siku kwa miaka miwili mfululizo; fedha hizo zilikuwa zinapelekwa au kuhifadhiwa katika akaunti gani?

Mheshimiwa Spika, hivyo basi tunaomba Serikali ikubaliane na hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto ili Tume iundwe kwa ajili ya uchunguzi wa fedha zote haramu zilizo nje ya nchi zirudishwe nchini.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja kuhusu kuitaka Serikali kuchukua hatua dhidi ya Watanzania walioficha fedha haramu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Tanzania, Sura ya Pili imeweka malengo muhimu na misingi ya mwelekeo wa shughuli za Serikali kwamba wananchi ndiyo msingi wa mamlaka ya Serikali, wajibu wa Serikali ni ustawi wa wananchi na Serikali itawajibika kwa wananchi; na kwamba mamlaka ya nchi na vyombo vyake vitawajibika kuhakikisha sheria za nchi zinalindwa na kwamba aina zote za dhuluma na rushwa zinadhibitiwa; na kwamba shughuli za uchumi haziendeshwi kwa njia zinazoweza kusababisha ulimbikizaji wa mali au njia kuu za uchumi katika mamlaka ya watu wachache binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo ya Kikatiba, Serikali inapaswa kutumia njia zote za kisheria za kitaifa na kimaitaifa kuhakikisha kwamba fedha zilizofichwa nje ya nchi Usvis na nchi nyilgine duniani zinarejeshwa na waliohusika na utoroshaji huo wanachukuliwa hatua za kisheria. Aidha, waliohusika na utoroshaji huo ambao wamehusika pia na ujisadi na matumizi mabaya ya madaraka wanachukuliwa hatua kali zaidi ikiwemo kufikishwa Mahakamani na wakikutwa na hatia mali zao kufilisiwa. Wakati kesi zao zinaendelea, mali zao zishikiliwe kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Haramu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuungana na maelezo, mapendekezo na maazimio ya mtoa hoja, yafuatayo yazingatiwe na Serikali, Wabunge na Bunge:-

- (i) Ichunguze akaunti za nje zilizokuwa chini ya aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu, Marehemu Daud Balali kutokana na mwaka 1998 kutuhumiwa kupewa hongo ya dola za Marekani milioni tano na kampuni ya Skanska Jensen ya Sweden.
- (ii) Wote waliohusika na kuidhinisha, kumruhusu au kunyaamazia malipo ya dola za Marekani 118,396,460 na kupelekwa katika akaunti moja ya Benki ya NedBank Limited ya Afrika Kusini, wachunguzwe na akaunti hiyo pamoja na akaunti za wahusika za ndani na nje zichunguzwe. Katika kufanya uchunguzi huo, Serikali irejee michango na maswali yangu Bungeni kuhusu ujisadi wa Meremeta, Deep Green na Tangold. Wafuatao wachunguzwe; aliyekuwa Waziri Nazir Karamagi, aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Gray Mgonja na aliyekuwa Mwanasheria Mkuu Andrew Chenge. Pamoja na akaunti ya Afrika Kusini, akaunti zilizopo Mauritius nazo zichunguzwe.
- (iii) Uchambuzi ufanyike kuhusu taarifa za uchunguzi wa mikataba yote ya madini za nyakati mbalimbali pamoja na taarifa za mapitio ya mikataba ya gesi asili inayoendelea.
- (iv) Ukaguzi ufanyike pia katika utoaji wa leseni za utafutaji wa mafuta. Makampuni yaliyoingia mikataba yenye mashaka na wahusika walioingia mikataba hiyo kujulikana. Benki Kuu na Sekretarieti ya Maadili ya Umma itoe taarifa, akaunti zao zichunguzwe.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja kuhusu Serikali kuchukua hatua kwa walioficha fedha haramu nje.

Mheshimiwa Spika, napeda kuchukua fursa hii kumpongeza Mtoa Hoja kwa hoja ambayo siyo tu ina kusudio la kurudisha fedha za Watanzania, ila pia kurudisha nidhamu kwa wanaopewa dhamana ya kuongoza nchi hii yenye rasilimali nyingi lakini watu wake ni maskini na wapo wasiojua kesho yao.

Mheshimiwa Spika, yawezekana jambo hili likaonekana kama ni uchochezi na uchonganishi na wapo wanaodhani ni harakati za mbio za Uraisi, sitokubaliana na mawazo hayo kwa kuwa sio tu mto hoja ni mzalendo na mtu maskini bali pia anatoka kwenye chama makini chenye nia thabiti ya kumsaidia Mtanzania mnyonge.

Mheshimiwa Spika, hali ya Watanzania inazidi kuwa mbaya siku hadi siku. Matabaka yameongezeka na chuki baina ya Watanzania inaongezeka. Yote haya ni matokeo ya ujisadi ambao umepigwa kelele tu za mdomo bila hatua madhubuti ya kukomesha ujisadi, ndiyo maana leo tunajadili haya. Kama hatua za kukomesha ujisadi zingechukuliwa toka mwanzo leo hapa tusingekuwa na mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nina ujumbe wa simu ninazopigiwa na ninaowawakilisha, tunaunga mkono hoja na mapendekezo yote ambayo mto hoja amependekeza iwe.

Mheshimiwa Spika, ujisadi ni kansa ya Taifa na kwa kasi kansa inasambaa, bado mgongwa (Serikali) anao uamuzi wa kiungo gani chenye ugonjwa kiondolewe, kama mgongwa (Serikali) haitokuwa tayari kuridhia basi maamuzi hayatakuwa ya mgongwa tena bali familia ya mgongwa (wananchi) wataamua nini kifanyike.

Mheshimiwa Spika, nategemea kwa faida ya nchi na wananchi leo mtaweza kabisa kubaliana na hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe na mapendekezo yake bila kujali itikadi zetu, tutaridhia na utekelezaji wa mapendekezo utafanyika mara moja.

Naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya kuitaka Serikali kuchukua hatua dhidi ya Watanzania walioficha fedha haramu nje ya nchi ya Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto (Mb).

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa masikitiko makubwa kushindwa kuamini hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto (Mb) ambayo ameinisha mfumo mzima uliotumika kutorosha fedha za walipa kodi wa Tanzania wenge matatizo makubwa ya kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kama Mbunge binafsi ameweza kupata taarifa hizi nzito kwa njia zake mwenyewe, taarifa ambazo zimetushangaza, nashawishika kukubali kuwa Tume Teule iundwe kupata ukweli kwa njia zilizo halali ili fedha hizi za Watanzania wenge kero mbalimbali za kujiletea maendeleo ziweze kurudishwa kuja kufanya kazi ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo mfano kujenga maabara, kununua madawati, nyumba za Walimu, madarasa, madawa, kujenga zahanati na kadhalika. Vilevile, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao kwani huu siyo utawala bora na ni tabia ya kutokuwathamini wengine.

Mheshimiwa Spika, sioni sababu ya Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto (Mb) kushindwa kutaja majina ya viongozi, watendaji wakuu na wafanyabiashara waliohusika kutorosha fedha na kwenda kuficha nchi za nje kwani Bunge ni mhimili unaojitegemea na unaendeshwa kisheria. Hii itakuwa ni fundisho kwa Watanzania wengine ambao wangeweza kushawishika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu. Ili kuondokana na mlolongo mrefu wa utekelezaji, ni vema atoe vielelezo vyote na kumkabidhi Mheshimiwa Spika ili Bunge liweze kutoa uamuzi wenge maslahi mapana na Serikali yetu na vilevile kupunguza gharama. Kwa ujumla

Mheshimiwa Zitto (Mb) ameonyesha uzalendo wa hali ya juu. Vilevile ninashauri account hizo zilizoko nchi za nje zifungwe mpaka ufumbuzi wake wa kuzirudisha ukamiliike kwani wanaweza wakaziondoa kwa njia wanazoju wenye. Ubinafsi huu lazima upate tiba ili uchumi wa nchi hii uweze kuwanufaisha Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, mambo yenye maslahi ya jamii nzima ya Watanzania ni vyema itikadi zetu tuziweke pembeni, utaifa uwe mbele.

Mheshimiwa Spika, naomba mchango wangu upokelewe na mawazo yangu yachukuliwe.

**SPIKA:** Mtoa hoja, Mheshimiwa Kabwe Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja ambayo niliwasilisha jana, kuhusiana na Watanzania ambao wana fedha katika akaunti mbalimbali za nje. Kwanza, ninapenda kuwatambua wachangiaji waliochangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Waliochangia kwa kuzungumza ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Mheshimiwa Ali Keissy Mohamed, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Luhaga Mpina.

Waliochangia kwa Maandishi ni Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Pofesa Kanalwanda Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Vincent Nyerere na Mheshimiwa David Silinde.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamezungumza masuala mengi sana, ambayo yote yana maana kubwa sana na ningependa Bunge liyazingatie tunapoangalia suala hili la kuhakikisha Watanzania ambao wameficha fedha nje, wanachukuliwa hatua zinazostahili na vilevile tuhakikishe tunaziba hiyo mianya.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina mianya mingi sana ya utoroshaji wa fedha, narudia, nchi yetu ina mianya mingi sana. Hivi sasa tayari kuna baadhi ya Mabenki Duniani ambayo yanataka kuitumia Tanzania nayo kama offshore vilevile kutokana na mianya ambayo ipo. Ningependa kunukuu taarifa moja ya Gazeti la Q Bytes ambalo linatoka Marekani, ambalo linazungumzia namna ambavyo watu wa Mataifa mengine pia wanaweza kuficha fedha zao Tanzania na wala wasipate shida yoyote. Ninaomba kunukuu:-

*"There's one country I know of, however, that is really off the radar when it comes to offshore banking. You can open multi-currency bank accounts here, and get full internet banking, including of course the chance to send multi-currency international bank wires online. US citizens are very welcome. And everything can be set up by mail, with no need to travel there."*

*This country, I should warn you, is in Africa. Some people lose interest right there, but I think that is a mistake. This is actually an important gold producing nation, so not surprisingly, it's doing well at the moment. If you think gold will keep going up in dollar terms (I do) then this country will continue to prosper. The bank I recommend there, to consulting clients, is actually based in Europe and owns a gold refinery. The country I'm talking about is Tanzania."*

*This is a US Magazine ambayo kazi yake ni kuhamasisha matajiri kuweza kuficha fedha zao kwenye nchi ambazo zina mianya ya utoroshaji. Tayari kutokana na namna ambavyo nchi*

yetu ina mianya mingi, zinapokuwa nchi nyingine zinaondokana na hiyo sifa ya usiri na kadhalika na urahisi wa kutuma hizo fedha, sasa watu wanaanza kuifkiria Tanzania kama eneo ambalo wanaweza kuja kuficha fedha na kuzipeleka nje watakavyo; kama mlivyoona mtu anaweza akatuma tu kutoka kwenye bank account akapeleka kokote anakotaka kwa njia za internet na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii inaonesha hivi ndivyo ambavyo Mataifa mengine yanatuona. Hivi ndivyo ambavyo nchi yetu sasa inaonekana kuwa ni nchi ambayo pia inaweza kutumika kuweza kuficha mabilioni ya fedha, licha ya kwamba nchi yetu inapeleka nje fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wametoa hoja nyingi sana na ninakubaliana nao kabisa na Wabunge wame-demand sana kwamba kwa nini tusitaje majina? Kwa nini Zitto asitaje majina? Kwa nini Mheshimiwa Membe ambaye aliwahi kusikika kuwa anayafahamu majina asiyataje?

Mheshimiwa Spika, inawezekana tukawa na hamu sana ya kusikia hayo majina; swali la msingi la kuijiliza mkishayasikia mnafanya nini? Ni mara ngapi majina yametajwa na hakuna kilichofanyika?

Tanzania; na hili Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ninaomba tulitilie maanani sana, siasa zetu zimekuwa za ku-trivialize vitu. Kwa hiyo, tunajikuta sisi kila wakati ni watu wa kuzungumza mambo yale yale. Mtu yeoyote makini anapaswa kuangalia ni namna gani atahakikisha mambo ambayo tunayazungumza sasa, miaka mitano, kumi, ishirini ijayo, yasiwepo tena.

Mheshimiwa Spika, kuna mashinikizo na juzi, Mzee John Malecela akiwa Uingereza alinitumia Kitabu kwa DHL, kinaitwa *Tressure Highlands, Tax Havens and the Men Who Stole the World*. Kinaelezea mfumo mzima wa namna ambavyo watu wanatorosha fedha. Akaniambia mwanangu nimeona hiki Kitabu nikiwa *Airport* na ninajua una hoja yako, ninaomba ukisome kikusaidie.

Mheshimiwa Spika, one quote kwenye kitabu hicho, *not really a quote, just a story*, kuna Mbunge mmoja anaitwa Fabian Albertin wa Ufaransa wa kutoka Chama cha Socialist, mwaka 1932, debate ambayo tunayo leo, Bunge la Ufaransa lilikuwa na debate kama hiyo. Wabunge wakawa wanamlazimisha huyu Mbunge Fabian kwamba, ‘wataje’ kama tulivyokuwa tunalazimishwa jana mimi na Mheshimiwa Membe, huyo Mbunge akasema mamlaka zifanye kazi. Wakati kelele zile zinaendelea Bungeni, Jeshi la Polisi la Ufaransa likavamia Commercial Banks zote pale Paris kuangalia transfer ya fedha kati ya Paris na Geneva, wakakuta watu wengi sana wa Ufaransa, wengine walikuwa Maseneta, wengine walikuwa miongoni mwa hao Wabunge ambaeo walikuwa wanamwambia Fabian, ‘wataje’. Kwa hiyo, mimi sitaki turudi katika Ufaransa ya mwaka 1932. Ninachokitaka, tuweke mazingira ambayo tutahakikisha mambo haya hayatokel, milanya iliyopo kwenye nchi yetu ni mingi sana.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba hatuna majina, tuna majina. Hapa kuna majina kumi na tatu ya watu wenye fedha lakini watu ambaeo wana fedha nje ni zaidi ya 200. Ukitaja leo majina 13, ndio stori imekufa, wala hakuna kazi ya ziada ambayo itakuwa imefanyika. Ndiyo maana tumeomba kwamba tuunde Kamati Teule wale ambaeo tumeshafanyakazi na tuna baadhi ya nyaraka na vitu mbalimbali tuvipeleke kule kwenye Kamati Teule, Kamati Teule ipanue wigo wa uchunguzi, tuletewe taarifa hapa imekamilika, taarifa ambayo haina mashaka. Kama mnataka tu *headlines* za kesho, watu wanaweza waka-provide *headlines* za kesho, then what next baada ya hizo *headlines*?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima tuwe responsible na mimi ningependa kusema tu, nitaandikwa mara moja, mara mbili, nitapata sifa, lakini nitakuwa nimeisadia nchi? Hapana! Sitakuwa nimeisadia nchi. Mimi lengo langu ninataka tuisaidie nchi iondokane na tatizo la fedha haramu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hizi fedha haramu mabilioni ambayo yanatunzwa na watu wachache nje, yatakuja kuwa-cost ninyi tu, si mnaenda kwenye uchaguzi? Yatawa-cost ninyi tu msipochukua hatua, wala msidhani kwamba yataenda kumgharimu mwananchi wa Kalinzi kule au Mtama kule au Masama kule Hai au Singida Mashariki kwa rafiki yangu hapa, itatu-cost sisi, mtakavyoona jinsi ambavyo fedha zitamwaga kwenye Majimbo yenu, fedha zitamwaga kwenye vyama vyetu, kuweza kuhakikisha kwamba wana-take control. Kuna watu wanasema kwamba *with 20 million dollars* Tanzania unaichukua, tunataka tuidhibiti hiyo isiwe na ndiyo maana nataka tuzibe hii mianya.

Mheshimiwa Spika, kuna njia mbili ambazo tunaweza tukafanya, wenzetu wa Kenya na Senegal wao wameajiri *Private Investigator* ambae amechambua na kuweza kupata complete list ya watu na fedha zao na wameipelekea Serikali yao na hiyo Serikali imesema hawa ni fedha halali, hawa siyo halali, hawa tunawachukulia hatua. Senegal huyu Rais Macky Sall ameingia juzi tu hatua ya kwanza aliyoifanya ni hiyo. Kenya wenzetu taarifa ilivyotoka tu mara moja waka-engage *Private Investigator*. Kwa hiyo, tunaweza tukaamua sisi kama nchi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali tukatafuta, tukatangaza kama ni tenda, mtafanya utaratibu wenyewe mnaoujua wa *Public Procurement*, tukapata a *Private Investigator* tukampa kazi kwa sababu suala siyo Switzerland peke yake, kuna maeneo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hili na Mheshimiwa Chenge anajua kwamba mimi ninamheshimu sana, Mheshimiwa Chenge yeeye alikiri, alikubali kwamba ana hela Jersey, wala hii siyo siri. Lakini sijui kama mamlaka zilimwuuliza kwamba kwenye fomu yako ya maadili ultangaza kwamba una hii akaunti, una hizi pesa? Sijui, hatujapewa taarifa. Sijui mamlaka kama TRA ali-declare, kwa sababu inatakiwa kila Mtanzania mwenye akaunti nje a-declare kila mwaka TRA kwa sababu za kikodi, kwa sababu ni resident hapa, anapita kwenye barabara za hapa, anapata huduma za hapa, kwa hiyo ni lazima alipe kodi za hapa. Mimi sijui kama Mbunge mwenzangu hayo yalifanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini ninyi mnafahamu kwamba aliyejikuwa deal maker wa radar Tonhil Somaishi Switzerland. Jana Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasema kwamba inabidi mseme kashfa gani, mtu gani...

**MBUNGE FULANI:** Ni Shailesh Vithlani!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** I am sorry, ni Shailesh Vithlani, ainaishi Switzerland, ana akaunti Switzerland, ana-transfer money from Switzerland. Sasa sijui kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali hata kwa huyu tu kama mlifanya hivyo na kuweza kupata na kumhitaji kurejesha fedha. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo lazima tuyaangalie kwa mapana yake na ndiyo maana nimeombwa hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna mambo mawili, twende na uamuzi wa *Parliamentary Investigation* ambao tutaipa mamlaka Kamati na hadidu za rejea na kadhalika tuweze kwenda kuchambua au twende na maamuzi very specific ya kuitaka Serikali siyo tu i-engage *Private Investigators* lakini pili, Serikali inaweza ikashirikiana sasa na taasisi za kimataifa kwa sababu tayari kuna taasisi za Kimataifa ambazo zinasaidia nchi zinazoendelea kwenye masuala kama

haya. Huu ni uamuvi wetu sisi, mimi kazi niliyoifanya ni kutimiza wajibu wangu kama Mbunge na nimefikia *limit* siwezi tena zaidi ya hapo. Kwa hiyo, ni Bunge kunisaidia na Executive kuweza kusaidia, ili tuweze kwenda *the way forward*.

Mheshimiwa Spika, jana nimeona mijadala ya Bunge. Njia nyingine ni kushauriana na marafiki zetu. Hili napenda nilizungumze vizuri sana, misaada tunayoipata kutoka nje (*foreign aid*), ni moja ya kumi tu ya fedha ambazo zinaibwa kutoka Tanzania, zinotoroshwa kupelekwa nje. Misaada hii tunapewa kwa masharti, tunaminywa, tunaambiwa tufuate yale ambayo wanayataka wao, ni lazima tuwe maskini jeuri. Nchi hizi ambazo zinatupa misaada tuziambie kwamba tusaidieni sasa tuondokane na huu utoroshaji ili tuachane na misaada. Kwa mfano, Ufaransa wana CDs *globally* za watu wote duniani.

#### **MBUNGE FULANI:** Wataje, aache stori!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Serikali yetu inaweza ikatumia mahusiano yake na Ufaransa, inaweza ikatumia mahusiano yake na Marekani, inaweza ikatumia mahusiano yake na Ujerumanu, kwa ajili ya kuweza kupata hivyo vitu. Ukienda *route* ya *Private Investigator* ni lazima mlipe, mkienda *route* na nchi zingine mnawenza mkajikuta kwamba mnapata hizo taarifa bila kuingia gharama zozote. Kwa hiyo, ni lazima tuhakikisha kwamba kwa pamoja tunashirikiana ili kufanikisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo ambalo ningependa kulisisitiza na ndiyo nadhani jambo langu la mwisho katika orodha yangu, *last but one*, jana nimeangalia michango ya Wabunge na nimesema kwamba nawapongeza sana Wabunge kwa michango mizuri sana. Ninawaomba sana na hasa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwamba jambo hili msilijadili *with a background* ya uchaguzi wenu, jambo hili mljadili kama Watanzania, mkishaweka makambi yenu hamtapata ukweli. Muwe above makambi yenu, msiangalie Tanzania ya 2015, iangalieni Tanzania ya miaka ya mbele inayokuja, tutapata ukweli na tutalitatua hili tatizo moja kwa moja. Huo ni ushauri wangu kwenu ninyi mlio wengi na Mheshimiwa Tundu Lissu jana amewaambia hapa kwamba *you have the responsibility*. Ninyi ndiyo wengi, mkiamua kupiga chini mambo haya yatapigwa chini, lakini historia itawahukumu. Mkiamua tufanye kazi kwa pamoja itakuwa kama jana kwamba *by partnership* tumekwenda tumeppata jambo zuri ambalo litaweza kusaidia nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, kuna baadhi ya vitu ambavyo ningependa kupendekeza zaidi vinatokana na ushauri ambaa nimeupata jana. Moja, Serikali yetu ianzee mazungumzo na Serikali za nchi ambazo fedha nyingi zinotoroshwa kwenda na mfano hapa ni Switzerland kwa ajili ya kuwa na *Tax Information Exchange Treaty*, ili kuwa na urahisi wa kuweza kupata taarifa. Baadhi ya nchi sasa zina-negotiate na nchi ya Switzerland kuwa na hiyo *Information Exchange Treaty*. Jambo la pili, tatizo ambalo tunalo ni la watu kuwa na akaunti bila ku-declare kwenye mamlaka za hapa ndani. Kwa hiyo, katika baadhi ya mapendekezo ambayo inabidi tuyaangalie ni pamoja na kuhakikisha kwamba raia yejote wa Tanzania hata kama ni lazima awe na akaunti nje lakini ni lazima hiyo akaunti iwe declared na hasa na TRA kwa sababu sehemu kubwa ya mapato haya yanatumika kwa ajili ya kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, tatu, jana niliwaambia kwamba Benki ya UBS ina *Customer Relationship Managers* 240 kwa ajili ya Tanzania peke yake na hawa watu wanakuja, wana-attend customers wao, wanaondoka. Hawa watu wanawasiliana kwa simu na customers wao na taarifa hizi zinaweza zikapatikana kwa kuangalia flow ya simu kati ya Tanzania na Switzerland, TCRA inaweza ikaifanya kazi hii vizuri sana, kama kutakuwa na demand ya kufanya hivyo na kama tukitaka kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ninachokipendekeza na ninachokiomba ni kwamba benki yoyote au taasisi yoyote ya Kifedha isiruhusiwe kuhudumia wateja wake bila kibali cha Benki Kuu ya Tanzania, kwa sababu wanachokifanya *UBS* wanawahudumia wateja wao hapa wakati hawana kibali cha Benki Kuu na sheria zetu haziwalazimishi wawe na kibali cha Benki Kuu. Kwa hiyo, any *Financial Advisor*, any bank, any *Financial Institution* ya nje yenye mteja Tanzania lazima tuiweke kwenye sheria iwe inapata kibali cha Benki Kuu, mkishafanya hivyo habari zote tutazipata na tutaweza kujua fedha zinazoibwa na kuziuia na fedha ambazo zinotoroshwa. Baadhi ya nchi zingine wamefanya hizo *measures*, wametoa *grace period* ya watu kutangaza na kurejesha na kadhalika, sisi tutaangalia ni namna gani ambavyo tunataka kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninapenda nishukuru sana kwa michango mbalimbali ya Wabunge, naomba sasa Bunge lako Tukufu, lipitie maazimio ambayo jana nimeyapendekeza katika Bunge hili ili tuweze sote kwa pamoja kupambana dhidi ya utoroshaji wa fedha haramu za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja *Ilitolewa iamuliwe*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nimeisikiliza michango ya Wabunge na hasa Mheshimiwa Kabwe Zitto kuhusu hoja hii. Hii ni hoja ambayo ina msisimko Lakini kitambo tu ultoa hukumu yako kwenye Bunge hili Tukufu, katika hukumu ile umezungumzia kitu ambacho Wabunge tunapaswa kukifkiria na kutafakari, nacho ni mamlaka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya, watu wengi hawapendi kuambiwa hawana mamlaka, wapo Majaji, wapo Wabunge na wapo Viongozi wengine katika mhimili wa Serikali, kuambiwa hawana mamlaka wanakasirika. Mamlaka ya Bunge yanatokana na Ibara ya 63 ya Katiba ya nchi yetu, Ibara ndogo ya 2 na Ibara ndogo ya 3. Katika kuishauri na kuisimamia Serikali, Bunge linafanya nini.

Mheshimiwa Spika, jana nilitoa taarifa kwamba nilikuwa natarajia kuyafanyia marekebisho mapendekezo ya rafiki yangu Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini. Sitofautiani naye lakini nachelea kusema kwamba tufanye vitu ambavyo Katiba inatupa mamlaka, tusije tukafanya kitu kwa sababu tunataka kuchukua mamlaka ya vyombo vingine.

Mheshimiwa Spika, jana nilizungumzia sheria na rafiki yangu, pacha wangu upande ule wa pili Mheshimiwa Tundu Lissu alisema kwamba nimetaja uititiri wa sheria, nilifanya hivyo ili kuonesha kwamba hakuna ombwe. Neno ombwe kwa Kiswahili ni zuri sana Waingereza hawana neno zuri, wanasema *vacuum* lakini siyo *vacuum* ndiyo maana walikopa neno la kilatini linaloitwa '*Casus Omissus*', yaani ombwe kwamba hiki kitu hakina mwenyewe. Kwa hiyo, zile sheria nilizotaja zilikuwa zinatoa mwelekeo kuonesha kitu kimoja kwamba jambo hili la wizi maana yake tunazungumzia watu wanaoficha, uvunjaji wa sheria ni jambo la jinai na kuna utaratibu wake.

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto ni kwamba tutumie sheria lakini vilevile tutumie njia nyingine zaidi ya sheria. Nikisema hivyo, nafikiri wengi mtaunga mkono njia hizo ambazo ni zaidi ya sheria siyo kunyonga watu wala kuwatesa, isipokuwa ni kutumia njia za diplomasia na *covert action*. Wale wanayoyajua haya, nafikiri Mheshimiwa Zitto

naye ameyasema na jana Dada yangu Profesa Tibajuka aliniambia kwamba kutumia sheria peke yake hatuwezi kupata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuzingatia hiyo, nilikuwa naomba kufanya marekebisho ili tupate muafaka, tuondoche hapa tukiwa wamoja kama tulivoambiwa na inawezekana kwa sababu Bunge hili ni Bunge la sheria, Bunge la Katiba, ni Bunge la Kanuni, ni Bunge la Miongozo na vitu kama hivyo, kwa hiyo, tukifanya hilo tutakuwa hatujavunja sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, ukiona pendekezo la Mheshimiwa Zitto ukurasa wa tisa, pendekezo la kwanza, nilikuwa naomba lile pendekezo tuliondoe lisiwepo kwenye mapendekezo haya kwa sababu vyombo na mamlaka za uchunguzi nchini zinalishughulikia jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa AG, naomba urudie sikusikia vizuri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, narudia. Ninapendekeza kwamba pendekezo la kwanza la Mheshimiwa Zitto Kabwe linalosema kwamba Serikali iwasiliane na Benki ya Dunia ili kupitia kitengo cha *Assets Recovery Unit* ili mabilioni ya fedha yanayomilikiwa na Watanzania katika mabenki ya nchini Switzerland na Visiwa na maeneo mengine yote ambapo hufichwa fedha hizo ili kukwepa kodi yarudishwe nchini mara moja. Ninachopendekeza ni kwamba jambo hili tayari linafanywa na vyombo vyetu vya uchunguzi na nikisema hivyo ni pamoja na mimi mwenyewe. Jana nimemsikia Mheshimiwa Lugola anasema yeze ni Mpelelezi, mimi ninawaelekeza Wapelelezi.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili kwamba Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni ifikapo Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge kwamba itakuwa ni marufuku kwa kiongozi yeoyote wa umma au mume au mke wake au watoto wake kuwa na akaunti katika mabenki nje ya nchi. Ninapendekeza pendekezo hilo liondolewe kwa sababu linashughulikiwa na Kifungu cha 6 cha Sheria ya Fedha za Kigeni (*Foreign Exchange Act*) pamoja na Kanuni zinazojitosheleza katika eneo hilo kwa mujibu wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tatu, napendekeza pia liondolewe kwa sababu, mnaweza kulisoma Waheshimiwa Wabunge, linasema kwamba katika Muswada tajwa huo ambao tumeuondo, Governor wa Benki Kuu ya Tanzania aimarishiwe mamlaka ya kutoa kibali kwa Mtanzania yeoyote anayetaka kufungua akaunti ya benki nje ya nchi na kwamba kila mwaka Governor atatangaza kwenye Gazeti la Serikali na magazeti yanayosomwa na wananchi wengi, orodha ya Watanzania walioomba na walioruhusiwa kuwa na akaunti ya benki nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza pendekezo hilo liondolewe kwa sababu linavunja msingi wa usiri wa mabenki, *the best banking practices* wa wateja wao. Watuhumiwa wa uhalifu watashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria zinazoinisha makosa watakayotuhumiwa nayo. Aidha, ukiukwaji wa Kifungu cha 7 cha Sheria ya *Foreign Exchange Act*, taarifa hutolewa kama kuna amri ya Mahakama. Kwa hiyo, kama tutapata amri ya Mahakama taarifa hizo tutazipata. Tufahamu Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili lilitunga Sheria ya kuweka adhabu kwa mtu anayetoa siri zinazotokana na kujua akaunti za watu wengine, adhabu yake ni shilingi zisizopungua milioni tano (5) au kifungo kisichozi miaka miwili (2) au adhabu zote mbili.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la nne kwamba Watanzania wote wenyе akaunti za fedha nje waeleze wamezipataje na TAKUKURU wachukue hatua za kisheria dhidi ya watu wote wenyе kumiliki fedha na mali kinyume na mapato yao halali. Ninapendekeza pendekezo hili liondolewe kwa sababu hii ndio kazi ya TAKUKURU, hiyo ndio kazi ya *Financial Intelligence Unit* na ndio kazi ya Kamati ya Taifa (*The National Multi-Disciplinary Committee on Anti- Money Laundering*) ambavyo ni vyombo vivilyoanzishwa chini ya Sheria iliyotungwa na Bunge lako ya Money Laundering na kazi kubwa sasa tuliyonayo sisi ni kuwatambua na ushirikiano unahitajika kwa mamlaka zote na watu wote pamoja na Wabunge ambaо wanasema wana taarifa hizo. Nimesikia hoja kwamba majina hayasaidii, kwa kweli majina yanakupeleka mahali, majina yanakupa anuani, majina yanatambulisha marafiki zako, kwa hiyo, ni muhimu sana kupata jina kusudi uweze kufahamu anuani ya mtu huyo, watu anaokula nao, akina dada anaotembea nao na mapenzi yake mahali gani yapо, ni muhimu sana. (Makof/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tano, nafanya hivi kwa nia njema, sina sababu ya kuipiga chini hoja kwa sababu mwisho wa siku tutafikia muafaka. Pendekezo la tano kwamba Serikali katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja, ilete taarifa ya hatua ilizochukua ili kuziba mianya ya utoroshaji wa fedha nje ya Tanzania. Hoja hiyo, nitakuja kuisemea mwisho.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la sita kwamba Serikali katika bajeti ya mwaka 2013, nafikiri 2013/2014 itaanzisha kodi maalum (*Financial Transaction Tax*) ya angalau asilimia 0.5 ya thamani ya *transactions*, Kiswahili chake, ili kuweza kuwa na rekodi za uhakika za fedha za ndani na zinazotoka nje ya nchi. Pendekezo hili ni zuri, lakini tunahitaji kulifanyia utafiti wa kutosha ili kuamua kama inafaa kuanzishwa kodi ya aina hiyo. Ninapendekeza pendekezo hilo liachiwe Serikali, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha kodi iitwayo *Financial Transaction Tax* na kuweka kiwango cha kodi hiyo kama ikiona inafaa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la saba napendekeza lifutwe kwa sababu hoja iliyopo mbele ya Bunge ni kuitaka Serikali kuchukua hatua dhidi ya Watanzania ambaо wameficha fedha haramu nje ya nchi na halihusiani na utaratibu wa kugawa vitalu vya utafuti mafuta na gesi. Suala la utafuti mafuta na gesi ni suala tofauti kabisa ambalo linashughulikiwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria ile ya *Petroleum Exploration and Production Act* na taratibu za kutunga Sheria hiyo na Sera, kutunga Sheria ya Gesi zinaendelea. Masuala yote hayo yatakuwa yameainishwa ipasavyo. Kwa hiyo, haya mambo mengine yanahitaji hoja mahsus, ile ya MEREMETA pamoja na ile nydingine aliyoisema, zinahitaji hoja mahsus na kweli Bunge linaweza kuwa bado lina nafasi kwa kutumia Kamati zake za Ulinzi na Usalama kupata taarifa ya Serikali kuhusu mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kuwa Serikali imekwishachukua hatua za uchunguzi kuhusu jambo hili na kwa vile kuna baadhi ya Wabunge wameshirikishwa katika uchunguzi huo na kwa kuwa ofisi yangu imekwishawasiliana na mamlaka zinazohusika katika baadhi ya nchi ikiwemo Uswisi. Kwa hiyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liiachie Serikali iendelee na hatua zinazoendelea za uchunguzi na kwamba hii nimeandika na naongeza maneno haya na kwamba vyombo vya uchunguzi vitakuwa huru kuwashirikisha wachunguzi wa nje ili kuharakisha na kuufanikisha uchunguzi huo. Serikali itatoa taarifa yake Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Moja kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, ngoja kidogo basi niseme, kwa mujibu wa Kanuni zetu, hoja ikitolewa inaweza kufanyiwa mabadiliko na kama itatokea hivyo, kuna mabadiliko kama yalivoletwa sasa, tunachojadili sasa ni haya aliyosema Mwanasheria Mkoo, tutakapokubaliana na hayo kama tunakubaliana nayo, basi hii itaondoka kama hatutakubaliana na mapendekezo ya Mwanasheria Mkoo basi tutaendelea na haya mengine moja kwa moja. Kwa hiyo, naruhusu, nilimwona Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Ole- Sendeka.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Naomba nilielekeze Bunge lako Tukufu katika masharti ya Kanuni ya 57(3) na 57(4) na vilevile nitaomba nilielekeze Bunge lako Tukufu katika masharti ya Kanuni ya 58(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia na Kanuni ya 57(3) na (4). Fasili hizo mbili nikianza na fasili ya (3) inasema kwamba:-

*"Kila badiliko linalopendekezwa sharti liwiane na hoja inayokusudiwa kufanyiwa mabadiliko na pia liungwe mkono na lisilingize jambo lolote ambalo, kwa maoni ya Spika, linaweza kuwasilishwa kwa hoja maalum."*

Mheshimiwa Spika, fasili ya (4) inasema:-

*"Badiliko lolote halitaruhusiwa kama, kwa maoni ya Spika linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa."*

Mheshimiwa Spika, sasa hoja za mabadiliko ambazo zimependekezwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali zinasema kwamba:-

- (a) Pendekezo la kwanza kwenye hoja liondolewe kwa kuwa vyombo na mamlaka za uchunguzi nchini zinalishughulikia jambo hili kwa msingi ya Sheria zilizopo;
- (b) Anasema pendekezo la pili liondolewe;
- (c) Pendekezo la tatu liondolewe;
- (d) Anapendekeza pendekezo la nne liondolewe vilevile; na
- (g) Vile vile anapendekeza pendekezo la saba liondolewe.

Mheshimiwa Spika, hayo mapendekezo yote yanayopendekezwa yaondolewe, kwa maoni yangu yanakinzana moja kwa moja na Kanuni nilizozitaja. Kanuni ya 57(3) na Kanuni ya 57(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni zinaruhusu amendment, zinaruhusu mabadiliko kwenye hoja, anachopendekeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali ni kufuta hoja, ni kufuta mapendekezo sio kuyabadiisha, Kanuni zetu zinakataza kufuta mapendekezo, zinaruhusu kubadili mapendekezo. (Makofi)

**SPIKA:** Sema Kanuni inayokataza kufuta.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Soma ile Kanuni inayokataza kufuta.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nachosema, Kanuni ya 57(3) inasema mabadiliko, inaruhusu mabadiliko sio kufuta, mapendekezo ya Mwanasheria wa Serikali anasema lifutwe kinyume kabisa na Kanuni. Najua watasema kwamba Kanuni ya 57(1) inasema unaweza ukafuta maeneo fulani ukaongeza mengine, lakini kufuta maneno sio sawasawa na kufuta hoja, anachopendekeza Mwanasheria wa Serikali hapa ni kufuta Maazimio yanayopendekezwa, hataki ku-amend, hataki kubadilisha anasema futa hii, futa hii, futa hii, inakatazwa na Kanuni, hawezo akafuta hoja anatakiwa aibadilishe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kibaya zaidi ni hiki ambacho amemalizia nacho kwamba ili hii hoja ya Mheshimiwa Zitto iondolewe na ili Serikali iachiwe kuchukua hatua za uchunguzi ambazo imeanza kuzichukua, anataka hoja yote sasa iondolewe. Kwa maoni yangu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali hana mamlaka hayo, mtu pekee mwenye mamlaka ya kuondoa hoja ni mto hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 58(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Sasa mto hoja ni Mheshimiwa Zitto Kabwe, ndiye pekee anayeweza kuifuta hoja yake, ndiye anayeweza kuiondoa hoja yake. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mamlaka yake kwa mujibu wa Kanuni hizi ni kuomba mabadiliko ya hoja, hawezo akaomba hoja hii ifutwe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba Kiti chako kwa sababu 57(3) na (4) zinasema inabidi urudhike wewe Mheshimiwa Spika, uridhike kwamba mabadiliko yanayopendekezwa hayapingani moja kwa moja na hoja na mabadiliko ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanapingana moja kwa moja na hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Zitto, hayaruhuswi.

Mheshimiwa Spika, nakuomba utumie mamlaka yako umwelekeze Mheshimiwa Mwanasheria wa Serikali kwamba hawezo akaleta mabadiliko haya kwa sababu yanakwenda kinyume na Kanuni za Bunge hili na vilevile hawezo akaomba hoja iondolewe yeze sio mto hoja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naongeza muda kwa mamlaka niliyonayo kwa mujibu wa Kifungu cha 28, naongeza nusu saa kabla ya saa ya kuahirisha Bunge. Naomba kila mtu ajielekeze kwenye badiliko hili sio vinginevyo. Mheshimiwa Chief Whip.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nimpongeze tena Mheshimiwa Zitto kwa hoja yake binasfi aliyoitoa tangu jana na wachangiaji wote.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, hoja hii ni muhimu, hakuna hata Mtanzania mmoja awe kiongozi wa Serikali, Mbunge au mwananchi wa kawaida ambaye anafurahia wizi na utoroshaji wa fedha kwenda nje, hakuna! Jana wakati wa michango, wengine walikuwa wanasema huko mbele huko, kote hakuna hata anayehusika yaani hakuna anayekubali jambo hili, sisi wote tunatoka katika mazingira yanayofanana, hakuna. Sasa mwizi atazamwe kama mwizi na lazima ahudumiwe kwa mujibu wa Sheria, ahukumiwe, achukuliwe hatua kama mwizi, lakini haliwezi kuwa jambo la jumla.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nampongeza sana Mheshimiwa Zitto leo, maana leo rafiki yangu Tundu Lissu anazungumzia karatasi za jana, lakini baada ya uchangiaji wote Mheshimiwa mto hoja amekuja na version tofauti maana leo alikuwa na fursa mto hoja ya kutafakari waliyoyasema wenzake wote na kuja na majumuisho haya aliyojuja nayo. Kwa hiyo, rafiki

yangu Lissu alikuwa anasoma karatasi ya jana lakini mto hoja amekuja na version mpya leo baada ya kuchangiwa jana na amekuja na version mbili, amekuja na maombi mawili, anasema Kamati Teule iundwe na yeche mwenye ushahidi na wengine wenyewe ushahidi watakuwa tayari kipeleka makaratasi yao pale yaani Kamati Teule ya Bunge, ndio nasema, sasa Mheshimiwa Halima utaomba nafasi yako baadaye, ya kwako ya ardhi ilikwisha jana. Amesema Kamati Teule au pendeleko la pili kama ikiwezekana angependa jambo hili lifanyiwe uchunguzi, lakini pia lishirikishe wachunguzi binafsi wa nje na ametoa mfano wa Senegal, ametoa mfano wa Kenya waliofanikiwa katika jambo hili.

**SPIKA:** Na Ufaransa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, ndio na Ufaransa, ametoa mfano ili kurahisisha jambo hili tutumie wachunguzi wa nje ambao wamefanikiwa, Ufaransa na Senegal Rais mpya aliyeingia amefanya jambo hili na amefanikiwa. Mimi nasema haya ni mawazo, huyu mto hoja baada ya kuwasikiliza wachangiaji wote na ndio utamaduni wa Bunge, huwezi kuwa na kichwa kilichoganda yaani tangu jana wote sisi tuseme pumba tu? Halafu unakuja kutoa majumuisho yako kwa maneno yaleyale ya jana? Mtoho hoja amelala, ametafakari, amekuja na hoja mahsus.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa sababu, kazi hii imeshaanza na Mwanasheria Mkuu anazo hata barua, amezisoma jana, ambazo amewasiliana na mamlaka za Switzerland; ameshasoma jana na TAKUKURU wenyewe wameshaanza na ni ukweli ulio wazi na baadhi ya Wabunge hapa wameshapewa hata mialiko na Taasisi hizi na Mheshimiwa Zitto anajua kwamba, baadhi ya Wabunge hawa wanaosema wameshapewa mwaliko na Taasisi hizi za uchunguzi kwenda kusaidia katika jukumu hili ambalo limeshaanza. Mheshimiwa Zitto, anajua na wengine wanajua, kwa hiyo, kazi hii imeanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninakubaliana kwamba kazi hii iende, lakini pia naunga mkono wazo la Mwanasheria Mkuu ambalo amelikopi kutoka kwa Mheshimiwa Zitto kwamba ili kasi hii iende vizuri, tushirikishe vilevile *Private Investigators* kama walivyoferia Senegal, Ufaransa na Kenya. Hili ni wazo ambalo Mwanasheria Mkuu amekubali. Mwanasheria Mkuu huyu hawezi kukaa hapa akavumilia wizi wa fedha ya Serikali, hawezi! Kama kuna njia yoyote ambayo inaiwezesha Serikali kupata hela zake na kupata taarifa yake, atafanya tu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hili ni wazo la Mheshimiwa Zitto lakini na Mwanasheria Mkuu hapa amekubali kwamba watawatumi hata hao Wapelelezi wa Kimataifa waliosaidia Kenya, Ufaransa na Senegal kupata pesa zao ili jambo hili likamilike. (Makof)

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu ambalo ninaunga mkono mapendekezo ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, taarifa hii Mheshimiwa Mtoho Hoja amesema isiihie huko; taarifa hii ya uchunguzi ambayo imeshirikisha na vyombo vya nje ilete hapa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Moja. Mwanasheria Mkuu, amekubali.

## TAARIFA

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa! Taarifa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, Taarifa!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa ni kwamba sijakubaliana kwamba hoja hii iondolewe kwa sababu ukishaiondoa hoja, ina maana kwamba, hakuna chochote ambacho tumekifanya toka jana.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, hii page moja, ni ya kuifuta hoja, ni ya kuiondoa hoja, naomba iangalie vizuri. Ikitomwa vizuri, hayo mapendekezo, hata kama atachomeka masuala ya Private Investigators, ukiisoma kwa ukamilifu wake, Mwanasheria Mkoo wa Serikali anataka hoja iondolewe Bungeni kitu ambacho sio sahihi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa kufanya ni kufanya amendments kwa ajili ya ku-improve na tuweze kutoka tukijua kwamba tunafanya hivi, tuna-engage Private Investigators na Mkutano wa Kumi na Moja tutaletewa taarifa ya utekelezaji huo. Kwa hiyo, kama Mwanasheria Mkoo atarekebisha na kuondoa hayo maneno ambayo yanaiondoa hoja kwenye Bunge, hatutakuwa na shida kama hii. Tatizo letu ni kwamba, amendments za Mwanasheria Mkoo wa Serikali, zinaifuta hoja, iwapo zitakubaliwa na Bunge.

**SPIKA:** Ngoja kwanza nimwite Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naendelea kumpongeza Mto Hoja kwa hoja yake nzuri...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, sijamaliza.

**SPIKA:** Mimi nilifikiri umemaliza!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Sijamaliza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, kidogo ukae kusudi tumwite Mheshimiwa Lukuvi, amalize maneno yake, kidogo tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana maana ndugu yangu Mheshimiwa Zitto, alinipa tu Taarifa ambayo bila ya shaka Mwanasheria Mkoo ameitaafakari na atatoa maelezo. Ni Taarifa imepitia kwangu lakini ilikuwa inaenda kwenye desk la Mwanasheria Mkoo.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi kwa sababu hatuna muda, ukisoma *spirit* ya Mheshimiwa Zitto, bado anakubaliana na mawazo ya AG, sipokuwa tu lugha irekebishwe.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliguna)

**SPIKA:** Naomba uendelee Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, lugha itarekebishwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo, amesikia, yeche asichotaka ni kwamba, hoja hii isiwekwe kapuni yaani isiondolewe, isitupwe, ndicho asichokitaka, ambacho anasema Mwanasheria Mkoo amekiandika. Sasa huu mgongano wa lugha Mwanasheria Mkoo ataujibu.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ninakubali kwamba consensus ni hiyo kwamba tulifanyie kazi jambo hili kwa kutumia mbinu zozote za ndani na nje na taarifa ije Mkutano wa Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pendekezo la Mwanasheria Mkoo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Naomba mzungumze kwa kifupi. Kwanza mnafanya amendments, ni dakika tatu tu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba tu kusema kwamba, pendekezo la Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali la kuiondoa kabisa hoja hii, sikubaliani nalo. Sikubaliani nalo kwa misingi kwamba, hii hoja sasa iko mbele yetu na ina mambo makubwa matatu au mawili.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni kudhibiti sababu zinazosababisha kuingia katika upotezaji wa fedha na kwenda kufichwa katika mabenki nje ya nchi. La pili, ni kuchukua hatua kwa watu ambao wametusababishia kufika hapa na kwa maana ya kuhakikisha kwamba fedha zetu zilizoenda nje tunazirejesha.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukianza na pendekezo la kwanza la Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali, anavyosema kwamba, vyombo vyaa mamlaka vyaa uchunguzi vimeshaanza kuchukua hatua na baadhi ya Wabunge wameshirikishwa, hilo mimi ninakir na mimi ni miongoni mwa Wabunge, hawakuniambia kama ni siri watu wa PCCB kwamba, waliniita na kunihoji kuhusu mambo haya. Kwa hiyo, ninakiri kwamba tayari baadhi ya Wabunge tumeshaanza kuhojiwa lakini bado haiondoshi hoja hii ya Bunge hili kuendelea kuiagiza Serikali kuchukua hatua dhidi ya suala hili zima. (Makof)

Mheshimiwa Spika, wakati wa Bunge lililopita, wakati mimi ninawasilisha hoja ile ya kuiagiza Serikali kuchukua hatua kwa watu walioficha fedha nje ya nchi, nikasema zile trillioni 11.6 kwa ujumla wake, nilisema mimi kama Mpina lakini mwenzangu Mheshimiwa Zitto Kabwe, anataka sasa alishirikishe Bunge hili, liiagize Serikali kwa ajili ya kwenda kuchukua hatua kwa watu walioficha fedha nje ya nchi na kuhakikisha kwamba fedha hizo zinarejeshwa hapa nchini kwa ajili ya ustawi wa Taifa na maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa ukienda kwenye hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe, ile ya kwanza, ndio hiyo inazungumzia suala zima la kuhakikisha fedha hizo zinafuatiliwa, fedha hizo zinachunguzwa na fedha hizo zinataifishwa na zinafilisiwa kwenye akaunti za wahusika na kuhakikisha kwamba zimerejeshwa nchini. Kwa hiyo, mimi kama Mpina, kuna mapendekezo yangu ambayo sijayaona, nimeboresha tu lile pendekezo namba moja, lakini ninaomba libaki palepale, Bunge liiagize rasmi leo, kuitaka Serikali kutaja majina ya watu walioficha fedha nje ya nchi, kuztaifisha fedha hizo, kuzifilisi fedha hizo na kuzirejesha hapa nchini kwa ustawi wa taifa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, namba mbili, kuna suala la pendekezo la Mwanasheria Mkoo kuiondoa kipengele namba mbili, nakubaliana nacho. Kuiondoa pendekezo namba tatu, nakubaliana. Kuiondoa pendekezo namba nne, sikubaliani kwa sababu, tunajua kwamba, vyombo hivi viro. Tunajua TAKUKURU ipo, tunajua Financial Intelligence Unit ipo, tunajua The National Multi-disciplinary Committee on Money Laundry, tunajua ipo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, tunapofikia kwenye kufanya uamuzi dakika sio 15 ni tatu (3) tu, kwa hiyo, muwe precise.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwa speed ili niweze kumaliza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pendekezo namba nne, mimi ninaomba libaki kama liliyvo, kama ambavyo limependekezwa na Mtoa Hoja. Pendekezo la tano, pia kwenye marekebisho yangu lipo; ninachotaka kuondoa tu ni kwamba, ile angalau 5% ya thamani ya transaction, ile tuiondoe na mwaka pale turekebishe badala ya mwaka 2013/2013 iwe 2013/2014; ikiondoka hiyo hapo baadaye Sheria hiyo ya kutaka hiyo *Financial Transaction Tax* itakapoletwa hapa, tutatafakari kuhusu kipengele hicho.

Mheshimiwa Spika, ninachokubaliana na Mwanasheria Mkoo, ni kipengele pia cha saba ambacho ni cha mwisho. Naomba hii hoja ya Mwanasheria Mkoo, *i-hold* kwenye kipengele kile cha saba; nakubaliana nacho hicho kwamba Serikali wao waendelee na uchunguzi wao, Bunge la mwezi wa nne watuletee uchunguzi wao na tusiporidhika na uchunguzi huo, Tume sasa ya Bunge iundwe ichunguze suala zima la utoroshaji wa fedha nje ya nchi. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi napenda niungane na wenzangu kuunga mkono hoja ya Mwanasheria wa Serikali kwamba suala hili lichukuliwe na Serikali. Si kwamba tunaitupa hoja, lakini tunachosema ni kwamba Serikali iichukue na wale ambao tuna uhakika kwamba, wenye wana sema kwamba, wana uhakika, wanalifahamu vizuri suala hili na kwamba hawawezi kutoa taarifa zao mbele ya Bunge au hawawezi kutaja majina mbele ya Bunge kwa sababu haina maana kufanya hivyo, basi wapeleke hizo taarifa zao.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa Kanuni za Bunge, unapozungumza suala lolote ambalo una makabrasha yoyote au una ushahidi, huwa tunaweka Mezani, kwa maana ya kwamba, unamkabidhi Spika, halafu Spika anapeleka kwenye chombo husika. Kwa hiyo, kama wao kwa kufanya hivyo wanaona aidha, watafilishi ule ushahidi au ni hatari kwao, basi tuwaombe wamwone Mwanasheria Mkoo wa Serikali ili asaidie vile vyombo kufanyia kazi hili suala ili Serikali katika Mkutano wa Kumi na Moja, itakapokuja kutoa taarifa, basi taarifa hizo na zenyewe ziwe zimeingiza na hayo majina ambayo yatakuwa yamepatikana kwa wakati huo ili iweze basi kushawishi Bunge kama ipo haja sasa ya kuunda hiyo Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, mimi ninachokiona, hivi tunaposema Kamati Teule iundwe ndio ikachunguze, hivi kweli, Bunge sisi ni chombo cha kuchunguza matuhuma makubwa kama hayo ya kuweka pesa nje? Sijui? Nitasaidiwa. Au unaiambia Kamati Teule sasa ianze kwenda katika Mabenki ya Swis, ambayo hatuyajui yako mangapi kwa sababu Tanzania nafahamu tuna mabenki karibia 48 au 44; sasa wanafika pale wanaanza kuuliza, tunaomba majina ya Watanzania ambao wamewewa pesa huku nje, hivi kuna mtu atatuelewa?

Mheshimiwa Spika, mimi nilifikiri ni vizuri wale wenzetu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Zitto, ambao wenye wana ushahidi, ni vizuri wakaisaidia Serikali kupeleka hayo majina ili hata Tume ikiundwa basi wakifika kwenye benki hizo zinazotajwa, wanafika pale wana sema tunaomba majina haya mtuambie wana pesa kiasi gani. Hii itakuwa rahisi kwa wale wanaochunguza kuweza kuchunguza, je, hizo pesa wamezipata kiuhalali au visivyo?

Mheshimiwa Spika, lakini si kama tu wataisaidia Serikali, pia watasaidia Wabunge wengine ili siku nyingine. kwa sababu hapa hawatoi hayo majina, lakini nina uhakika si ajabu Mheshimiwa Zitto, akikaa nje huko wakati mwingine kuna watu anawaambia ni fulani na fulani na fulani. Sasa, ili kuondoa ile hali ya kutuhumiana au hali ya kuchangia kama juzi alivyochangia Mheshimiwa Kessy kwamba pesa zipo, tunaomba twende kwa Wazungu tuwaambie waturudishie pesa zetu; lakini akiitwa siku nyingine na Kamati, hebu zitaje hizo pesa ziko kiasi gani, ni Wabunge kiasi gani, nadhani yatakuja majibu kama ambayo Mheshimiwa Spika muda mfupi hapa umekuwa ukiyasema. Sasa hii itasaidia kuondoa hiyo dhana ya Wabunge kujisemeasemea tu, akina Mheshimiwa Tundu Lissu, kuita vyombo vyaya habari wakazungumzazungumza tu vitu ambavyo havina ushahidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niliombe Bunge lako Tukufu, wale wote ambao wana ushahidi wa majina na Benki walikoweka, wampatie Mwanasheria wa Serikali ili akatumie hivyo vyombo ambavyo kisheria anaweza kufanya navyo kazi, akafanye kazi kwa kipindi hiki mpaka Mkutano wa Kumi na Moja, watutolee taarifa, ili hoja ile ya Mheshimiwa Zitto ijadiliwe vizuri zaidi katika Bunge hilo la Mkutano wa Kumi na Moja na hapo ndipo tutakapoamua kama kuna haja ya kuunda ile Kamati au la. Lakini pia ili kuwasadia Wabunge kuitwaitwa kwenye Kamati ya Haki na Maadili ya Bunge, kwa sababu tu ya kusemasema maneno ya kusikia. Tunaomba wenyewe majina wapeleke, wenyewe ushahidi wapeleke, kwa sababu hapa imethibitika hakuna aliyeomba kuyataja yale majina. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka! Muda wenyewe muangalie. Mheshimiwa Ole-Sendeka!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Nataka niseme jambo moja kwa mabadiliko yaliyotolewa na Mheshimiwa Attorney General. Ukichukua hoja ya Mheshimiwa AG, kimsingi inaondoa kama ikitaki kama ilivyo, inakosa sifa ya hata ya kujadiliwa kwa sababu, inakinzana na Kanuni ya 57(1)(a) inayosema:-

"Hoja ikishatolewa ili iamuliwe inaweza kubadilishwa kwa:-

(a) *Kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine*". (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hapa hoja haiingizi lolote, inaondoa yote bila kuingiza chochote. Lakini la pili kwa maana hiyo, sasa unaendelea kwenye Kanuni hiyohiyo ya 57(3) na (4), utaendelea mwenyewe kwa faida ya yejote anayetaka.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni tusifanye dhambi ya kuondoa hoja hii, hoja hii ni ya msingi sana. Ni ya msingi, lakini ningetaka sana ipate maana zaidi kwa watu kupata ujasiri wa kukamilisha hoja hii iweze kuwa na mashiko. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na namna yake ni kutaja majina. Bunge hamwezi mkaambwa tu kuna watu wameweka fedha Uswisi, mkaufika mahali pa kuunda Kamati Teule, mkatafuta Private Investigator, wakati hamna hata mahali pa kuanzia. Mimi ningependa kusikia mlongoni mwa wenyewe fedha hizo ambazo tunahisi ni fedha haramu ni fulani na fulani, lakini wako wengi, tuendelea na kujua na wengine na uhalali wa fedha walizonazo, wala msione haya. Rafiki yangu Mheshimiwa Zitto, wala usidhani kwamba ukiwataja hao utakuwa umekosea, utakuwa umekamilisha hoja yako, itakuwa ni hoja halisi na itawasaidia hata wanaochunguza; iwe ni Private Investigator, iwe ni Kamati Teule ya Bunge, itatusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninataka kusema kwa mfano, leo ukizungumza habari ya kama pendekero la saba lilivyo, pale chini umetaja mionganoni mwa fedha zilizokwu zimetoka Benki Kuu kuitia Kampuni ya Meremeta na Deep Green Finance, hawa wapo na

wanajulikana. Deep Green na hawa waliokuwa Meremeta wanajulikana. Ukienda kwa Wasajili wa makampuni pale, utajuwa ni akina nani waliokuweko mle ndani, ni rahisi kujua, umewataja maana tayari hizi ni Taasisi, ni legal entities, unaweza kujua wanaouna ni akina nani lakini hao walioweka fedha huko, tusaidieni, wala si fedheha kuwataja na hapo Bunge hili litapata uhalali wa kuunda Kamati Teule kwa mujibu Azimio namba saba, hata mimi nitaunga mkono pendekezo hilo la kuundwa kwa Kamati Teule. Kama basi hamkutaja majina, basi twendeni kwa Private Investigator akachunguze, ili uchunguzi uletwe hapa lakini kama mna majina, tuunde Kamati Teule, tuenze na hao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ni rai yangu kwamba, hoja hii isiwekwe pembedi. Twende na Azimio la kuchunguza ili kuinusuru nchi hii na watu ambao wanakuwa na fedha haramu katika mabenki ya nje na msione haya kwa yeyote yule...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Jamani, ninaishiwa muda, naomba sasa nimwite Mto Hoja. Tunazungumzia mabadiliko haya tu, Mheshimiwa Mto Hoja!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nami nina uchungu sana. Ninatafuta njia ya kufikia huko ambako Waheshimiwa Wabunge wanapenda tufike. Kitu nilichofanya mimi, sikufuta hoja. Ukitosha Kanuni ya 57(1) (a), (b) na (c), nimeondoa maneno, nimeingiza maneno.

Mheshimiwa Spika, ninachosema mimi ni kwamba, Select Committee ya Bunge, inanipa matatizo kwenye Katiba; ndicho nilichosema Waheshimiwa Wabunge. Kwenye Kanuni, tulipatana juzi, basi nimekusamehe Mbunge wangu wa Ubungo. (Kicheko)

**SPIKA:** Naomba uongee na mimi hapa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichosema ni hicho kwamba kama inawezekana...

## TAARIFA

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Waheshimiwa, naomba tuendelee muda unakwisha. Maana tuna...

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwenye Pendekezo la kwanza...

**SPIKA:** Waheshimiwa, mna haki ya Taarifa lakini mimi hapa ninakaa kusudi nisikilize kila mtu anamalizaje neno lake, mkimuingilia na mimi mtanichanganya, Mheshimiwa endelea kidogo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimeondoa lile pendekezo la kwanza, lakini bado pendekezo lile linaweza kubaki kwa sababu ndicho kinachofanyika. Sasa tuliongeze kwamba Serikali na vyombo vyake vya uchunguzi iwasiliane na Benki ya Dunia ili kupitia Kitengo cha Assets Recovery Unit, ili mabilioni hayo, bla, bla, mpaka mwisho kule basi libaki hilo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, suala lile la pili la Muswada, nimesema kwamba sheria ile ya *Foreign Exchange Act* ina masharti hayo yanayozuia na Gavana anayo mamlaka kwa kanuni zile zilizotungwa na Waziri. Kwa hiyo, ile ya pili na ya tatu zinaangukia pamoja.

Mheshimiwa Spika, ile ya nne, ile ya kwamba hawa watu waeleze tunaweza kuiacha ikabaki kama ilivyo lakini ndivyo vyombo hivi vinafanya hayo. Kwa hiyo, nilichosema mimi ile nilikuwa nimeondoa kusudi isomeke vizuri.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwenye ile ya tano niseme kwamba hili jambo kwa ujumla wake ndiyo maneno nilioingiza kwa ujumla wake Serikali iyafanyie kazi na ije kwenye Bunge la Kumi na Moja itoe taarifa ya hatua zillizofikiwa. Ndicho nilichokuwa nasema. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ile ya sita mnaona kwamba hilo ni suala ambalo huwezi kuliamulia ukiwa na *microphone*, unatakiwa ulifanyie utafiti. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwamba hili la sita siyo kwamba tunalitupa, Serikali italiangalia na itatoa taarifa yake kwamba tumeliona hili jambo tunastahili kufanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama kweli kuna mapesa haya na kwa watu ambao hawakupata kibali cha Gavana, inawezekana hii haitoshi, sasa hilo hatuwezi kufahamu.

Mheshimiwa Spika, hili la saba nasema kuna vitu vitatu vinazungumzwa mle ndani, kwa mujibu wa kanuni zetu, hii hoja inatakiwa kuwa mahsus. Hoja iliyo mbele yetu ni kuhusu kuficha fedha. Sasa inawezekana mwingine anasema kwenye sijui Meremeta ndizo hizohizo. Mheshimiwa lazima niwe mkweli kwamba suala la Meremeta mimi nilikuwa napendekeza kwamba Serikali itoe taarifa yake kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, Kamati ya Bunge kwenye Bunge la Aprili, Bunge la Kumi na Moja kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Kabwe kuna mambo mengine hatuwezi kujivua nguo.

Mheshimiwa Spika, basi kwa maana hiyo, kwa *spirit* hiyo ya kuleta uelewano ndani ya Bunge lako na kwamba maslahi yetu ni mapana kuliko koti yangu, nchi hii mazingira yake ni makubwa. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wakubaliane na mimi na Serikali ilete taarifa ya utekelezaji wa mambo haya. Katika kufanya hivi, vyombo vya uchunguzi vinaweza kutumia *Private Investigators*, vinawenza kutumia mamlaka yoyote ya nje ili kupata hizo taarifa kwa usahihi. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wenye majina, nawaombeni mpelekee vyombo vya uchunguzi, TAKUKURU na kama unaona TAKUKURU labda watakuuliza maswali ya uchaguzi na nini niletée mimi nitawapelekea.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimeona tu nisimame kutumia muda wako mfupi kwa ajili ya jambo hili kubwa ambalo limekuwa na mjadala mkubwa sana tangu jana.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Kabwe kwa kuwasilisha hoja hii lakini niwapongeze vilevile Wabunge wote kwa ujumla kwa sababu michango ilikuwa ya wazi na kila mmoja alisema mawazo alivyoona inafaa. Lakini namshukuru vilevile AG kwa mchango wake mzuri.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni jambo kubwa na lazima tulifanye kwa umakini mkubwa na nafikiri ndiyo maana Mheshimiwa Kabwe kwa msingi huo wa umakini amekuwa mwangalifu sana kila tunapajaribu kumbana ataje majina anayo lakini anasita, nadhani ni kwa sababu za msingi kabisa kwamba kweli uhalali wa yale yaliyofanywa na hao kumi na wa tatu ni vizuri yakafanywa kwa namna ambayo inampa comfort na kumwondolea ile hali ambayo inaweza kuibuka baadaye ya kuzua jambo ambalo pengine huna ushahidi nalo. Kwa hiyo, mimi nafikiri ni jambo nzuri sana na mimi nakusifu sana kwa jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tupo hapa kwa kweli kwa jambo moja tu, kujua ni nani hawa Watanzania ambao wamekwenda wameweka fedha nje ya nchi kinyume cha sheria. Kwa sababu kuweka fedha nje si tatizo lakini lazima iwe kinyume cha sheria na ndiyo haswa msingi wa mjadala ndani ya Bunge. Sasa fedha hizi zinaweza kuwa zimetoka hapa Tanzania, lakini inawezekana kuna wajanja wameiba nchi nyininge vilevile lakini Watanzania wakaenda kuweka hukohuko, sasa concern yetu ni zile fedha ambazo ni haramu lakini zimetoka Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niombe, kikubwa hapa mimi ninachokiona, hoja hii mimi sina ugomvi nayo, ukichukua ya kwanza, ya pili, tatu mpaka ya mwisho, alichokuwa anajaribu kufanya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba pengine tunahitaji kufanya kazi kwenye hatua ile ya Select Committee ambayo itaiwezesha Serikali vilevile kuwa ni sehemu ya yale yanayotakiwa kufanyika kwa sababu kuna mahali pengine mtatuhitaji hasa baada ya kubaini ukweli wa kiasi fulani pale lazima tufuate mikondo rasmi ambayo inataka sasa mahusiano ambayo hayaleti tena migogoro ya kwa nini. Mimi katika jitihada hizi za kujaribu kufuatilia jambo hili, kimoja ambacho tulikwama ni pale waliposema hatuwezi kusema lolote mpaka mtwambie ni nani huyo mnayemtuhumu, ana shauri gani la kisheria ambalo linafanya sisi tuseme kwa sababu hiyo basi tunatoa jina. Sasa sisi hatukuwa na kitu na msingi wowote wa kisheria pale. Kwa hiyo, hii ni fursa nzuri ambayo inaweza ikatuwezesha tukafika pale. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi napenda kukubaliana na AG lakini lazima tu-modify ili Bunge lijisikie kwamba wote tumeridhika, wasiwasi kwamba likienda kule kimyakimya tutaficha baadhi ya taarifa, hatuna sababu ya kuficha kama ni mwizi ni mwizi tu, kama ameiba hela yetu ni mwizi tu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukubali vyombo viendeleze hili zoezi kwa sababu ya fursa ile waliyonayo. Lakini tumwombe vilevile Mheshimiwa Kabwe atu-link na huyo mtu anayeweza kutusaidia kama mchunguzi ambaye amebobea katika vyombo hivyo tum-hook na vyombo hivyo. Mimi naamini taarifa itakayoletwa, itakuwa ni taarifa safi kwa sababu sisi hatuwezi kuwa ni wajinga, Kabwe atoe majina kumi na matatu, atudokeze na mtu ambaye atatuwezesha halafu sisi tuchakachue wakati majina anayo atasimama hapa na kusema nyie ni watu wa ajabu sana, nimewapeni fursa kubwa mmekwenda kule mmemwacha Pinda, mmemwacha nani, hata Werema hakumweka pale, kwa hiyo naamini mwisho wa yote tutafikia lengo nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikusihu tu ukikubali hilo basi kama tutashindwa kwenye Mkutano wa Kumi na Moja na mimi nasema hatutashindwa labda kama huyo mtu ambaye ndiye Kabwe anamsema awe ni mtu ambaye naye afike mahali aseme bwana sikuwa na

uhakika na haya, tatarudi na kusema ametuambia hivyo lakini vinginevyo nadhani tuna kila sababu. Kwa kufanya hivyo, tutafikia mahali pazuri na hatutalilaumu Bunge wala Serikali wala mtu mwingine yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa na shughuli ya kusoma kila Azimio la hoja ya Mheshimiwa Zitto, nikakuta kifungu cha saba cha kuunda Kamati Teule, haiwezi kuundwa Kamati Teule kwa hoja hii, lazima ije kwa hoja yenyewe inayojitegemea. Kwa hiyo, kwa maana ya kifungu cha saba, hata tungefanya nini, muda tulionao hawezu kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule, naomba muelewe hivyo kwa sababu hoja hii haiundi Kamati Teule, Kamati Teule ina utaratibu wake na nafikiri wote mnaufahamu.

Lakini ukiondoa hiyo ya saba, ukasoma ya kwanza inasema kwamba, Serikali iwasiliane na Benki Kuu. Ukisoma ya pili inasema kwamba, Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni. Ukisoma ya tatu inasema kwamba, katika Muswada uliotajwa hapo Gavana wa Benki Kuu ni Serikali. Ukisoma ya nne inasema kwamba, Watanzania wote wenye akaunti zao nje waeleze wamezipataje na huwezi kuzipata mpaka umewataja hao. Ya tano inasema kwamba, Serikali katika Mkutano wake wa Kumi na Moja ilete taarifa kuhusu haya mambo na hatua zilizochukuliwa. Ukisoma ya sita inasema kwamba, bajeti ya Serikali ifanye hivyo. Kwa hiyo, ukiangalia yote haya *in short* yanasema kwamba, kwa kuwa Serikali imekwishachukua hatua au inaendelea kuchukua hatua, ikafanye tena zaidi kuhusiana na masuala haya, yote ameagiza Serikali na Serikali inasema inaomba iendelee. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hoja iliyohapa kwamba haya ya Zitto siyo kwamba yanaondolewa kwa maana ya kuyatupa yameingia katika utaratibu mzima ambao Serikali itakwenda kufanya kazi ambapo katika Mkutano wa Kumi na Moja Serikali iweze kuleta taarifa, kama hawajaridhika siku hiyo Kamati Teule iundwe, hivyo ndiyo inavyotakiwa. Sasa nitawahoji. (Makofi)

(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Kwa hiyo basi, naomba ieleteke kwa vyombo nya habari, Azimio la Mheshimiwa Zitto halijatupwa, katika nafasi zake zote alikuwa anaitaka Serikali, Serikali yenyewe inaji-commit kwamba itumie vyombo vyake nya ndani na nje iweze kukamilisha haya Mheshimiwa Zitto aliyyaweka. Kama watakuja katika Mkutano wa Bunge la Kumi na Moja hawana maelezo ya kutosheleza, iletwe hoja mahsusni ya kuunda Kamati Teule. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nina uzoefu, kama niliyosoma leo hii, taarifa hii imenisumbua sana, tunapenda sana Wabunge ushabiki, tunatumia hela za Serikali kwa ushabiki mkubwa sana, ukifika watu wanakuambia mimi nilinogewa tu na hoja, hapana jamani tufanye kazi muhimu, hili suala ni zito na mimi nasema kama tukifanikiwa, tutakuwa tumefanya *milestone* ya nchi kabisa kujigeuza kwenda kule tunakotaka. (Makofi)

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nina tangazo moja tu dogo, sijui nani hawa, Bunge Sports Club, wanasema wakutane sasa hivi katika ukumbi wa Msekwa.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.30 Mchana Bunge *lilisitishwa*  
mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

**SPIKA:** Agenda tuliyobakia nayo ni moja na wengine hawataki kuahirisha kikao, wameshajahirishia huko huko na wengine ndiyo hivyo wamechelewa.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema, mkumbuke leo itakuwa ni siku ya mwisho kuwa pamoja. Kuna suala zima la kujaza Fomu za Maadili. Msifanye mchezo, kwa sababu hali halisi kuhusu Fomu za Maadili ni muhimu sana. Mkumbuke kwamba ambao hawajachukua hapa, chukueni, maana mkienda Dar es Salaam itakuwa ni shughuli ngumu sana kwa sababu kwanza kwenda sijui wapi huko halafu ndiyo mjaze, itakuwa ngumu.

Pili, ni suala zima la *NIDA*. Kwa hiyo, nayo pia...

**WABUNGE:** Hatusikii!

**SPIKA:** Hamsikii?

**WABUNGE:** Ndiyo!

**SPIKA:** Tunasikilizana sasa?

**WABUNGE:** Ndiyo!

**SPIKA:** Nilikuwa nasema kwamba, zile Fomu ambazo tulikuwa tunatoa pale, ni vizuri kabisa msifanye usahafulifu wa kutokuzichukua kwa sababu siku hizi zile fomu ni muhimu. Unaweza kupelekwa Mahakamani kwa kutokujaza zile fomu. Siyo kwa kujaza habari isiyo sahihi, lakini kutokujaza peke yake ni kosa. Kwa hiyo, mnaombwa sana mlifikumbuke hilo kwa sababu unaweza kujikuta unapoteza muda wako kwenda huku na kule kwa sababu hiyo tu.

Pia, suala la kuweka mihuri vidole vyenu, ingawa leo ilikuwa ni siku ya mwisho, nadhani mmeweza ku-meet sehemu hiyo.

Sasa mambo mengine, mtoa hoja wa kuahirisha kikao sijui amekwama na traffic njiani? Naomba msubiri dakika mbili tu.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge Walimsubiri Mto Hoja  
kwa Dakika Mbili Kama Ilivyoamuliwa na  
Mheshimiwa Spika)

**SPIKA:** Katibu naomba kengele ipigwe ili kuingiza watu ukumbini, naomba kengele ipigwe.

(Hapa kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge  
Waingie ndani ya Ukumbi)

(Hapa Mto Hoja Aliingia Ukumbini)

**SPIKA:** Katibu tuongoze tafadhali!

**KATIBU WA BUNGE - DKT. THOMAS D. KASHILILAH:** Hoja ya Kuahirisha Bunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu utoe hoja ya kuahirisha Bunge.

#### **KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, katika masuala ya jumla, kwanza ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tunapohtimisha shughuli zilizopangwa kufanyika katika Mkutano wa Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kipindi tulichokuwa hapa takriban siku 11, wapo Waheshimiwa Wabunge ambao walipoteza wapendwa wao, akiwemo Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki, aliyepoteza mtoto wake kwa kuzama majini pale Dar es Salaam. Tunampa pole sana. Aidha, tunawapa pole wote walipoteza Wapendwa wao kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Tisa, jumla ya maswali 119 ya msingi na 293 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge. Maswali mengine 14 ya msingi na 11 ya nyongeza yaliulizwa kwa utaratibu wa Maswali kwa Waziri Mkuu kila Alhamisi.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Miswada ya Serikali ifuatayo ilisomwa na kujadiliwa:-

(i) Muswada wa Sheria ya Haki za Wagunduzi wa Mbegu za Mimea wa Mwaka 2012 [*The Plant Breeders Rights Act, 2012*]; na

(ii) Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2012 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.3) Act, 2012*].

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge waliweza kujadili na kuitisha Maazimio yafuatayo:-

(i) Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Pili ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya pamoja na Nchi Wanachama wa Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pasifikasi [*Cotonuo Partnership Agreement*];

(ii) Azimio la Bunge la Kuridhia Kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane;

(iii) Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka na Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa Gombe;

(iv) Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki [*The Protocol on the Establishment of the East African Kiswahili Commission*];

(v) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba Mpya wa Umoja wa Posta Afrika, 2009 [*The Convention of the Pan African Postal Union (PAPU) of 2009*]; na

(vi) Azimio la Bunge la Kuridhia Katiba na Mkataba wa Mawasiliano Afrika, wa Mwaka 1999 [*Constitution and Convention of the African Telecommunications Union (ATU) of 1999*].

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipokea Kauli ya Serikali kutoka kwa Mawaziri kuhusu masuala yafuatayo:-

- (i) Fao la Kujitoa (*Withdrawal Benefit*) toka kwa Waziri wa Kazi na Ajira;
- (ii) Viwango vya Chakula cha Wafungwa Magerezani kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi;
- (iii) Tatizo la Utengenezaji wa Dawa Bandia ya Kupunguza Makali ya UKIMWI kutoka kwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii;
- (iv) Mpango Maalum wa Serikali wa Kutatua Tatizo la Maji katika Jiji la Dar es Salaam kutoka kwa Waziri wa Maji; na
- (v) Tatizo la Mafuta Nchini kutoka kwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Bunge lako Tukufu limepokea na kujadili Hoja Binafsi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambazo tumeweza kuzijadili hadi mwisho.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika Bunge la Bajeti tulipitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013 ya jumla ya Shilingi Trilioni 15.19. Kati ya fedha hizo, Fedha za Matumizi ya Kawaida ni Shilingi Trilioni 10.60 na Fedha za Matumizi ya Maendeleo Shilingi Trilioni 4.59. Katika kutekeleza Bajeti hiyo, Serikali ilikadiria kukusanya Mapato ya Ndani kiasi cha Shilingi bilioni 8,714.7 (bila kujumuisha mapato ya Serikali za Mitaa) kwenye robo ya kwanza, ikiwa ni sawa na asilimia 18.0 ya Pato la Taifa. Katika Robo ya Kwanza ya mwaka 2012/2013, makusanyo ya kodi na yasiyo ya kodi yalifika jumla ya Shilingi bilioni 1,922.3 sawa na asilimia 91.1 ya makadirio ya kukusanya Shilingi bilioni 2,111.2. Kiasi hicho cha makusanyo kimeongezeka kwa asilimia 19.1 ikilinganishwa na kipindi kama hiki kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato yanayotokana na uingizaji wa bidhaa kutoka nje, katika robo ya kwanza ya mwaka, makusanyo ya kodi kutokana na uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi (ikijumuisha Ushuru wa Forodha, Kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa Bidhaa) ilikuwa Shilingi bilioni 616.1, ikiwa ni asilimia 90.2 ya makadirio ya kukusanya Shilingi bilioni 683.1.

Kuhusu Mapato yanayotokana na mauzo ya ndani, makusanyo halisi ya mapato katika robo ya kwanza yalikuwa Shilingi bilioni 407.4 ambayo ni sawa na asilimia 90.1 ya makadirio ya kukusanya Shilingi bilioni 452.1 katika kipindi hicho. Makusanyo kutokana na Kodi ya Mapato katika robo ya kwanza yalikuwa Shilingi bilioni 691.1 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 657.6, sawa na asilimia 105.1 ya kadirio hilo. Kwa ujumla ukusanyaji wa aina zote za kodi ya mapato ulikuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika robo ya kwanza ya mwaka 2012/2013, mapato halisi kutokana na vyanzo vinginevyo vya kodi yalikuwa Shilingi bilioni 183.6 ikiwa ni silimia 89.9 ya lengo la kukusanya Shilingi billioni 204.1. Makusanyo kutokana na mapato yasiyo ya kodi yalikuwa chini ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni 175.5 ambapo Shilingi bilioni 79.0 zilipatikana, ambayo ni asilimia 45.0.

Wakati huo huo, katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2012, Serikali ilipokea Misaada ya jumla ya Shilingi bilioni 469.8 sawa na asilimia 74 ya makadirio ya Shilingi bilioni 635.8. Kati ya misaada hiyo Shilingi bilioni 402.6 zilikuwa ni misaada ya kibajeti na Shilingi bilioni 67.1 ni za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya Serikali, katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2012/2013, matumizi yalikuwa Shilingi bilioni 2,445.1, ikilinganishwa na makisio ya matumizi ya Shilingi bilioni 3,142.07, ikiwa sawa na asilimia 77.8. Kati ya matumizi yote, Shilingi bilioni 1,924.1 ni matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 521.1 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo zikijumuishwa na fedha za miradi inayogharamiwa na wahisani wa nje. Jumla ya matumizi katika robo ya kwanza yalionesha ongezeko la asilimia 6.0 ikilinganishwa na matumizi katika kipindi kama hicho katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, matumizi kwa ajili ya mishahara yalikuwa Shilingi bilioni 824.2 katika robo ya kwanza ya mwaka huu ikilinganishwa na Shilingi bilioni 679.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la Shilingi bilioni 144.37 au ongezeko la asilimia 21.2. Ongezeko hili lilitokana na marekebisho ya Mishahara katika Sekta ya Umma kuanzia Julai 2012. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, katika kipindi cha robo mwaka, matumizi ya maendeleo yalikuwa ni asilimia 57.4 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kutoa taarifa hii hapa Bungeni, kuonesha kwamba utekelezaji wa Bajeti ya Serikali umeanza vizuri. Aidha, Serikali itaendelea na juhudi zake za kuhakikisha kwamba, mapato ya ndani yanaimarishwa na misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje, hususan kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (Development Partners) na Taasisi mbalimbali za fedha za Kimataifa, inaendelea kuwa chanzo muhimu cha mapato ya kugharimia bajeti ya mwaka 2012/2013. Tayari Serikali imepokea jumla ya mikopo ya Shilingi bilioni 642.5. Kati ya kiasi hicho, mikopo ya nje yenye masharti nafuu ilikuwa Shilingi bilioni 143.4, sawa na asilimia 62 ya makadirio na mikopo yenye masharti ya kibashara kutoka nje ilikuwa Shilingi bilioni 46.6, sawa na asilimia 7.3 na Shilingi bilioni 452.6, ilikuwa ni mikopo ya ndani.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kuwa kwa mara kadhaa ndani ya Bunge lako Tukufu nimekuwa nikieleza nia ya Serikali ya kubana matumizi yasiyo ya lazima wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Nchi yetu ni masikini, hivyo, hatuna budi kutumia kiasi kidogo cha fedha zilizopo kuondokana na umasikini huo na kuwa nchi yenye angalau uchumi wa kati. Kwa mfano, nimekuwa nikizungumzia kupunguza ununuzi wa magari ya kifahari kama vile Toyota Landcruiser VX. Zipo Toyota Landcruiser VX 8- High Specifications na Toyota Landcruiser VX 8- Standard. Bei ya VX 8- High Specifications ni zaidi ya Shilingi milioni 300 kwa gari moja. Kiasi hicho pekee kinatosha kujenga Zahani moja na nyumba mbili za Watumishi.

Aidha, kiasi hicho kinatosha kujenga nyumba sita za Watumishi wa Vituo vya Afya au kujenga madarasa 17 ya Shule za Msingi. Kiasi hicho kinatosha kununua madawati 2,500 ya kukaliwa na wanafunzi watatu watatu, au kununua vifaa vya Maabara katika Shule za Sekondari, na kadhalika. Hivyo, mtaona kuwa tukiacha kununua gari moja la VX-8 tunaweza kusaidia jamii ya Watanzania kwa kiasi kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili kubana matumizi, tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali zifuatazo:-

- (i) Tumekamilisha uchambuzi wa maeneo yasiyo ya lazima kwenye Bajeti yakiwemo Semina, posho zisizo za lazima na kiasi halisi cha fedha zinazoweza kuhamishwa;
- (ii) Tumekamilisha uchambuzi wa maeneo au miradi ambayo inahitaji kuongezewa fedha na kiasi cha fedha kinachohitajika;
- (iii) Hivi sasa tunaandaa Mwongozo wa Ununuzi wa Samani za Serikali; na

(iv) Tumeanza mchakato wa kuwa na viwango maalum vyta magari ya Serikali kwa kuzingatia uwezo wa kiuchumi na madaraja ya Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, ili kuwe na maendeleo, lazima tulipe gharama ya maendeleo hayo. Hii ni pamoja na kujinyima sasa ili tunufaikie zaidi baadaye, sisi na watakaotufuatia kwa maana ya Vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi masikini. Hivyo, tunalo jukumu la kujinyima zaidi kwa ajili ya wananchi wetu. Waswahili husema: "Mchumia Juani, Hulia Kivulini." Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Viongozi mbalimbali na wananchi tukubaliane kwa pamoja katika hatua za kubana matumizi kwa manufaa ya uchumi na maendeleo yetu. Sote kwa pamoja hatuna budi kujenga utamaduni wa kuendesha shughuli za Serikali kwa gharama ndogo. Aidha, maagizo yangu kwa Watendaji wote wa Serikali katika ngazi zote ni kuzingatia Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na kuendelea kuwa na nidhamu katika matumizi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Matumizi ya Serikali. Aidha, tushirikiane kusukuma shughuli za maendeleo katika maeneo yetu ili yaende katika kasi inayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kama baadhi yetu tunavyofahamu, yapo mapendekezo na ushauri ambaa umekuwa ukitolewa na Bunge kuitia Kamati zake kuhusu Serikali kuandaa na kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya ratiba mpya ya maandalizi ya Bajeti ya Serikali. Lengo ni kuleta ufanisi, tija na ubora wa Mipango na Bajeti za Serikali zinazopitishwa na Bunge na kutekelezwa na Serikali.

Katika kuzingatia ushauri huo, Serikali imeandaa mapendekezo ya ratiba hiyo ambayo imewasilishwa kwenye Kamati ya Uongozi ya Bunge ili Kamati iweze kutafakari na kuishauri Serikali ipasavyo. Hata hivyo, mapendekezo hayo ya ratiba mpya ya uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti yameainisha changamoto mbalimbali na mapendekezo ya kukabiliana nazo. Katika mapendekezo hayo, Serikali imefanya marekebisho kwa kuandaa ratiba mpya ya mzunguko wa uandaaji na utekelezaji wa mipango na bajeti ya Serikali ambayo yatasaidia kuboresha utaratibu wa uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali. Mambo muhimu yaliyozingatiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha mwongozo wa uandaaji wa mipango na bajeti ya Serikali unatoka mapema zaidi;

(ii) Uandaaji wa mipango na bajeti kwa Wizara mbalimbali uwe na muda wa kutosha;

(iii) Vikao vya uchambuzi wa mipango na bajeti kati ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango pamoja na Wizara mbalimbali viwe na muda wa kutosha kuchambua mipango na bajeti za mafungu;

(iv) Vikao vya uchambuzi wa mipango na bajeti kati ya Kamati za Kudumu za Kisekta za Waheshimiwa Wabunge pamoja na mafungu viwe na muda wa kutosha kuchambua mipango na bajeti za mafungu;

(v) Bajeti ya Serikali pamoja na Miswada ya Sheria ya Fedha (*Finance Bill*) na Sheria ya Matumizi (*Appropriation Bill*) zipitishwe na Bunge mwishoni mwa mwaka wa fedha;

(vi) Ratiba mpya inazingatia pia ushirikishwaji wa kina wa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta kabla ya uandaaji wa Mipango na Bajeti kukamilika;

(vii) Ratiba mpya ya uandaaji na utekelezaji wa Mipango na Bajeti iwezeshe ushirikishwaji wa wadau wengi ili kuhakikisha bajeti inazingatia matakwa ya Wananchi walio wengi zaidi; na

(viii) Katika mapendekezo hayo, utoaji wa taarifa za uandaaji wa mipango kazi, mipango ya ununuvi na uratibu wa utekelezaji wa mipango na bajeti zimezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba, mara makubaliano yatakapofikiwa, utaratibu wa kutumia ratiba hii utanza kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge walipokea na kujadili pamoja na mambo mengine, Maazimio mbalimbali. Niruhusu nirejee Azimio lilonigusa sana kuhusu Uanzishaji wa Kamisheni ya Lugha ya Kiswahili. (Makofi)

Awali, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Chama cha Kiswahili Tanzania (CHAKITA) na Wawakilishi kutoka Uganda walianzisha wazo la kuwa na Mpango wa Kuundwa kwa Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki. Hata hivyo, Baraza hilo halikuanzishwa, badala yake ikapendekezwa kuanzisha Kamisheni ya lugha ya Kiswahili. Azimio la Kuanzishwa kwa Kamisheni hiyo ya lugha ya Kiswahili tumelipitisha katika Bunge hili. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango mliyoitoa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala kuhusu kuanzishwa kwa Kamisheni hiyo, michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge imeonesha umuhimu wa kutumia fursa zilizopo kwa Tanzania kuwa dira, mfano na kitovu cha lugha ya Kiswahili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge walionesha umuhimu wa kutumia Kiswahili kama nguzo imara ya mshikamano, amani na utulivu mionganoni mwa Watanzania. Lakini pia majadiliano yamebaini changamoto zilizopo.

Moja ya Changamoto hizo ni hoja ya Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba, nchi jirani ya Kenya inatumia fursa zilizopo za lugha ya Kiswahili vizuri zaidi kuliko sisi. Kutokana na uzito wa hoja hiyo, ndiyo maana ninapenda kuchangia machache.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni Mdau Mkuu wa Matumizi ya Kiswahili katika Afrika. Ziko taarifa kwamba Watanzania ndio walioanzisha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Ghana, Chuo Kikuu cha Port Harcourt, Nigeria na Chuo Kikuu wa Sebha, Libya. Inawezekana upo ukweli pia kwamba leo hii wengi walioko katika Vyuo hivyo ni kutoka Kenya, Japo imekuwa vigumu kupata takwimu za ajira ya Walimu wanaofundisha katika nchi hizo kutokana na kwamba ajira iko katika Soko Huria. Hakuna chombo maalum kinachoratibu ajira za Walimu hao kwenye Vyuo Vikuu. Nina hakika hii ni moja ya sababu zilizofanya wachangiaji wengi kutumia "Uzoefu" zaidi katika kujenga hoja hiyo kwamba Walimu wengi wanatoka Kenya. Wakati sasa umefika wa kuwa na utaratibu mahsus wa upatikanaji wa Walimu wa Kiswahili wenye sifa za kufundisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameainisha upungufu mbalimbali ambao unachangia katika tofauti iliyopo kati yetu na jirani zetu wa Kenya. Pamoja na upungufu huo, bado Tanzania imekuwa kitovu cha lugha ya Kiswahili duniani. Walimu wa Kiswahili nchini Ujeruman, Hamburg, Berlin, Colon, Leipzig na Chuo cha INALCO Ufaransa, walifundishwa na Walimu kutoka Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI) Zanzibar na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mwalimu wa siku nyingi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha London (*School of Oriental African Studies - SOAS*) anatoka Tanzania, Prof. Farouk Topan ambaye ndiye alikuwa Mkuu wa kwanza wa Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Walimu wa Kiswahili hadi sasa

kule Korea, katika Chuo Kikuu cha Hankuk wanatoka Tanzania. Walimu wa Osaka, Japan walitoka Tanzania katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, yapo mahitaji makubwa ya lugha ya Kiswahili kwa sasa. Katika Afrika ya Mashariki peke yake, Uganda wanahitaji Walimu zaidi ya 10 kwa ajili ya Vyuo vyao Vikuu. Vilevile, wanataka Walimu katika Shule za Sekondari. Rwanda na Burundi wanahitaji Walimu na Jamhuri ya Watu wa Kongo (DRC) wanahitaji Walimu kwa ajili ya Vyuo vyao vya Lubumbashi na Kalemie; DRC wanahitaji pia vitabu vya Kiswahili Sanifu.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya Kiswahili yako katika nchi nyingi. Chuo Kikuu cha Kwazulu, Natali, Afrika ya Kusini kimeanzisha masomo ya BA Kiswahili. Hivyo, watahitaji Walimu. Chuo Kikuu cha Zimbabwe kinahitaji Walimu wa Kiswahili. Namibia wameombwa Walimu kuanzisha Kiswahili katika Chuo chao Kikuu. Jamaica Wanahitaji Walimu wa kuanzisha masomo ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha West Indies. Baadhi ya Vyuo Vikuu vya Marekani kikiwemo Chuo Kikuu cha Lugha cha Monterey, California wanahitaji Walimu wa Kiswahili. Hapa Nchini Vyuo Vikuu zaidi ya 20 kando ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vimeanzisha masomo ya Kiswahili na vitahitaji Walimu wenye Shahada za Uzamili na Uzamivu katika Kiswahili. Hivyo, mahitaji ni makubwa kipita kiasi na hivyo hii ni fursa kubwa kwa Watanzania wenye sifa kujipatia ajira.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Desemba, 2005, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akifungua rasmi Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema na nanukuu: "Lugha ya Kiswahili imeanza kupata umaarufu Afrika na Duniani. Umoja wa Afrika umekubali Kiswahili kuwa moja ya lugha zake kuu. Aidha, Nchi za Kanda ya Maziwa Makuu zimekubali kutumia na kuendeleza Kiswahili. Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha kuwa juhudhi hizi zinaendelezwa na kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inakua nje ya mipaka ya Afrika." Mwisho wa Kunukuu.

Kwa maneno haya ya Mheshimiwa Rais, ni dhahiri kwamba, Serikali inajali umuhimu wa kuendeleza lugha ya Kiswahili, kwa vile ina nafasi nzuri ya kupanuka na kushiriki katika ujenzi wa jamii ya Watanzania na Jamii mpya ya Afrika ya Mashariki na hata duniani kote.

Mheshimiwa Spika, tunayo changamoto ya kukifanya Kiswahili kiwe lugha ya dunia. Lakini pia tunalo jukumu la kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inafundishwa na kutumika Mashulen, ikiwa ni pamoja na Shule za Msingi, na kwamba inafundishwa katika Shule za Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu. Aidha, tunahitaji kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inatumika vizuri na kwa ufasaha katika Shughuli za Serikali hapa Bungeni, katika Mahakamani na maeneo mengine kwa faida ya wananchi wetu na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo, pamoja na msisitizo huo, yapo maeneo ambayo tunahitaji kuyafanya kazi zaidi. (Makofsi)

Kwa mfano, kwanza, bado kuna maeneo mengi yanayohusu taaluma ya Kiswahili ambayo hayajafanyiwa utafiti wa lugha. Utafiti ndiyo uhai wa taaluma na chimbuko la maarifa mapya. Ni kazi ya Wanataalam wa Kiswahili kufanya tafiti za kina ambazo zitakifanya Kiswahili kitumiwe Kimatalfa.

Pili, Vyuo Vikuu vilivyoanzishwa, pamoja na kuweza kufundisha somo la Kiswahili kwa Wanachuo wa Shahada ya Kwanza, bado havina Wahadhiri wa kutosha wa kufundisha mafunzo ya Uzamili na Uzamivu. Tunalo jukumu la Kuanzisha Programu za Shahada za Uzamili na Uzamivu zitakazokidhi mahitaji makubwa ya uhaba wa Wataalamu wa Kiswahili ndani na nje ya nchi.

Tatu, hapa nchini hakuna Chuo Kikuu kinachotoa mafunzo ya Ukalimani. Watu wanaohitaji stadi hii ya ukalimani wanalahazimika kwenda kusomea katika Vyuo Vikuu vya Nje ya

Afrika Mashariki. Mimi najiuliza, hivi hili nalo tunalikubali wakati lugha ni yetu? Ninaamini tunao uwezo wa kutumia Vyuo Vikuu na Vyuo vingine tulivyonavyo kufanya kazi hii ya kufundisha Wakalimani. Hivyo, ni vizuri Vyuo vyetu nchini vianzishe Idara za Mafunzo ya Ukalimani ili kupunguza tatizo hilo. (Makofi)

Nne, imebainika pia kwamba hata kama kukiwepo na Wakalimani, bado hakuna Kumbi za kisasa zenyen vifaa nya kusikilizia tafsiri za lugha mbalimbali. Kumbi nyengi tunazofanya Mikutano tukiacha Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha (AICC) hazina vifaa hivyo. Changamoto tulionayo kama nchi na hasa Wawekezaji wa Kumbi za Mikutano ni kuhakikisha Kumbi zinazojengwa na zilizopo zinakuwa na vifaa nya kutoa huduma ya Ukalimani. Lengo ni kutumia fursa hiyo katika kukuza lugha yetu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, wakati mwininge napata shida sana kuona Warsha yenye wageni wasiozidi 10 na Waswahili 200 inaendeshwa kwa lugha ya Kiingereza, tena bila kujali kama Waswahili hao wanaelewa Kiingereza au la. Wanachojali ni kuwafurahisha wageni wachache. Kwa maoni yangu, hii ni kasumba isiyo na maelezo. (Makofi)

Changamoto iliyopo mbele yetu ni kuondoa kasumba hii kwa kupenda kutumia lugha yetu ya Kiswahili wakati wote. Tuondoe wasiwasi katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Tumeshuhudia Kiswahili kikikuzwa na kutandazwa katika mifumo ya Kompyuta ya Linux na Microsoft. Tumesikia pia kwamba, kama njia mojawapo ya kuboresha matumizi ya Kiswahili sanifu, tayari wataalamu wa lugha kwa kushirikiana na wataalamu wa Kompyuta wameweza kutengeneza Programu Maalum ya Kisahihishi cha Lugha ya Kiswahili katika Kompyuta ambayo inatumia kusahihisha maneno ya Kiswahili. Haya ni maendeleo makubwa yaliyofikiwa ya kukiingiza Kiswahili katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Duniani.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba lugha ya Kiswahili imekua sana. Wote ni mashahidi kwamba Mashirika makubwa ya Utangazaji Duniani yanatangaza Kiswahili. Tunajua sana Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), Sauti ya America, Redio ya Ujerumani Deutsche -Well na Radio France International; wako pia Al-Jazeera, Radio Vatican, Radio Japan na Redio ya Umoja wa Mataifa. Aidha, ziko nchi zenyen Vituo nya Redio vinavyotangaza kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, China, India, Syria, Misri, Sudan, kwa kutaja chache. Hii pia ni ishara kwamba Kiswahili kinakua kwa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kuongea mengi ya nadharia kuhusu lugha yetu nzuri ya Kiswahili kwa muda mrefu. Tunatakiwa sasa tuanze kutekeleza hayo mengi kwa vitendo. Naomba kuhimiza basi Taasisi mbalimbali nchini, ziweke juhudhi zote katika kukuza lugha ya Kiswahili ili iweze kutumika katika nyanja zote za mawasiliano ikiwemo Sayansi na Teknolojia. Vilevile, natoa rai kwa Watanzania wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kujitahidi kila tunapozungumza Kiswahili kuepuka kuchanganya na maneno ya lugha ya Kiingereza kwenye mazungumzo yetu. (Makofi)

Baadhi yetu tunamkumbuka Mwandishi na Mshairi wa Riwaya Bwana Shaban Robert (1909 – 1962) ambaye aliandika kuhusu lugha ya Kiswahili na kukifananisha na ladha ya Titi la Mama. Katika moja ya Mshairi yake, aliandika na nanukuu:-

*"Titi la Mama litamu, hata likiwa la Mbwa,  
Kiswahili naazimu, sifayo iliyofumbwa,  
Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo Kubwa,  
Toka kama mlizamu, funika palipozibwa,  
Titi la Mama litamu, jingine halishi hamu.*

*Lugha yangu ya utoto, hata sasa nimekua,  
 Tangu ulimi mzito, sasa kusema najua,  
 Ni sawa na manukato, moyoni mwangu na pua,  
 Pori bahari na mto, napita ikitumia, Titi la Mama litamu,  
 jingine halishi hamu".*

Mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Anachosema Bwana Shaaban Robert, ni kuonesha thamani ya Kiswahili jinsi kilivyo na utamu wa aina yake katika matumizi. Historia ya Shaaban Robert, tunaambwa alithubutu kulikataa kabile lake la Kiyao na kijiita Mswahili kuonesha jinsi alivyokipenda Kiswahili. Nasi tujivunie Kiswahili, tukipende, tukitumile, tukienzi na tukithamini. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumechangia katika kuendeleza lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Watanzania sasa siyo wakati wa kulalamikiana wala kulaumiana juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili, bali sasa tushirikiane kujenga lugha yetu ya Kiswahili. Njia iko wazi, nadhani kazi sasa ni kwetu! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kuhusu kuanzishwa kwa huduma ya Usafiri wa reli jijini Dar es Salaam. Huduma ya usafiri wa njia ya reli Jijini Dar es Salaam ni mojawapo ya hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kupunguza tatizo la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Mwezi Agosti, 2012 wakati Waziri wa Uchukuzi alipokuwa anasoma Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, alilieleza Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yake inakusudia kuanza kutoa huduma ya usafiri wa njia ya reli kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari barabarani katika Jiji la Dar es Salaam kuanzia mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2012.

Ili kufanikisha lengo hilo, Wizara ilichukua hatua za maandalizi kwa kukarabati na kuweka miundombinu muhimu ya kuwezesha kuanza kwa usafiri katika njia za reli zifuatazo:-

(i) Reli ya TAZARA kati ya Vituo vya Kurasini kuitia Stesheni ya TAZARA, Dar es Salaam hadi Pugu Mwakanga (Km. 24.5); na

(ii) Reli ya Kampuni ya Reli (TRL) kutoka Ubungo Maziwa kuitia Tabata-Relini, Tabata – Matumbi na Buguruni – Mnyamani hadi Katikati ya Jiji (Km.12).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Reli ya TAZARA, miundombinu ya reli hii haikuhitaji matengenezo makubwa. Hata hivyo, ukarabati mkubwa ulifanywa wa mabehewa saba na vichwa viwili vya treni. Pia maboresho yalifanywa na yanaendelea kufanywa ya ujenzi wa vituo na sehemu zilizoinuliwa kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria pamoja na vibanda vya kukatia tiketi. Hivyo, usafiri wa Treni ya TAZARA umekuwa wa msaada mkubwa na wa haraka kwa wakazi wa Dar es Salaam waishio karibu na reli hiyo hadi Pugu Mwakanga na Kurasini. Wastani wa abiria 6,000 hutumia huduma ya reli hii kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika reli ya Kampuni ya Reli (TRL), kazi ya ukarabati wa miundombinu ilihusisha:-

(i) Ukarabati wa Reli yenye na ujenzi wa sehemu zilizoinuliwa kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria (*platforms*);

(ii) Ujenzi wa vibanda vya kukatia tiketi na vibanda vya wasafiri kusubiria treni;

- (iii) Ujenzi wa Stesheni ya Buguruni kwa Mnyamani pamoja na eneo la kupishania treni;
- (iv) Ujenzi wa Stesheni ya Ubungo pamoja na sehemu ya kugeuzia treni;
- (v) Kuweka mfumo wa mawasiliano ya uendeshaji treni;
- (vi) Ujenzi wa vyoo kwenye stesheni za Dar es Salaam na Ubungo;
- (vii) Ujenzi wa Vivuko vya Barabara na Reli (*Level Crossings*) na vibanda vya Walinzi wa Vivuko hivyo (*level crossing attendants*); na
- (viii) Ukarabati wa Mabehewa 14 na injini tatu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2012, ukarabati wa miundombinu hiyo ulikuwa umekamilika kwa kiasi kikubwa na hivyo kuwezesha treni moja tu kuanza kufanya safari. Hivyo, ukarabati bado unaendelea ili kuwezesha treni mbili kufanya kazi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa yamepatikana kutokana na kuanza kwa huduma hii. Tangu huduma hii ianze kutolewa tarehe 29 Oktoba, 2012, imepata mwitikio mkubwa kutoka kwa wakazi wa Dar es Salaam. Hivi sasa huduma inatolewa kwa kutumia Treni moja yenye mabehewa sita yenye uwezo wa kubeba abiria 600 kwa safari moja. Siku za huduma hii ni kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi isipokua siku za Jumapili na Sikukuu. Aidha, Treni hii hufanya safari mara sita kwa siku, yaani safari tatu asubuhi na jioni sawia. Safari huanza saa 12.00 hadi saa 5.00 Asubuhi kutoka Stesheni ya Ubungo Maziwa hadi Stesheni ya Dar es Salaam na kusimama hadi saa 9.40 alasiri ambapo huanza tena hadi saa 2.00 usiku. Muda wa safari ni takribani nusu saa hadi dakika 40. Inatarajiwa kwamba usafiri huu utakuwa na ubora zaidi hapo ujenzi wa miundombinu muhimu itakapokamilika kuruhusu treni mbili kupishana na kuwezesha kichwa cha treni kugeuza katika Stesheni ya Ubungo Maziwa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mradi huu unashabihiana kihuduma na Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (*DART*) utakapoanza huduma ya Mabasi yake. Uhusiano huo unatokana na Vituo vingine vya Treni kuwa karibu na Vituo vya *DART* na hivyo kuwezesha Miradi hii miwili kutoa huduma ya usafiri wa Abiria kwa ukamilifu zaidi.

Napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe - Waziri wa Uchukuzi na timu yake katika Wizara pamoja na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Uchukuzi, hasa Kampuni ya TRL, TAZARA, RAHCO na SUMATRA kwa kuwezesha kuanza kwa usafiri huu. Mmefanya kazi nzuri ingawa najua bado kuna changamoto nyingi. Nawaomba msiridhike na mafanikio hayo, kwani mafanikio hayo yameibua pia changamoto nyingi ambazo mnapaswa kukabiliana nazo kikamilifu ili huduma hii iwe endelevu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wananchi wanaotembea kwa miguu katika njia za reli na wengine wanaotumia njia za reli kama sehemu za kufanya biashara ndogo ndogo kuacha kufanya hivyo. Watambue kwamba matumizi ya njia ya reli ni kwa ajili ya treni na kwa hiyo, waone umuhimu wa kulinda usalama wao na wa abiria wa treni. Pia waepuke kuzalisha takataka zinazochafua mazingira katika njia za reli, Vituo vya Treni na kuziba mifereji ya kupitishia maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 hadi 18 Septemba, 2012 nilifanya Ziara ya Kikazi katika Mikoa ya Shinyanga (Kahama), Geita na Mwanza. Madhumuni ya ziara hiyo yalikuwa ni kuona

fursa za maendeleo zilizopo katika Mikoa hiyo na jinsi zinavyoweza kutumiwa kwa ajili ya maendeleo ya Wakazi wa Mikoa hiyo na kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Aidha, nilitaka kuona jinsi Mikoa hiyo na Wilaya zake inavyotekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi, MKUKUTA II, na Malengo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa na katika kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara yangu hiyo, yapo masuala muhimu yaliyojitokeza, na ambayo nimeona ni vyema kuyawekea msisitizo. Kwa mfano, nikiwa Wilayani Kahama, Mkao wa Shinyanga na Wilaya ya Geita katika Mkoaa Mpya wa Geita, nilipokea maombi kutoka kwa vijana wengi wa maeneo hayo wakitaka wapatiwe ajira Migodini. Hata hivyo, changamoto kubwa inayowakabili vijana hao ni ukosefu wa ujuzi na stadi stahiki katika Sekta ya Madini. Hali hiyo imesababisha nafasi za ajira kuchukuliwa na vijana kutoka nje ya Mikoa hiyo na vijana wa maeneo hayo kukosa ajira katika Migodi iliyoko kwenye Mikoa yao. Kwa ujumla kukosekana kwa ujuzi na stadi kumetokana na kutokuwa na Vyuo au Taasisi zinazotoa mafunzo kuhusu usimamizi au uchanguaji na uongezaji thamani katika madini yanayotoka katika Migodi hiyo. Aidha, Vyuo vya VETA vya Shinyanga na Mwanza havina kozi stahiki kuhusu madini.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto hiyo, niliviagiza Vyuo vyote vya VETA katika Mikoa hiyo vianzishe utaratibu wa kuwa na Kozi fupi na ndefu zitakazowajengea uwezo vijana katika masuala ya madini ili waweze kupata fursa ya kuajiriwa katika Migodi hiyo au kujajiri wenyewe. Aidha, kama suluhisho la muda mrefu, Serikali tutaendelea kutoa msukumo kuhakikisha kuwa Vyuo vya VETA vinakuwa na mitaala maalum kuhusu masuala ya madini hasa katika maeneo ya Kanda ya Ziwa. Kwa mantiki hiyo, napenda kutoa wito kwa Uongozi wa Vyuo vya VETA Nchini kuanzisha kozi maalum zitakazosaidia vijana kuajiriwa au kujajiri katika maeneo maalum kulingana na fursa zilizopo katika maeneo yao kama vile madini kwa sehemu zenye madini na Uvubi wa Kisasa. Kwa kufanya hivyo, tutasaidia sana vijana wetu kupata ajira na hata kujajiri kutokana na fursa zilizopo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo pia nilibaini kuwa bado tunahitaji kuongeza bidii katika kuwawezesha wananchi kuongeza matumizi ya zana bora za kilimo hususan matrekta makubwa na madogo. Bado wananchi kiasi cha asilimia 70 wanategemea jembe la mkono.

Hata hivyo, ni wazi kuwa kilimo cha jembe la mkono kamwe hakiwezi kumfanya mkulima kupata mazao zaidi ili aweze kujipatia chakula cha kutosha na ziada ambayo anaweza kuuza na kuinua kipato chake. Ni jukumu letu kumsaidia mwananchi ili aondokane na hali ya kutegemea dhana duni za kilimo ikiwemo jembe la mkono. Hivyo, naziagiza Halmashauri zote nchini ziwasaidie wananchi kuunda Vikundi vya Uzalishaji na kuwawezesha kupata matrekta ili kukuza kilimo na kuongeza uzalishaji. Pamoja na mpango huo, kila Halmashauri inapaswa ihakikisha matrekta hayo yanapatikana na yanakopeshwa kwa wananchi kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na jitihada za kuagiza matrekta zaidi kwa lengo la kuwafikishia wananchi wote nchini. Hivi sasa Serikali inazungumza na Serikali ya India ili kupata tena matrekta 3,000 kupitia SUMA JKT kutoka nchini India baada ya matrekta ya awali kununuliwa yote kutokana na uamuzi wa Serikali wa kuyapunguza bei na ubora wake.

Nashauri Uongozi wa Mikoa kuchangamkia fursa hiyo mapema, kwani kwa mwenendo huu, matrekta hayo yanaweza pia kwisha mapema kutokana na mwamko mkubwa ambaio wananchi wameupata. Aidha, nawaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kufuatilia kwa karibu matumizi ya matrekta hayo, kwani lengo ni kuongeza tija na uzalishaji katika Kilimo cha Mazao. Haitakuwa na maana kwa Mkoaa au Halmashauri yoyote kuwa na matrekta mengi wakati hayatumiki kwa shughuli za kumwondolea mwananchi Umaskini. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa ili kumkomboa mwananchi, sharti kuwe na mikakati ya kumwezesha Mkulima kuwa na kilimo cha uhakika kisichotegemea misimu ya mvua. Hata hivyo, katika ziara yangu nilibaini kuwa maeneo mengi yanayofaa kwa ajili ya Kilimo cha Umwagiliaji hayatumiki ipasavyo. Kilimo cha Umwagiliaji kina nafasi muhimu ya kuwaleta wananchi maendeleo. Hivyo, naziagiza Halmashauri zote nchini hasa zile za Kanda ya Ziwa kuandaa na kutekeleza Programu za Umwagiliaji kwa kutengeneza Skimu za Umwagiliaji ili ziweze kufikia angalau nusu ya eneo linalofaa kwa Umwagiliaji. Siyo lazima kuanza na teknolojia ya hali ya juu na ambayo ni ghali. Tunaweza kuanza na teknolojia rahisi na za bei nafuu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika ziara yangu niliweza pia kuzindua Miradi ya Wawekezaji Wazalendo ukiwemo Mradi wa Kilimo cha Mboga katika Kampuni ya Ngongoseke Horticulture Farm - Kijiji cha Nsola, Wilaya ya Magu na Mradi wa Supermarket ya Kimataifa Mjini Kahama. Nimefarijika sana kuona jithada hizi kubwa zinazofanywa na Watanzania wenzetu na wananchi wazawa katika kuwekeza katika maeneo ya nyumbani kwao. Huu ni mfano mzuri unaopaswa kuigwa na watanzania wengine wanaoishi nje ya Mikoa au Wilaya zao kwa kuwekeza miradi ya maendeleo katika maeneo wanakotoka. Jambo la kutia moyo zaidi, katika miradi hiyo ni kuzalishwa kwa ajira nyingi kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, katika ziara yangu pia nilipokea malalamiko ya wananchi wakitaka kujuu kwa nini zao la Pamba kwa msimu wa mwaka 2011/2012 ilikuwa na bei ya chini kuliko msimu uliopita na pia chini ya matarajio yao? Nilitumia muda mwingi kufafanua jambo hili kwa maelezo ya aina mbalimbali. Hata hivyo, napenda kutumia Bunge hili kutoa tena ufanuzi kuhusu bei ya Pamba.

Mheshimiwa Spika, kimsingi bei ya pamba niliwaeleza inapangwa na Soko la Dunia. Hata hivyo, katika msimu wa mwaka 2011 bei ya pamba ilikuwa juu ambapo hapa nchini, ilifikia Sh. 1,100/= . Kupanda kwa bei hiyo kulisababishwa na uhitaji mkubwa wa Pamba duniani na kutokana kwamba nchi zinazozalisha Pamba kwa wingi duniani hazikuweza kuzalisha kwa sababu ya mafuriko. Katika msimu wa mwaka 2012, nchi hizo hazikukumbwa na mafuriko na zimezalisha Pamba kwa wingi na hivyo dunia kuwa na ugavi (supply) mkubwa wa Pamba ikilinganishwa na mahitaji (demand) na hivyo bei kushuka. Kimsingi, bei halisi ya Pamba ilikuwa Sh. 420/= kwa kilo, lakini baada ya Serikali kuingilia katika ilipandisha bei hadi kufikia Sh. 660/= kwa kilo.

Kwa hiyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa makali ya madhara ya kuyumba kwa bei ya Pamba duniani yanadhibitiwa. Moja ya hatua hizo ni kuuza Pamba inayolimwa hapa nchini katika Soko la ndani, lengo likiwa ni kuboresha viwanda vya ndani vya nguo na pia kumpatia mkulima uhakika wa soko kwa mazao yake.

Kama mnavyokumbuka, katika Mkutano wa Bunge uliopita tuliwaeleza kuwa Serikali imeridhia kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Viwanda vya Nguo Nchini ili viweze kuongeza uzalishaji wa nguo kama vile kanga, vitenge, sare kwa wanafunzi na kadhalika na kupunguza bei za nguo zinazozalishwa na viwanda hivyo ili kumnufaisha mwananchi.

Naomba kutoa wito kwa Viwanda vya Nguo Nchini kuona uwezekano wa kuzalisha Sare (Uniforms) mbalimbali zinazotumiwa nchini zikiwemo sare za shule pamoja na Sare za Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kutumia Pamba tunayozalisha. Hali hii itaongeza matumizi na bei ya Pamba tunayozalisha na kumnufaisha mkulima badala ya kutegemea bei ya Pamba katika Soko la Dunia ambayo haina uhakika.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Victoria ni rasilimali ambayo inatosha kabisa kuipandisha kiuchumi Mikoa inayozunguka Ziwa hilo pamoja na wananchi wake kutoka kwenye umaskini.

Ziwa hili lina jumla ya Kilomita za Mraba 68,800. Kati ya hizo, Kilomita za mraba 35,088, sawa na asilimia 51 ya ukubwa wa Ziwa lote zipo Tanzania. Kilomita za Mraba 29,584, sawa na asilimia 43 zipo Uganda, na Kilomita za mraba 4,128, sawa na asilimia 6 zipo Kenya.

Ziwa Viktoria ni fursa kubwa kwa wananchi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa katika Sekta ya Kilimo cha Umwagiliaji, Uvuvi na Utalii na lina nafasi kubwa ya kuongeza kipato cha wananchi. Pamoja na fursa zilizopo katika Ziwa hilo, bado hazijaweza kutumika ipasavyo.

Vilevile, zipo Changamoto nyingi zinazojitokeza. Changamoto hizo ni pamoja na kupungua kwa kiasi cha samaki kunakotokana na kutozingatiwa kwa Kanuni bora za Uvuvi. Takwimu zinaonesha kuwa uvuvi haramu unaongezeka siku hadi siku. Uvuvi haramu una athari kubwa kwa masalia ya samaki na ukuaji wake na unaharibu uwiano kati ya ukuaji wa samaki na uvunaji wake. Uvuaji wa samaki wachanga, matokeo yake ni kupungua kwa samaki kwa kasi kubwa.

Napenda kuwakumbusha kuwa, utafiti uliofanywa na Shirika la Chakula Duniani (FAO) unaonesha kuwa kwenye Ziwa Victoria, samaki aina ya Sangara wamepungua kwa asilimia 60 hadi kufikia mwaka 1999; asilimia 32 katika kipindi cha mwaka 1999 hadi 2007; na asilimia 16 kipindi cha mwaka 2007 hadi 2009.

Naomba nitoe rai kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa kuwa, utajiri wa Samaki uliopo leo katika Ziwa hili, siyo wa kudumu iwapo wataendelea na uvuvi haramu. Rasilimali hii ni ya kutunzwa ili fursa hii iweze kutumika na kizazi hiki na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali katika Sekta ya Mifugo ni kutaka kuondokana na kuchunga mifugo mingi isiyokuwa na tija na ambayo haiendani na eneo la ardhi inayotosheleza kwa malisho ili pia kuepuka uharibifu wa mazingira. Nikiwa katika ziara wa Mikoa hiyo, nilibaini kuwa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kama ilivyo Mikoa mingine nchini, kuna mifugo mingi ambayo haiendani na uwezo wa malisho (*Carrying Capacity*). Kwa takwimu za Kitaifa inashauriwa kuwa ng'ombe mmoja hutumia Ha 4.03 za malisho kwa mwaka.

Naomba kutoa wito kwa wafugaji kutumia mifugo mingi walionayo kama fursa ya kumnumfaisha mfugaji na kumwingizia kipato, kwa kuuza na kubakiza kiasi ambacho kinaendana na eneo liliopo. Nawahimiza wachukulie mifugo kuwa ni shughuli ya kuwaondolea umaskini na waachane na mazoea ya kuwa na makundi makubwa ya mifugo yenye tija ndogo.

Natoa wito kwa Viongozi wa Mikoa na Wilaya kuwaelimisha wananchi kuhusu suala hili. Aidha, Halmashauri zote ziwasimamie kikamilifu Watumishi wa Sekta ya Mifugo ili watekeleze majukumu yao ipasavyo kwa kufungua Mashamba Darasa ya Mifugo ya kuwaelimisha wafugaji.

Mheshimiwa Spika, upo umuhimu wa kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi na kutenga maeneo maalum ya malisho ya mifugo. Katika maeneo hayo, lazima kuzingatia uwiano baina ya ardhi na idadi ya mifugo iliyopo. Aidha, maeneo hayo yawekewe miundombinu muhimu ya kufugia ikiwemo malambo, majosho, na kadhalika. Kwa kufanya hivyo, tutaeppuka migogoro mingi inayojitokeza kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, nilishawahi kuliarifu Bunge lako Tukufu juu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuijunga rasmi na Mpango wa Uendeshaji Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership – OGP) tarehe 21 Septemba, 2011. Uamuzi wa kuijunga na mpango huo ulilenga katika kuimarisha utekelezaji wa mipango mingine ya maboresho

ambayo Serikali inayatekeleza na faida ambazo mpango huu utatuletea kama tukiutekeleza kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, mpango huu unajikita katika maeneo makuu manne ambayo ni: Moja, Kuweka Uwazi zaidi katika uendeshaji wa shughuli za Serikali; pili, Ushirikishwaji wa wananchi katika kuweka mipango na utekelezaji wa shughuli za Serikali; tatu, kuimarisha uwajibikaji katika utendaji na kuimarisha juhudzi za kuzuia na kupambana na rushwa; na nne, kuweka umuhimu wa matumizi ya teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeamua kutekeleza Mpango wa OGP katika Sekta tatu za huduma za Jamii ambazo ni Afya, Maji na Elimu. Pamoja na Mpango kujielekeza kwenye Sekta hizo, pia umejikita katika maeneo ya uwazi, ushirikishwaji wa wananchi, uwajibikaji na uadilifu, na teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vilivyopo kwenye Mpango huu vitatekelezwa na Wizara na Taasisi za Serikali kwa kutumia rasilimali zinazosimamiwa na Makatibu Wakuu. Sekta zinazohusika moja kwa moja na utekelezaji zitaweka kwenye Bajeti na Mipango yao, utekelezaji wa Mpango wa OGP. Wizara husika zimeandaa Mpango Mkakati wa Utekelezaji unaoainisha muda wa kutekeleza, wahuksika (watakaoteketeleza) na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, tayari Kamati ya Kitaifa imeshaandaa Roadmap ya shughuli zitakazoteketeleza hadi kufikia Juni, 2012 ukionesha Commitments za kila Sekta. Mpango Kazi umeainisha shughuli zitakazoteketeleza, viashiria, muda na bajeti za utekelezaji. Sekta zimeandaa pia Mpango Kazi na kuziwasilisha kwenye Kamati. Asasi zote Zisizo za Kiserikali zilizo elekezwa kuandaa Mipango Kazi bado hazijatekelezwa kufanya hivyo. Tunaendelea kuwakumbusha.

Mheshimiwa Spika, Taarifa za utekelezaji wa Mpango huu za Robo Mwaka ya Kwanza (Julai – Septemba, 2012) zimeanza kupokelewa kutoka katika Sekta za Utekelezaji. Tumeweza kuandaa Mkakati wa Mawasiliano kuhusu utekelezaji wa Mpango wa OGP Tanzania (OGP Communication Strategy) kwa ajili ya kutangaza zaidi kwa wananchi Mpango huu. Pia Kamati inashirikiana kwa karibu na Wakala wa Serikali Mtando (e-Government Agency) kuhakikisha Tovuti ya Wananchi (Citizen portal) inaanza kazi mapema iwezekanavyo ili itoe huduma na maelekezo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, toka tuijunge na tulipoanza utekelezaji wa Mpango Kazi wetu, tumepata changamoto mbalimbali. Bado wananchi wana uelewa mdogo kuhusu Mpango wa OGP. Hivyo kuna haja ya kuutangaza zaidi Mpango huu. Aidha, taarifa kuhusu Mpango wa OGP ilichelewa kufika katika Sekta zinazoteketeza Mpango huu. Kutokana na hali hiyo, Wizara hazikuweza kuijandaa vya kutosha na hivyo baadhi ya Wizara na Taasisi kushindwa kutenga fedha za kutosha za kutekeleza Mpango wa OGP. Kiasi kidogo cha fedha zilizotengewa kwa baadhi ya Sekta hazikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, Serikali imejipanga kutekeleza Mpango huo, kwani una manufaa kwa nchi yetu. Tunapenda kutoa shukrani zetu kwa wadau wote na wananchi kwa ujumla kwa kutoa maoni yao wakati wa kuandaa Mpango Kazi wetu. Tutaendelea kushirikiana na wadau wote katika kuhakikisha utekelezaji wa Mpango Kazi huu. Aidha, tunatoa wito kwa Taasisi zote za Kiserikali, Wizara na Asasi Zisizo za Kiserikali ambazo zinatekeleza Mpango Kazi huu kuutekeleza kikamilifu ili kuleta faida ambazo zinaletwa na utekelezaji wa vipaumbele tulivyojiweka.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 12 Juni, 2011 nilikutana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani na Naibu Waziri Mkuu wa Ireland ambapo niliahidi kwamba Serikali itatekeleza azma yake katika kupambana na tatizo la lishe nchini. Aidha, mwezi Septemba, 2011 Mkakati wa Taifa wa Lishe Ulizinduliwa rasmi.

Katika kutekeleza ahadi hiyo, Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Lishe wa mwaka 2011/2012 - 2015/2016, umeandaliwa na sasa uko kwenye hatua ya mwisho ya kukamilishwa. Mpango huo umeainisha kwa kina kazi zitakazofanyika katika miaka mitano ijayo ikiwa ni pamoja na kuandaliwa Bajeti ya Utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Bajeti wa mwaka 2012/2013 umetoa maelekezo maalum ya msisitizo kwa Sekta husika na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa kipaumbele katika suala la lishe. Aidha, Wizara ya Fedha imeanzisha kasma maalum ya lishe ili Wizara zinazohusika na masuala ya lishe zianze kukasimia fedha kwa ajili ya shughuli za lishe.

Hata hivyo, imebainika kwamba katika mwaka huu wa fedha (2012/2013), Wizara na Halmashauri nyingi hazikutenga fedha za lishe kwa kutumia kasma zilizoanzishwa. Napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba katika Bajeti ya mwaka 2013/2014, tutaendelea kufuatilia ili fedha zaidi za Mpango huu zitengwe kwa kutumia kasma zilizoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mkakati huu unakwenda vizuri kama ilivyopangwa, Halmashauri zote zimeanzisha Madawati ya Lishe na Maafisa husika walipewa Semina Elekezi ya jinsi ya kupanga na kubajeti masuala ya lishe. Katika mchakato huo, Halmashauri zote za Mikoa 19 kati ya Mikoa 25 zimeanzisha Kamati za Kuratibu Lishe. Aidha, Wizara zinazohusika na utekelezaji wa masuala ya lishe, moja kwa moja zimetuea Wataalam watakaoratibu masuala hayo kwenye Wizara zao. Wizara zinazohusika ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maji, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Tume ya Mipango.

Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Halmashauri 106 kati ya 168 na Mikoa 14 kati ya 25 tayari zimeajiri Maafisa Lishe ambao watakuwa kiungo muhimu katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Lishe Nchini. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia Kanuni za kuweka virutubisho kwenye chakula (Food Fortification) zilizotangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali mwezi Julai, 2011, na kuanza kutekelezwa na wafanyabiashara na katika Halmashauri za Mikoa iliyokabiliwa na Utapiamlo mkali kwa lengo la kuboresha lishe nchini. Tutaendelea kusimamia utekelezaji wa azma ya Serikali ya kupambana na tatizo la lishe nchini kama ambavyo tumedhamiria. Nitoe Wito kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa azma ya Serikali kuhusu kupambana na tatizo la lishe inatekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, katika miezi ya Septemba na Oktoba, 2012, nchi yetu ilikumbwa na machafuko yallyosababishwa na baadhi ya wananchi kufanya maandamano na vurugu kwa visingizio vya imani za dini na masuala ya siasa, maandamano ambayo kimsingi hayakuwa na vibali vya Mamlaka husika. Kama tunavyoolewa, kabla ya kufanya maandamano yoyote na Mikutano ya hadhara, ni lazima wahusika watoe taarifa Polisi ambao ndio Mamlaka iliyopewa jukumu la kuruhusu au kuzuia kufanyika kwa Maandamano na Mikutano hiyo, lengo likiwa kuratibu masuala yote ya usalama wa wananchi na mali zao katika mikusanyiko ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, kufanyika kwa vurugu hizo kwa kiasi kikubwa kulisababishwa na wahusika kutokutii Mamlaka halali ambayo ni Jeshi la Polisi. Kwa mfano, kwa matukio yaliyotokea katika Mikoa ya Morogoro pamoja na Iringa, ni baada ya Polisi kukataza

Maandamano na Mikutano ya hadhara kutofanyika kutokana na kuwepo kwa zoezi la Sensa liliokuwa likiendelea kwa wakati huo.

Aidha, matukio mbalimbali huko Zanzibar na katika Jiji la Dar es Salaam kwa nyakati tofauti pamoja na mambo mengine yalishinikizwa na hisia za imani za kidini miongoni mwa waandamanaji. Nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi wote waelewe kuwa, nchi yetu inaendeshwa na Utawala wa Sheria. Hivyo, ni vyema tukazingatia na kutii Mamlaka zilizopo na amri zake. Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa wananchi wanapata madhara ikiwemo majeraha, upotevu wa mali na wengine kuwekwa ndani na wengine hata kupoteza maisha kwa kitendo tu cha kushindwa kutii Mamlaka za nchi, ikiwemo Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile hali hii ambayo imejitokeza inaonekana kushika kasi katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu, ninawahimiza Viongozi wenzangu wa Siasa, Viongozi wa Dini na Taasisi mbalimbali tushirikiane kuwaongoza wananchi kwa kuwaelimisha umuhimu wa Utii wa Sheria, Kanuni na Taratibu ili kudumisha amani na utulivu katika nchini yetu. Tukiwaelimisha tutasaidia kuwaepusha na madhara yanayoweza kutokea baada ya Mamlaka husika kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, mwenendo huu wa kutii Mamlaka unachangiwa pia kwa kiasi kikubwa na mmomonyoko wa maadili hasa kwa vijana wetu ambao bado tuna wajibu wa kuwaelimisha masuala mbalimbali, yakiwemo utii wa Sheria na Mamlaka za nchi. Kwa kuwa zoezi la kutoa elimu kwa Umma kuhusu utii wa Sheria ni shirikishi, napenda kutoa wito kwa Vyama vya Siasa, Madhehebu ya Dini, Wanahabari na Taasisi zisizokuwa za Serikali zishiriki kikamilifu katika uenezi wa Elimu ya Utii wa Sheria na Elimu ya Uraia kwa ujumla nchini.

Aidha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu haina budi sasa kuweka Programu mahususi ya Elimu ya Uraia Nchini katika Mitaala yake ili kujenga uzalendo na kukuza maadili kwa vijana wetu wa ngazi zote tukianza na Shule za Msingi, Sekondari hadi Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kila mtu ana uhuru wa kuabudu kama Katiba yetu inavyoelekeza. Wakati huo huo kila mtu ana wajibu wa kuheshimu dini na imani za watu wengine. Kufanya miyadhabara ya kukashifu dini nydingine ni makosa kwa mujibu wa Sheria zetu. Napenda kusisitiza tena kwamba, Serikali haitawavumilia watu ambao wanajaribu kuvuruga amani na usalama nchini. Aidha, itahakikisha wale wote wanaoleta uchochezi wa kujaribu, kuvuruga amani na utulivu nchini, wanachukuliwa hatua stahiki. Kwa vile, Jeshi la Polisi Nchini ni chombo muhimu katika ulinzi na usalama wa Raia na mali zao, nawahimiza wananchi wote wakiwemo Vyama vyote vya Siasa nchini na Taasisi za Dini kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutekeleza majukumu haya kwa faida yetu wote.

Mheshimiwa Spika, natoa tena wito kwa wananchi wote kuithamini amani tuliyonayo ambayo ni tunu tulivoachiwa na Waasisi wa Taifa hili. Ninawashi wananchi, Viongozi wa Kisiasa pamoja na Viongozi wa Dini kuilinda amani tuliyonayo kwa ustawi wa Taifa letu. Taifa hili halina nafasi ya udini wala ukabila wala ubaguzi wa alna yoyote ile. Napenda kusisitiza umuhimu wa wananchi kutii Sheria na kutimiza wajibu wao wa kutii Mamlaka za nchi, kwani hakuna haki isiyo na wajibu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, niruhusu niongelee jambo moja ambalo limejitokeza katika utaratibu wa Mfumo wa Malipo ya Fedha za Serikali kuititia Mtandao wa Malipo wa EPICOR-9. Hivi karibuni kumekuwa na taarifa za ucheleweshaji wa malipo mbalimbali kwa Watumishi wa Serikali na wale wa Taasisi na Sekta Binafsi wanaofanya kazi zinazolipiwa kuititia Hazina.

Sababu za ucheleweshaji huo zilitokana na kuzorota kwa Mfumo wa Malipo kulikosababisha kasi ndogo ya malipo mbalimbali ikiwemo mishahara hasa mwishoni mwa mwezi. Kwa sasa Mfumo huo umefanyiwa maboresho na kurudi katika hali ya kawaida. Hata hivyo, pamoja na juhudhi hizo, bado kuna changamoto kidogo ambazo zimejitokeza kama ifuatavyo:

(i) Katika kipindi cha siku mbili mfululizo, mfumo huo wa EPICOR uligoma kupeleka malipo ya Wizara ya Katiba na Sheria hasa Mahakama kwa sababu mbili: Kwanza, ni kutokana na kutokuwepo taarifa ya kutosha kutoka kwa watayarishaji; na Pili, kukosea katika uingizaji tarakimu kwa Kanuni ya Kiuhasibu yaani "inakotoka" na "inakokwenda" (Debit and Credit Principle). Tatizo hilo linarekebishwa na Wizara yenyewe kwa kushirikiana na Hazina.

(ii) Lakini pia kumekuwa na tatizo la tofauti ya kumbukumbu (records) za mishahara, hususan ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambazo ziko Utumishi na zile za komputa. Tofauti hizo zimesababisha ucheleweshaji wa malipo ya Watumishi wa Wizara hiyo, zikiwemo Posho za Askari wetu. Tatizo hili limeshughulikiwa kwa haraka na hakuna Mtumishi wa Wizara hiyo ambaye atakosa malipo yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashakikishia Watumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara nyingine na Wananchi wote kwa ujumla kwamba Mfumo huu umekwisha kuwa tulivu (*Stabilized*) baada ya kufanyiwa marekebisco. Aidha, wasidanganyike na taarifa za kupotosha kwamba mishahara yao imechukuliwa kwa ajili ya kulipia kazi nyingine sijui za Chama, za Serikali, siyo kweli! Napenda kuwashakikishia kwamba, taarifa hizo hazina ukweli wowote! Kwa sasa nawaomba wawe watulivu kwa vile tatizo la mtandao lillojitokeza limepatiwa ufumbuzi na naamini utakuwa ufumbuzi wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, mwisho na kama ilivyo ada, napenda niwashukuru wote waliofanikisha Mkutano huu wa Tisa wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa namna ya pekee kwa kutuongoza vizuri hadi tunapohitimisha siku ya leo. Namshukuru vilevile Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri waliyoifanya. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. Namshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake kwa huduma nzuri walizozitoa wakati wote tukiwa hapa. Nawashukuru Watumishi wa Serikali na Taasisi mbalimbali kwa michango yao. Nawashukuru Waandishi wa Vyombo vyta Habari kwa kuwashabarisha wananchi yote yaliyotokea katika Mkutano huu na kwa wakati. Wote kwa ujumla nasema, ahsanteni sana kwenu ninyi nyote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunakamilisha Mkutano wa Tisa wa Bunge lako Tukufu amba ni wa mwisho kufanyika kwa mwaka 2012. Mkutano wa Kumi utafanyika wakati ambapo tutakuwa tumeanza mwaka 2013. Nitumie fursa hii kumwomba Mwenyezi Mungu atupatie afya njema na kutufikisha salama mwisho wa mwaka tuweze kusherehekeea Sikukuu Njema ya Kristmas na Mwaka Mpya kwa amani na furaha! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawatakia safari njema na kuomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi Siku ya Jumanne tarehe 29 Januari, 2013 Saa 3.00 Asubuhi katika Ukumbi huu hapa Dodoma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono. Mimi pia napenda nimshukuru Waziri Mkuu kwa maneno mazito aliyojasema kututakia kheri ya mwaka mpya, lakini kama ilivyo ada mimi pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa ambao tumekuwa nao katika kipindi hiki. Kama nilivyoeleza katika taarifa yangu niliyosoma, dhana nzima ya uhuru wa Wabunge ni lazima tuwe na uadilifu wa hali ya juu.

Ni lazima tuwe tunaweza kufanya utafiti wa hali ya juu sana kuhusu mambo yetu tunayoyafanya kwa sababu sisi ni Wawakilishi Rasmi wa Wananchi, hakuna mwingine isipokuwa sisi. Nchi hii ina mihimilli yake mitatu na kila muhimilli una shughuli yake. Shughuli yetu sisi ni kuisimamia Serikali. Hata haya aliyojasema Mheshimiwa Waziri Mkuu mkipenda ni lazima myasimamie. Maana kasema maneno mengi mazuri, sasa nayo pia ni wajibu wetu kuyasimamia kama yanatakelezeka kweli.

Halafu ni lazima hata katika ngazi ya Kamati tusimamie kwa uadilifu. Waheshimiwa Wabunge kama uadilifu wa Bunge haupo, nchi imeshakufa. Kama uadilifu wa Bunge haupo nchi imeshakufa! Kwa hiyo ni mategemeo yangu kwamba kila mtu anapokwenda nyumbani, hilo limgone kwamba mimi ni sehemu ya kuua nchi kama sitatimiza wajibu kwa kadri inavyopaswa. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nalisema hili kwa dhati. Nchi yetu inatutegemea sisi. Mtu kusema kwa ukali ni sawa kama ana uhakika, kwani ubaya wake ni nini? Ila awe na uhakika na yale anayosema kwa sababu unawafanya Wabunge wenzako wakuamini, unafanya nchi ikuamini; lakini kama ni kweli kwanini usiseme hivyo? Hilo ndilo ninaloliomba.

Sasa katika kufanya hivyo, kuna wengine wana tabia ya kuudhika. Hakuna kuudhika humu ndani! Kila mtu ana kinga mtu. Zungumza kwa nguvu yako hata akikugusa uwe mvumilivu. Ukiondoka hapa msitengeneze hila kati yetu. Ni mtu ametimiza wajibu wake, katika mawazo yake kwa mujibu wa Katiba ibara ya 100. Tusiondoke na kisa kwamba fulani kanisema, hapana! Hivyo sivyo Wabunge wanavyofanya. Nawashukuru kwa kiwango kikubwa hilo siku hizi halipo. Mtasemana humu, mkiondoka mnashikana mkono, mnakunyuwa chai kama ipo na ndivyo inavyopaswa kuwa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mimi nawashukuru sana na yale ambayo tulipishanapishana humu ndani kwa sababu ya kutokuelewana, kwa kweli haikuwa kwa makusudi, ilikuwa bahati mbaya mtusamehe, hasa sisi tunaokaa kwenye Kiti hiki. Hatuwezi kufanya maamuzi yetu bila kukanyaga vidole vya watu na wala hatukanyagi kwa nia mbaya. Kwa hiyo, mtusamehe tu bure. Mtusamehe bure kwa sababu hatuna hata nia mbaya.

Kwa hiyo, nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge tujenge tabia hii, hivyo ndivyo Mabunge yote yalivyo. Fanyeni utafiti, zungumza kwa hoja unayoiamini na uweze ku-support kile kitu unachokiamini. Baada ya hapo, usitengeneze uadui na mtu yejote. Kwa hiyo, huo ndiyo wosia wangu.

Waheshimiwa Wabunge, naona kuna matangazo mengine yanakuja *last minutes*. Mwenyekiti wa Bunge Sports Club anasema, anaomba niwatangazie wachezaji watakaotarajia kwenda kwenye mashindano ya mpira wa miguu na pete kama ilivyo chini, orodha ya wachezaji wanaotarajia kwenda kwenye michezo Arusha kati ya tarehe 14 na 19 ni kesho kutwa tu.

Mpira wa miguu ni Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Joshua J. Nassari, Mheshimiwa Dkt. Hamis A. Kigwangala, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu na Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani. (Makofi)

Watumishi ni Ndugu Carlos Kidiru, Ndugu Michael Kadebe Ndugu Paul Chima, Ndugu Mark Tanda, Ndugu Waziri Kizingiti, Ndugu Christopher Kanonyele, Ndugu Abeid Kikula na Daktari wa timu. (Makofi)

Mpira wa pete, Wabunge watakaohusika, ni Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Neema M. Hamid na Mheshimiwa Susan L. Kiwanga. (Makofi)

Watumishi watakuwa Restuta Michael na Justina Shauri. Kwa hiyo, nadhani mnafahamu hiyo safari yenu ikoje. Baada ya kusema hayo, naomba tusimame kwa Wimbo wa Taifa.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba  
Wimbo wa Taifa)*

**SPIKA:** Leo mmeimba! Maana siku nyingine huwa mnakiachia kile chombo kidogo wala hakina hata sauti.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutokuwa na matangazo mengine, naomba niwatakie kheri kubwa sana katika Siku Kuu ya Krismasi na mwaka mpya na ninapenda nahirishhe kikao hiki mpaka tarehe 29 Januari, 2013 Saa Tatu Asubuhi hapa Dodoma.

*(Saa 12.30 jioni Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 29 Januari, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*

## VIAMBATISHO

### HOJA YA KUFANYA MABADILIKO KATIKA HOJA JUU YA KUITAKA SERIKALI KUCHUKUA HATUA DHIDI YA WATANZANIA WALIOFICHA FEDHA HARAMU NJE YA NCHI

[Kanuni ya 57(1)(b), 57(2), 57(7) na 58(1)]

---

1. **Mheshimiwa Spika**, Hoja iliyowasilishwa katika maelezo ya Mhe. Kabwe Zuberi Zitto (Mb) inahusu matumizi ya Sheria mbalimbali za kijinai. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Kanuni ya Adhabu (**Penal Code, Cap.16**); Sheria ya Mapato ya Kijinai (**Proceeds of Crime, Cap.256**); Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai (**Mutual Assistance in Criminal Matters Act, Cap.254**); Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha (**Banking and Financial Institutions Act, Act No.6/2006**); Sheria ya Ushahidi (**Evidence Act, Cap.6**); Sheria ya Mwenendo wa Jinai (**Criminal Procedure Act, Cap.20**); Sheria ya Kudhibiti Uhaliwa wa Uhujumu Uchumi (**Economic and organized Crime Control Act, Cap.200**); na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (**Sheria Na.11/2007**).
2. Serikali kuitia vyombo vyake vya uchunguzi pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa vinaendelea na uchunguzi wa jambo hili. Aidha, ofisi yangu ilikwishawasiliana na mamlaka za kisheria za nchi ya Uswisi kuhusu suala hili. Suala hili bado halijafikia tamati. Hata hivyo, Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai ina masharti ya kutaja majina ya wenyewe Akaunti hizo na kutoa maelezo ya makosa yanayowahu.
3. Kutokana na maelezo hayo, ninatarajia kupendekeza mabadiliko yafuatayo katika hoja iliyotolewa:
  - (a) Pendekazo la kwanza kwenye hoja liondolewe kwa kuwa vyombo na Mamlaka za Uchunguzi nchini zinalishughulikia jambo hili kwa misingi ya Sheria zilizopo;
  - (b) Kuliondoa pendekazo la pili;
  - (c) Pendekazo la tatu liondolewe. Pendekazo linavunja Msingi wa Usiri wa Mabenki na wateja wao. Watuhumiwa wa uhalifu watashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria zinazoainisha makosa watakayotuhumiwa nayo. Aidha, ni ukiukwaji wa kifungu cha 7 cha Sheria ya **Foreign Exchange Act**;
  - (d) Pendekazo la nne liondolewe. Hii ndiyo kazi ya **TAKUKURU, Financial intelligence Unit na Kamati ya Taifa (The National Multi-Disciplinary Committee on Anti-Money Laundering)** ambavyo ni vyombo vilivyoanzishwa chini ya Sheria ya **Anti-Money Laundering Act**;
  - (e) Pendekazo la tano lisomeke kwamba:-

"Serikali itoe taarifa kuhusu uchunguzi wa tuhuma za walioficha fedha nje ya nchi katika Mkutano wa 11".

(f) Pendelekezo la sita linahusu sera. Linahitaji kufanyiwa utafiti wa kutosha ili kuamua kama inafaa kuanzisha kodi ya aina hiyo. Ninapendelekezo pendelekezo lisomeke kama ifuatavyo:-

*"Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha kodi iitwayo "financial transaction tax" na kuweka kiwango cha kodi hiyo."*

(g) Pendelekezo la saba lifutwe, hoja iliyopo mbele ya Bunge ni kuitaka Serikali kuchukua hatua dhidi ya Watanzania walioficha fedha haramu nje ya nchi na haihusiani na utaratibu wa kuagawa vitalu vyta utafutaji mafuta na gesi. Suala la utafutaji wa mafuta na gesi ni suala tofauti kabisa ambalo linashughulikiwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria ya (**Petroleum Exploration and Production Act, Cap.328**) na taratibu za kutunga Sheria ya Gesi zinaendelea na masuala haya yote yatakuwa yameainishwa ipasavyo. Hoja ya mambo hayo inapaswa kuwa mahsusii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

#### **MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

